# Nipashe

Alhamisi Novemba 7, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580069

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Askari polisi watupiwa lawama kifo cha mtoto aliyekufa maji

UKURASA 3




UKURASA 13

# Sarakasi uchaguzi mitaa zazidi kunoga

• **Wagombea** Chadema wamvaa DED, mwingine adaiwa kuuawa, viongozi wawekwa lupango, Kamati Kuu kujifungia, Lipumba atoa tamko... *Endelea uk.2*



Distributed via ippmedia



Baadhi ya wagombea wa uchaguzi wa serikali za mitaa waliokwama kuteuliwa kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), wakielekea katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Itilima, mkoani Simiyu jana, ili kupatiwa ufafanuzi. **PICHA NDOGO:** Msimamizi wa uchaguzi wa wilaya hiyo, Amina Mbwambo (kulia), akipokea malalamiko yao. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

## Bangi nchini pasua kichwa

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Mbunge ataka mawaziri wabanwe uhujumu uchumi

UKURASA 2


MICHEZO ZAHERA ACHOMOA BETRI YANGA UK.32

MAONI, KATUNI UK.6



Machinga wa eneo la barabara ya Soko Kuu jijini Mwanza na eneo la Shule ya Sekondari Pamba wakiwa wamefunga barabara ya Pamba jana, wakipinga kauli ya Mkurugenzi wa Jiji hilo, Kiomoni Kibamba iliyowataka wahamie eneo la soko jipya lililopo mtaa wa Mbugani. **PICHA: ROSE JACOB**

## Mbunge ataka mawaziri wabanwe uhujumu uchumi

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MBUNGE wa Manyovu (CCM), Albert Ntabaliba, amesema ni wakati mwafaka sasa kwa mawaziri, wakuu wa wilaya na wakurugenzi watakaobainika kushindwa kusimamia miradi ya maendeleo, washtakiwe kwa kuhujumu uchumi.

Amesema ni jambo la kushangaza viongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru wanabaini ufisadi katika miradi ya maendeleo wakati waziri, mkuu wa wilaya na mkurugenzi wanaohusika na mradi huo hawakugundua.

Aliyasema hayo bungeni mjini Dodoma wakati akichangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21.

"Tulitunga sheria ya uhujumu uchumi, sasa naomba Spika iingie ofisini iwahusu mawaziri kwa sababu nao wanashindwa kusimamia fedha wanazozitoa. Haiwezekani Mwenge upite katika eneo la mradi kwa muda wa dakika tano tu ugundue tatizo wakati DC (Mkuu wa Wilaya) mkurugenzi, waziri wapo," alisema.

"Wizara ilikuwa wapi? Mkuu wa wilaya alikuwa wapi? Wataalamu walikuwa wapi? Mkuu wa Mkoa alikuwa wapi? Waziri wa kisekta alikuwa wapi?" Alihoji Ntabaliba.

Mbunge huyo, maarufu kama Obama, alisema viongozi hao wanapaswa kushtakiwa kuhujumu uchumi kwa kushindwa kubaini upungufu katika mradi wa maendeleo ulioko katika maeneo yao.

Alisema ni wakati mwafaka sasa kwa sheria hiyo itoke kwa wafanyabiashara iende kwa wataalamu hususan wale ambao watashindwa kusimamia miradi ya maendeleo na kwamba wananchi ndio wanaokatwa katika kodi.

Wabunge wengine, wakichangia mpango huo, waliitaka serikali kuweka mkazo katika kilimo, uvuvi, ufugaji ili kuongeza pato la taifa na kufikia Tanzania ya viwanda.

INAENDELEA UK. 8

# Sarakasi uchaguzi mitaa zazidi kunoga

**Na Waandishi Wetu**

MADAI ya kufanyiwa rafu katika mchakato unaoendelea wa uchaguzi wa serikali za mitaa, yameendelea kutolewa na vyama vya upinzani, huku Kamati Kuu ya chama kikuu cha upinzani nchini, Chadema, ikitarajiwa kukutana leo kuamua hatua za kuchukua.

Distributed via ippmedia

Imeelezwa kuwa katika kikao hicho maalum cha dharura, kutakuwa na ajenda hiyo ya taarifa ya uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji kwa mwaka 2019.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa chama hicho, Tumaini Makene, ilieleza kuwa kikao hicho kitafanyika chini ya Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, kwa mujibu wa Ibara ya 7.7.15 ya Katiba ya chama hicho toleo la mwaka 2016.

Makene alieleza katika taarifa hiyo kuwa baada ya kikao hicho, Kamati Kuu itakutana na wabunge wa chama hicho.

Wakati Kamati Kuu ya Chadema ikijipanga kukutana leo, zaidi ya wagombea 100 wa ngazi ya vijiji na vitongoji wa chama hicho wilayani Itilima mkoani Simiyu, jana walilazimika kwenda Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo ili ya kuonana na Msimamizi wa Uchaguzi wa Wilaya kuwasilisha malalamiko yao.

Wagombea hao ambao hawakuteuliwa kugombea nafasi hizo, walifika katika ofisi hiyo kwa lengo la kuwasilisha malalamiko yao, wakidai kuhujumiwa na wasimamizi wasaidizi kwa mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutopokewa kwa fomu zao za pingamizi la kutoteuliwa.

Wakiwa na fomu hizo, wagombea hao walifika kwa msimamizi huyo majira ya saa nne asubuhi, wakiongozwa na Katibu wa Chadema katika wilaya hiyo, Goleha Lazaro.

Mbele ya msimamizi huyo, Lazaro alidai waliamua kuchukua uamuzi huo kutokana na wasimamizi wasaidizi wa maeneo yao kukataa kupokea fomu hizo kinyume cha utaratibu.

Alidai wasimamizi hao wamekataa kupokea fomu zao mpaka wapate maelekezo kutoka kwa msimamizi wa uchaguzi wilaya.

"Kwenye uteuzi tumekutana na hujuma nyingi sana, hawa wasimamizi wasaidizi wamekuwa wakifunga ofisi na kuondoka, wakati mwingine ofisi zinakuwa wazi, lakini wahusika hawapo," Lazaro alisema.

"Sasa tumekuja kwako msimamizi wa uchaguzi wilaya, tunataka ufafanuzi, ni wapi kwenye sheria inasema wasimamizi wasaidizi wanatakiwa kupokea maelekezo kutoka kwako ili wapokee fomu za pingamizi?" Lazaro alihoji.

Akijibu hoja za walalamikaji hao, Mbwambo alikiri wasimamizi wasaidizi hawatakiwi kukataa kupokea fomu hizo na wala hakuna kipengele kwenye sheria ya uchaguzi huo kinachosema lazima wapate kwanza maelekezo kutoka kwake.

Alisema kama kuna msimamizi msaidizi anakataa kupokea fomu hizo, anakiuka sheria na kanuni za uchaguzi huo, kisha akawataka wagombea kurudi tena kwa wasimamizi wasaidizi kukabidhi fomu hizo ili zifanyiwe kazi.

Kabla ya kukutana na wagombea hao, msimamizi huyo aliwaambia waandishi wa habari kuwa katika wilaya hiyo, uteuzi wa wagombea ulifanyika vizuri, akibainisha kuwa wagombea 76 wa nafasi ya uenyeviti wa kijiji kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) wamepita bila ya kupingwa.

Alisema wilaya hiyo ina vijiji 102. Kati yake, 26 waliteuliwa wagombea kutoka CCM, CUF, Chadema na UDP ambao watalazimika kupigiwa kura.

Kwa upande wa ngazi ya kitongoji, msimamizi huyo alisema wagombea 302 wa CCM wamepita bila ya kupingwa kati ya vitongoji 586 vya wilaya hiyo.

Wilayani Meatu, wagombea wa CCM wamepita bila kupingwa katika vijiji 98 kati ya 105 na vitongoji 645 kati ya 681.

**MGOMBEA CHADEMA AUAWA**

MKAZI wa Kijiji cha Itunya Kata ya Kapalamsenga Tarafa ya Karema wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi, Dominic Mwile(54), ambaye aliyekuwa ameteuliwa kuwa mgombea wa nafasi ya wenyekiti katika Kitongoji cha Itunya kupitia CHADEMA, anadaiwa ameuawa kwa kupingwa na silaha za jadi na askari mgambo wapatao 15 wa wa Kata ya Karema.

Kwamujibu wa ofisa mtendaji wa kijiji hicho, Sofia Lumbwe, tukio hilo lilitokea juzi usiku katika Kijiji hicho jirani na nyumba aliyokuwa akiishi na familia yake.

Alisema kabla ya tukio hilo yeye kama ofisa mtendaji wa Kijiji aliwapokea askari mgambo wapatao 15 waliokua wametoka makao makuu ya tarafa hiyo katika Kata ya Karema ambao walifika ofisini hapo majira ya saa 12 jioni.

Alisema kuwa walimueleza kuwa lengo lao kufika kijijini hapo walikuwa wamekwenda kufanya shughuli ya kulinda usalama kwenye kijiji hicho kwa kile walichodai kuna uwezekano wa kutokea vurugu kwa kuwa wagombea wa nafasi ya uongozi wa Serikali ya Kitongoji cha Itunya majina ya wagombea waliowengi yameondolewa likiwemo jina la Mwile.

**TAMKO LA LIPUMBA**

Wakati hali ikiwa hivyo mkoani Simiyu, Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, jana aliitaka serikali kuruhusu kuongeza muda wa siku nne ili kutenda haki kwa wananchi waliojitokeza kusaka nafasi za uongozi.

Alisema kuna haja wagombea wote waliojaza fomu na kudhaminiwa na vyama vya siasa kuwania uchaguzi wa serikali za mitaa, wateuliwe kugombea nafasi hizo.

Akisoma tamko la chama hicho jijini Dar es Salaam jana, Prof. Lipumba alidai kumekuwa na upendeleo kwa CCM, ambacho wagombea wake katika maeneo mengi wamepita bila kupingwa.

"Kwa kuwa kumekuwa na upungufu wa wazi wa kupendelea wagombea wa CCM wapite bila kupingwa, wagombea wote waliojaza fomu na kudhaminiwa na vyama vya siasa wateuliwe kugombea nafasi walizoazimia kugombea," Prof Lipumba alisema.

Alidai kuwa kama serikali inataka mgombea wa CCM wa nafasi ya mwenyekiti wa kitongoji, kijiji na mtaa apite bila kupingwa, ni wazi itataka mgombea wa CCM wa urais, ubunge na udiwani apite bila kupingwa katika uchaguzi

INAENDELEA UK. 8

# Abbas afafanua maagizo ya Rais

**Na Romana Mallya**

MSEMAJI Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, amefafanua kuhusu madai ya Rais kuingilia utendaji wa Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Baada ya kumwapisha Charles Kichere kuwa CAG jijini Dar es Salaam Jumatatu, Rais John Magufuli alitoa maagizo kwa bosi huyo mpya wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, ambayo baadhi ya wachambuzi walidai ni kuingilia utendaji wake.

Jana, akijibu maswali ya waandishi wa habari kuhusu miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, Dk. Abbas alisema Rais hajaingilia uhuru wa Ofisi ya CAG kwa kutoa maagizo kwa Kichere.

Alisema Rais anapomteua mtendaji yeyote, anamteua kwa mamlaka aliyopewa na Ibara ya 36 ya Katiba ya Tanzania na anapompa majukumu hatungi.

"Watanzania tusikosee, hili nimekuwa nikilisisitiza sana ndani ya hii miaka minne, tusikosee kuwa na uhuru wa mawazo, kitaaluma kwa kusikiliza watu wanaoitwa wachambuzi wa mambo.

"Mfano, magazeti ya leo (jana), wagombea wa upinzani kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa wote wamekatwa. Ukiuliza ni nani, utaambiwa kwa mujibu wa wachambuzi wa mambo.

"Lakini nenda kwenye ukweli, tuna vitongoji zaidi ya 64,000, nikikuuliza zaidi ya vitongoji 64,000, wangapi wamekatwa, wangapi waligombea kwa maana ya kupeleka fomu, wangapi walijitoa, lakini ukiwauliza wachambuzi wa mambo wanakwambia sarakasi, hakufai wamekatwa wote," alisema.

Dk. Abbas alisema si CAG Kichere peke yake aliyepewa maagizo na Rais, akibainisha kuwa hata Rais mwenyewe ana masharti ya kazi yake kikatiba, sawa na ilivyo kwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na wengine.

"Nenda kifungu cha nne cha Sheria ya Huduma, (mimi) nina masharti yangu kuanzia sifa za kuteuliwa, sasa Rais akikukumbusha nenda kafanye kazi, ndiyo anakuingilia uhuru wako wa kazi?

"Achana na wachambuzi wa mambo, jiridhishwe mwenyewe, tuache habari za alisema, alisisitiza, akaongeza, akafafanua. Yaani Rais kumtaka CAG akafanye kazi yake ya ukaguzi ambayo ipo kwenye Ibara 144, hizo ni kazi zake CAG kuanzia kifungu cha sita. Kwa hiyo, kumwambia kafanye na usipofanya ujue tutakuondoa, amekosea nini?

"Tulitaka tumwambie utakwenda kuangalia utakachoona? Tunataka serikali ya namna hiyo? Hapana! Unapewa hadidu

INAENDELEA UK. 8



Wananchi wa kijiji cha Mkunywa katika Kata ya Madibira wilayani Mbarali, wakifunika mwili wa mtoto, Jidamabi Lwenge (15), baada ya kuuopoa kutoka katika Mto Lyandembela, Jumatatu Novemba 4, ambamo anadaiwa kutumbukia wakati alipokuwa anafukuzwa na askari wa Jeshi la Polisi, waliomtuhumu kuchungia mifugo kwenye mashamba ya chama cha ushirika wa wakulima wa mpunga Madibira. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Polisi lawamani kifo cha mtoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kijiji cha Mkunywa katika Kata ya Madibira wilayani Mbarali, Mkoa wa Mbeya, wamelituhumu Jeshi la Polisi kusababisha kifo cha mtoto, Jidamabi Lwenge (15), ambaye anadaiwa kufa maji alipotumbukia mtoni wakati akifukuzwa na askari.

Askari hao walikuwa wanamtuhumu kuchungia mifugo kwenye mashamba ya Chama cha Ushirika wa Wakulima wa Mpunga wa Madibila (Mamcos).

Wakizungumza na waandishi wa habari kijijini hapo, wananchi hao walidai kuwa Lwenge pamoja na mwenzake mmoja walikuwa walienda eneo hilo kwa ajili ya kunywesha mifugo ndipo wakaanza kufukuzwa na askari hao ambao walikuwa wamebeba silaha za moto.

Mmoja wa wananchi hao, Mwigulu Ucheyeki, alisema mtoto mmoja ambaye alifanikiwa kuwatoroka askari hao, alienda kutoa taarifa nyumbani kwamba mifugo imekamatwa, lakini walipomuuliza kuhusu mwenzake aliko, alisema hajui alikoelekea.

Alisema baada ya kupewa taarifa hizo, alienda Polisi kwa ajili ya kukomboa mifugo, na alipofika alitozwa faini ya Sh. 2,000,000 na akarejea nayo nyumbani, lakini walipojaribu kumtafuta Lwenge, hakuonekana.

"Mchungaji wangu alinieleza kuwa walitishiwa na bunduki kisha wakaanza kukimbia kila mtu uelekeo wake, ikabidi tumuulize maeneo walipokuwa, na ndipo tukamkuta Lwenge siku ya pili mwili wake ukiwa unaning'inia hapa akiwa ameshafariki," alisema Ucheyeki.

Alisema wamekuwa wakinyanyaswa mara kwa mara na askari hao, ambao wanakamata mifugo hata kama haipo kwenye mashamba ya ushirika ili walipe faini.

Naye Daniel Limbe, alisema askari hao wanawafanya wafugaji wa Kijiji hicho kama kitega uchumi kwa kukamata mifugo yao mara kwa mara na kuwatoza faini, huku akidai kuwa wakati mwingine hawapewi stakabadhi za malipo.

Alisema kwa sasa hawana amani katika eneo hilo kutokana na manyanyaso wanayoyapata kutoka kwa askari hao, ambao huwa wanawatoza shilingi 50,000 kwa kila ng'ombe anayekamatwa na askari, na kwamba wakati mwingine huwa wanalazimisha hata kama mifugo hiyo haipo kwenye mashamba ya ushirika.

Alisema kutokana na tukio la kifo cha mtoto Jidamabi, wanaiomba serikali kuingilia kati kutatua mgogoro uliopo baina yao akidai kuwa umefikia hatua mbaya ambayo sasa imeanza kugharimu maisha yao.

"Hatujawahi kuambiwa kuwa hatutakiwi kufuga katika kijiji hiki, na wala hakuna kiongozi aliyewahi kutuelimisha kuwa tunatakiwa tuchungie sehemu fulani...sasa tunaomba serikali ituelekeze kama hatutakiwi kufuga ili tutafute njia nyingine ya kuishi," alisema Limbe.

Katibu wa Chama cha Wafugaji wa Wilaya ya Mbarali, Matagili Mbigili, aliwataka wafugaji hao kuwa watulivu katika kipindi hiki ambacho wanafuatilia tatizo hilo, huku akisisitiza kuwa serikali ya awamu ya tano ni sikivu na itawasaidia.

Aliwataka wananchi hao kuendelea kushikamana hasa katika kudai haki yao, na kwamba yeye kama kiongozi atahakikisha suala hilo linaisha na wafugaji wanapata haki.

**KAULI YA POLISI**

Akizungumzia tukio hilo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alikana askari wake kusababisha kifo cha mtoto huyo kwa madai kuwa alikufa baada ya kuzidiwa na maji wakati akivusha mifugo.

Alisema baada ya tukio hilo, wananchi hao walitoa taarifa katika Kituo cha Polisi cha Madibira na ndipo waliposhirikiana kuutafuta mwili, na kwamba baada ya kuupata familia ilikabidhiwa kwa ajili ya kuendelea na taratibu za mazishi.

Distributed via inmedia

# Bangi nchini pasua kichwa

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MATUMIZI ya dawa za kulevya aina ya bangi, yametajwa bado ni tatizo nchini, huku Mkoa wa Mara ukiwa ni kinara kilimo cha zao hilo ikifuatiwa na Tanga.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, ndiye aliyebainisha hayo bungeni jana, wakati akiwasilisha taarifa ya hali ya dawa za kulevya kwa mwaka 2018.

"Pamoja na jitihada zilizofanywa na serikali katika kupambana na dawaza kulevya nchini, bangi imeendelea kuwa tatizo kubwa nchini, mikoa ambayo inaonekana kuathirika zaidi na kilimo cha bangi ni pamoja na Mara, Tanga, Morogoro, Arusha, Kagera na Ruvuma," alisema Mhagama na kuongeza:

"Kwa kipindi cha mwaka 2018 juhudi za vyombo vya dola kwa kushirikiana na wananchi zilifanikisha ukamataji wa tani 24.3 za bangi zikiwahusisha watuhumiwa 10,061."

Alisema dawa za kulevya aina ya mirungi nayo imeendelea kutumiwa nawatu wa rika mbalimbali, kwamba kwa mwaka 2018 vyombo vya dola vilikamata tani 8.97 za mirungi zikiwahusisha watuhumiwa 1,186.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2018, kesi 7,592 zikiwa na watuhumiwa 10,979, zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali, kesi 7,174 zilizowahusisha watuhumiwa 11,045 ziliendelea kusikilizwa.

"Serikali imeendelea kutoa huduma za tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevya, jumla ya vituo sita vilivyopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Dodoma viliendelea kutoa huduma, hadi mwaka 2018 zaidi ya watumiaji 8,000 waliendelea kupatiwa huduma za Methadone katika vituo hivyo," alisema Mhagama.

Mhagama alisema mwaka 2018, dawa za kulevya aina ya Cocaine kilo 8.9 zilikamatwa, na watuhumiwa 156 walifikishwa katika mikono ya sheria.

Alisema kwa mujibu wa Shirika la Kimataifa la Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC), Tanzania ilipunguza uingizaji wa dawa za kulevya nchini aina ya Heroine kwa asilimia 90.

Naye, Kamishna wa Kinga na Tiba kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini, Dk. Peter Mfisi, alisema serikali hainunui dawa za Methadone bali zinanunuliwa na wafadhili kutoka Canada, thamani yake ni Dola za Marekani 1,500 kwa kilo moja.

Alisema India kilo moja ya Methadone ni Dola za Marekani 650 hadi 700, kwa mwaka matumizi ya dawa hiyo nchini ni kilo 300.

Dk. Mfisi alisema kilo moja ya Methadone inahudumia watu 600 hadi 700 kwa mwezi.

# Madini sasa kuanza kusafishwa nchini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema itaanza kusafisha dhahabu nchini ili kuongeza thamani, hivyo kusaidia kuongeza pato la taifa na kuhifadhi fedha Benki Kuu (BoT) kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Katika kutekeleza hilo, imesema itajenga kituo cha kuchakata dhahabu jijini Dodoma na Geita kwa ajili ya kusafisha dhahabu na kuongeza pato la taifa kutokana na madini hayo.

Akizungumza katika mkutano wa ufunguzi wa Wiki ya Asasi za Kirais (Azaki), Naibu Waziri wa Madini, Stanislaus Nyongo, alisema dhahabu inayopatikana hivi sasa ni asilimia 80. Hivyo wanahitaji isafishwe nchini na kufikia asilimia 99.9 ili BoT ipate fedha kutokana na dhahabu hiyo.

Mbali na fedha kupelekwa BOT, pia wakianza mchakato huo, watakuwa na uwezo wa kuanza kuuza kwa gramu tofauti kwa wadau na kuzidi kuongeza pato la taifa.

Alisema lengo la mipango mikakati hiyo ni kuongeza asilimia ya pato litokanalo na madini ambalo awali ilikuwa asilimia.3.5, lakini hivi sasa limefikia asilimia tano kutokana na usimamizi mzuri wa serikali ya awamu ya tano.

Hata hivyo, alisema hadi ifikapo 2025, ifike asilimia 10 la pato litokanalo na madini.

Naibu waziri huyo alisema awali pato la uchumi litokanalo na madini lilikuwa dogo, lakini toka wameweka usimamizi mzuri katika sekta hiyo na kupelekea kufikia asilimia hizo.

Kutokana na hilo alisema wameamua kuanza kusafisha dhahabu hapa nchini lengo likiwa kila pato linalopatikana pale wanapovuna dhahabu fedha inachukuliwa na serikali.

Hatua hiyo pia alisema imetokana na kuanzishwa kwa Tume ya Madini ambayo inaundwa na watu kutoka sekta tofauti ambayo inahusika kutoa leseni za wachimbaji wadogo. Alisema lengo la kufanya hivyo ni pamoja na kutaka kuondoa ukiritimba uliokuwa ukileta kelele nyingi kwa wachimbaji wadogo.

"Tumeamua sasa kuunda tume hiyo lengo ni kuondoa malalamiko kwa wachimbaji jambo ambali hivi sasa tunakwenda vizuri," alisema Nyongo.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakipita jirani na ujenzi unaoendelea wa barabara za mpishano (Ubungo Interchange), katika eneo la mataa ya Ubungo, jijini humo, jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Watuhumiwa sugu ujambazi wauawa Dar

**Na Mary Geofrey**

JESHI la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, limewaua watu wawili wanaodhaniwa kuwa ni majambazi sugu, akiwamo aliyefahamika kwa jina la 'Kambale' ambaye alikuwa akitafutwa kwa muda mrefu.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wanahabari na kusema kuwa 'Kambale' alijipatia umaarufu wa jina hilo kwa sababu alikuwa akikamatwa na kutoroka.

"Tunawashukuru Watanzania wanaendelea kutoa taarifa za uhalifu kwa Jeshi la Polisi, usiku wa kuamkia leo (jana) tumekamata pisto (bastola) moja na majambazi wawili waliokuwa wakiwahangaisha wananchi," alisema Mambosasa na kuongeza:

Distributed via inmedia

"Wameangushwa chini (wameauawa). Mmoja alikuwa akijiita Kambale kutokana na kuwaponyoka askari kila alipokamatwa, ametesa sana wakazi wa Madizini, Ukonga na maeneo mengine."

Aliongeza kuwa 'Kambale' alikuwa akishirikiana na wenzake wanakodi pikipiki, wanaielekezea sehemu alipo 'Kambale', wakifika alikuwa anawachoma kisu na kukimbia na pikipiki.

"Amekuwa akiwateka na kuwaua madereva bodaboda, kila alipokuwa akikamatwa anateleza na kuwatoka askari kama vile samaki aina ya Kambale, lakini mwisho wake na yeye ametangulia mbele za haki," alisema Mambosasa.

Mbali na hilo, Mambosasa alisema jeshi hilo limeimarisha ulinzi katika maeneo yote ya jiji hilo, wakati wanapotarajia kupokea wageni wanaoshiriki mkutano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Sadc) unaotarajiwa kufanyika kuanzia kesho jijini Dar es Salaam.

Mambosasa aliwatahadharisha wakazi wote wa jiji hilo kuwa endapo watafanya utapeli kwa wageni hao sifa itakayobebwa ni ya Watanzania wote na kwamba Jeshi hilo halipo tayari kuona sifa ya Tanzania inachafuliwa.

"Tumejipanga na doria zinaendelea mtaani kwa ajili ya kikao cha Sadc, wageni wetu wanaoingia kuanzia Airport (uwanja wa ndege), mahali watakapofikia hadi kwenye kikao watakuwa salama," alisema na kuendelea:

"Fukwe zote na eneo la mkutano tumehakikisha usalama upo. Kila mmoja anatakiwa awe mlinzi wa mwenzake, wanaofanya ujanja ujanja toeni taarifa, tutawashughulikia, tusikubali mtu mmoja akachafua sifa ya nchi yetu."

# Mabalozi waahidi kutangaza uwekezaji nchini

**Na Mwandishi Wetu**

MABALOZI wapya waliloteuliwa na Rais John Magufuli wameahidi kufanya kazi kwa karibu na Mamlaka ya Uwekezaji wa Ukanda Maalum wa Uchumi (EPZA) ili kusukuma mbele diplomasia ya uchumi na kuwavutia wawekezaji sekta ya viwanda.

Akizungumza kwa niaba ya mabalozi wengine baada ya kutembelea mamlaka ya EPZA na baadhi ya viwanda vilivyo katika eneo maalum la uwekekezaji, Balozi Maimuna Tarishi, alisema moja ya jukumu katika nchi wanazoenda kufanya kazi ni kuzitangaza fursa za uwekezaji zilizopo Tanzania.

"Kuvutia wawekezaji kwenye sekta ya viwanda ni moja ya jukumu la msingi ambalo tutaenda kufanya katika nchi tutakazoenda kufanya kazi," alisema wakati akitoa shukrani baada ya wasilisho lililofanywa na Mkurugenzi EPZA, James Maziku. Alisema, ziara yao EPZA wamejifunza na kuhabarishwa namna watakavyotangaza fursa na vivutio mbalimbali vya uwekezaji hasa kwenye viwanda nchini.

Balozi Tarishi alisema kuwa diplomasia ya uchumi ni muhimu sana katika kufikia malengo ya kujenga uchumi wa viwanda na kuifanya nchi kuingia katika kipato cha kati mwaka 2025.

Mabalozi walifurahishwa na uwekezaji mkubwa uliofanywa na kampuni ya Tooku inayozalisha nguo aina ya `jeans' na kuuza katika soko la Marekani na kuajiri zaidi ya Watanzania 2,600.

Kiwanda hicho kinatarajiwa kuongeza uzalishaji na kufikia jeans 800 kwa mwezi ifikapo mwezi Machi mwakani lengo pia likiwa kuzalisha nguo 1,000 kwa mwezi.

Naye balozi mpya na Mkurugenzi wa zamani wa Usalama wa Taifa, Modestus Kipilimba, alipongeza jitihada zinazofanywa na EPZA kuvutia wawekezaji katika viwanda, hata hivyo, wasiwasi wake ni kiwanda kununua malighafi nje ya nchi kuwa inakosesha fursa wakulima wa nchini.

Akijibu hoja mbalimbali za mabalozi, Mkurugenzi wa EPZA, Maziku alisema mwekezaji wa Tooku aliwaambia kuwa ana lengo la kununua malighafi kutoka Tanzania, lakini gharama ni kubwa za kuchakata pamba na kufikia viwango vinavyotakiwa kutengeneza nguo za kuuza marekani.

Alisema ili kuzalisha malighafi nchini kunatakiwa kuwe na viwanda vingi vya aina ya Tooku ambavyo vitachukua malighafi nyingi na kuvutia wawekezaji wengi kuchakata pamba kwa ajili ya utengenezaji wa nguo aina ya jeans.

Balozi Gaudence Milanzi kwa upande wake, alisema uendelezaji wa viwanda nchini upo chini ya mamlaka ya EPZA na hivyo ni muhimu kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuvutia wawekezaji zaidi.

"Sisi tunaahidi kushirikiana kwa karibu na mamlaka ya EPZA katika kuzitangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini katika nchi tunazoenda kufanya kazi," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Benki Azania yazindua huduma za kidigitali

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Azania imezindua huduma ya Azania Plus Digital Experience, inayolenga kuwasaidia wateja wake kupata huduma za kibenki mahali popote kwa urahisi kupitia mawakala, simu ya mkononi na huduma ya intaneti kwa saa 24.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Charles Itembe, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi huo, jana jijini Dar es Salaam, alisema anaamini upatikanaji wa huduma za benki haupaswi kuwa mgumu na wenye mihangaiko.

Alisema huduma hiyo itawawezesha wateja wao kutuma na kupokea pesa, kulipa bili kama maji na umeme na kuomba mikopo popote walipo bila kutembelea tawi la benki.

"Wateja wetu wana uhuru wa

INAENDELEA UK.8



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akishiriki katika sala ya kumwombea marehemu kaka yake, Mzee Bakari Majaliwa iliyofanyika katika kijiji cha Nandagala, wilayani Ruangwa, mkoani Lindi jana, kabla ya mazishi yaliyofanyika kijijini hapo. **PICHA: OWM**

# TPA kujenga gati kupokea meli tani 100,000

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Bandari (TPA), inatarajia kujenga gati la kisasa lenye uwezo wa kubeba meli kubwa ya mafuta yenye ujazo wa tani 100,000.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Deusdatus Kakoko, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea Bandari ya Tanga pamoja na uongozi wa bodi hiyo, kwa lengo la kukagua mradi wa upanuzi wa kina cha maji unaoendelea katika bandari hiyo.

Alisema mpango huo ni awamu ya pili ya upanuzi wa bandari hiyo ambao tayari wameshaingia mkataba kwa ajili ya kufanya usanifu, ambao unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 170.

Awamu ya kwanza ya mradi ni uchimbaji wa kina cha maji kutoka mita tano hadi 17 ambao unagharimu Sh. bilioni 17 na kwamba utakapokamilika utahudumia meli kubwa zaidi.

"Kukamilika kwa miradi hii sasa kutawezesha meli kubwa ya aina yoyote duniani kutia nanga katika bandari hii ya Tanga, kuzidi zile zinazotia nanga katika Bandari ya Dar es Salaam," alisema Kakoko.

Alisema kwa sasa Bandari ya Dar es Salaam ina urefu wa kina cha mita 15.5 na malengo ni kuongeza kina hicho na kufika 19.

"Kwa sasa Bandari ya Tanga ndio itakuwa na kina kirefu zaidi kuliko Dar es Salaam na Bandari hii itahudumia meli zenye ukubwa duniani," alisema Kakoko. Alisema tayari Bandari ya Tanga imeshapokea meli kubwa ya mafuta yenye urefu wa mita 220 iliyobeba ujazo wa tani 30,000.

Kwa sasa Bandari ya Tanga ina uwezo wa kuhudumia tani 750,000 kwa mwaka na wanaendelea na mpango wa kuchukua tenda ya tani za ziada 250,000 za mizigo ya wakazi wa mikoa ya Kaskazini zinazohudumiwa na bandari za nchi jirani.

Alisema mipango mikakati ya miaka 10 ya TPA ni bandari hiyo kuhudumia tani 30,000 ifikapo 2028, wakati uwezo wa bandari zote nchini ni kuhudumia tani milioni 100.

Mwenyekiti wa Bodi ya TPA, Prof. Ignas Rubaratuka, alisema fedha zote zinazotumika katika miradi hiyo ni za ndani isipokuwa kwa Bandari ya Dar es Salaam inategemea fedha za mikopo na mchango wa serikali.

"Menejimeti ya TPA ina mpango kabambe kuhakikisha miundombinu ya bandari inaboreshwa kwa asilimia 100 ili kuhakikisha huduma zinaboreshwa na kuongeza mapato," alisema Prof. Rubaratuka.

Meneja wa Bandari ya Tanga, Ajuaye Msese, alisema kukamilika kwa miradi hiyo kutapunguza muda wa kupakua na kupakia mizigo hali itakayovutia wawekezaji wengi kutumia bandari hiyo. "Bandari ya Tanga, itaongeza mapato yake kutokana na shughuli zitakazokuwa zinafanywa na bandari yetu," alisema Msese.

Distributed via ippmedia






# Kortini kufanya ugavi bila usajili

**Na Hellen Mwango**

WATU 18 wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, wakikabiliwa na shtaka la kufanya kazi za ununuzi na ugavi bila kusajiliwa na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSTB).

Washtakiwa hao ni Jema Mbugi, Julieth Daniel, Jeremiah Mafuru, Lucy Wanne, Odillo Benedict, Bibiana Romanus, Bahati Wonnandi, Raphael Waryana, Joseph Mhere na Victor Kilonzo.

Wengine ni Moshi Mohamed, Avitus Rutayuga, Esther Reyemamu, Ruth Mwaipyana, Beatrice Mushi, Julieth Mwihambi, Geogre Lyimo na Estonia Kalokola

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao na Mwendesha Mashtaka wa PSTB, Suleiman Mzava mbele ya Hakimu Mkazi Hudi Hudi. Mzava alidai kuwa wanakabiliwa na shtaka la kufanya kazi za ununuzi bila kusajiliwa na bodi hiyo.

Mzava alidai kuwa kati ya Februari 11 na 15, mwaka huu katika ofisi mbalimbali jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao walikutwa wakifanya kazi za ununuzi na ugavi bila kusajiliwa na PSTB, huku wakijua kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Wakati mashtaka hayo yanasomwa, washtakiwa Mehere, Mohamed, Mwaipyana na Mwihambi hawakuwapo mahakamani na upande wa Jamhuri uliomba mahakama itoe hati ya kukamatwa kwao. Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba mahakama kupanga tarehe ya washtakiwa hao kuzomewa maelezo ya awali.

Hata hivyo, washtakiwa walikana mashtaka hayo, Jamhuri haikuwa na pingamizi la dhamana.

Hakimu Hudi aliwataka washtakiwa kila mmoja kuwa na mdhamini mmoja mwenye barua kutoka Ofisi ya Serikali ya Mtaa na awe na kitambulisho cha taifa atakayetia saini hati ya dhamana ya Sh. milioni tano. Washtakiwa waliachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza masharti na kesi hiyo imeahirishwa hadi Novemba 21, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Asasi zikitumika vizuri zina mchango mkubwa

**ASASI** zisizo za kiserikali zina mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa kwa namna mbalimbali.

Asasi hizi zinafanya mambo mengi na mazuri, hivyo kuisaidia serikali katika mambo mengine ambayo utekelezaji wake una changamoto.

Kimsingi, serikali haiwezi kufanya kila kitu katika kuwaletea wananchi maendeleo, kwa sababu wakati mwingine inakabiliwa na ufinyu wa bajeti.

Kwa hiyo asasi hizo zimekuwa zikichangia katika maendeleo ya uchumi wa taifa ikiwamo kutoa ajira kwa wananchi pamoja na kusapoti miradi kadhaa ya maendeleo ambayo serikali ingetakiwa kuitekeleza kwa kutumia fedha nyingi.

Maadhimisho ya Wiki ya Azaki yanayofanyika jijini Dodoma yamebainisha bila kuacha shaka kuhusiana na namna gani azaki zinatoa mchango mkubwa katika uchumi wa taifa na maendeleo kwa ujumla.

Mambo yaliyobainishwa kuchangiwa na azaki hizo katika uchumi wa taifa ni dhahiri kuwa yangegharimu fedha nyingi za walipakodi, ambazo kwa sasa zinatukuka kutekeleza miradi mbalimbali ikiwamo mikubwa ya kimkakati.

Aliyoyaeleza Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Twaweza, Aidan Eyakuze, kuhusiana na mchango wa Azaki katika uchumi wa taifa, yanaakisi uhalisia.

Akizungumza na wanahabari baada ya kuwasilisha mada ya mchango wa asasi za kiraia kwenye uchumi wa nchi, ikiwa sehemu ya maadhimisho hayo jijini Dodoma juzi, Eyakuze, alisema kwamba katika utafiti walioufanya kwa kipindi ya miaka mitatu 2016-2018, mchango wa asasi za kiraia 16 kwenye uchumi wa nchi ni kiasi cha Sh. bilioni. 236.

Alisema kiasi hicho cha fedha kilichopatikana kutokana na asasi za kiraia kwa kipindi cha miaka mitatu ni sawa na kilo 2,181 za dhahabu zinazosafirishwa na kuuzwa nje.

Pia, kiasi hicho cha fedha ambacho kimechangiwa na asasi hizi 16, kwa kipindi hicho ni sawa na serikali kuingiza watalii 42,316 na kukaa nchini kwa wiki moja au ni sawa na lita 247 milioni za petroli, dezeli na mafuta ya taa, na kuwa katika kipindi cha miaka mitatu 2016/18 kiasi cha kodi ambayo imelipwa na azaki hizo 16 kwa serikali ni Sh. bilioni 19.

Kwamba kiasi hicho cha kodi kilichokusanywa kwa kipindi hicho ni sawa na mapato yatokanayo na maji ya kunywa, vinywaji laini na sigara ya mwaka 2018/19 ambayo yalikuwa ni Sh. bilioni 18.8.

Au kiasi hicho cha kodi kilichokusanywa kinaweza kulinganisha na kodi iliyokusanywa na Mamalaka ya Mapato Tanzania (TRA) 2018/19 katika mikoa ya Rukwa, Lindi, Simiyu, Songwe na Katavi kwa pamoja ambayo makusanyo yao ni Sh. bilioni 21.

Mchango huu ni mkubwa kwa uchumi wa taifa letu, hivyo kwa maoni yetu tunaona kuwa azaki ziendelee kuwa mdau mkubwa wa serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Tunasema hivyo tukiamini kuwa serikali inauona mchango huo na kuuthamini, kwa kuwa unawezesha wananchi na taifa kupata maendeleo na kupaa kiuchumi.


Tunashauri kuwa serikali iendelee kuziwekea azaki mazingira mazuri ya kufanyia kazi, ili ziendelee kuchangia katika maendeleo ya wananchi na uchumi wa taifa.

Kwa upande mwingine, azaki nazo ziwajibike kufanya shughuli zao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za nchi, ili kuepuka kuingia katika migogoro na serikali.

Ni jambo la kutia moyo kusikia kwamba serikali inathamini mchango huo kutokana na kauli iliyotolewa katika maadhimisho hayo na Mratibu wa Asasi za kiraia nchini kutoka Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa- Tamisemi), Denis Londo, kwamba asasi la kirai zina mchango mkubwa kwa taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Barabara hii jijini Mwanza ni kero na hatari kubwa

Na Yasmine Protace

Distributed via ippmedia

**KWANZA** kila mtu anajua pasipo ubishi, kwamba Mwanza ni jiji kubwa na kuna uwezekano mkubwa juu ya ukweli huo.

Hapa jijini Mwanza kuna mlolongo katika barabara zake. Katika Barabara ya Kiloleli, hadi sasa kunakabiliwa na mateso kwa wavukaji kutokana na kasi kubwa ya magari na bodaboda zinazokatiza mahali hapo.

Awali, kabla ya kuwekwa lami kwenye barabara hiyo, magari na bodaboda zilipita katika mwendo wa kawaida na daima hazikuwa na kasi inayoshuhudiwa leo.

Lakini, baada ya kuwapo mabadiliko, barabara hiyo haijawekwa lami na haikuwa na mwendokasi unaoshuhudiwa hivi sasa.Ikumbukwe, ni barabara yenye kona nyingi, hali inayowafanya hata wavukaji kwa miguu, kukumbana na changamoto nyingi wakati wa kutafuta huduma mahali hapo, inayowalazimu kuvuka barabara.

Ni kawaida, kila kukicha tunashuhudia katika barabara hiyo kuwapo daladala barabarani zinazopakia abiria na kushusha, wakati pembezoni kuna mitaro.

Kutokana na kuwapo kona nyingi barabarani, ni hali inayosababisha hatari kwa wavukaji wanaojikuta wakikimbia ovyo, kuepuka, wasigongwe na magari.

Tukiwarejea wanafunzi wa shule za msingi wanaosoma Kiloleni na watu watokao katika nyumba za ibada, nao wakiwa katika makundi au mmoja mmoja wanakuwa katika mtihani mkubwa, wakati wa kuvuka.

Ni mtihani kwa wavukaji, watoto kwa watu wazima wanaolazimika kukimbia sana kuelekea upande wa pili.

Pia, kuna kundi la watu maalumu wanaopata shida kuvuka barabara hiyo.

Niseme maeneo ya Barabara ya Kiloleni, kuanzia eneo la Kona ya Bwiru hadi kufika Njia Panda Msikiti wa Kiloleni, kunatakiwa kutafutiwe ufumbuzi wa usalama barabarani, kuwawezesha watu wavuke mahali hapo salama na daima wasikimbie ovyo.

> **Niseme maeneo ya Barabara ya Kiloleni, kuanzia eneo la Kona ya Bwiru hadi kufika Njia Panda Msikiti wa Kiloleni, kunatakiwa kutafutiwe ufumbuzi wa usalama barabarani, kuwawezesha watu wavuke mahali hapo salama na daima wasikimbie ovyo.**

Hata kwa wasio na matatizo na viungo mwilini, bado imekuwa tabia ya kawaida, bado uvukaji kwao huendana na kusikiliza milio ya magari na wakijiridhisha hawapo, wanatoka mbio kuelekea upande mwingine.

Watu wazima wasio na matatizo, wanalalamika kila siku kazi yao imekuwa mchezo wa kukimbia kuelekea upande mwingine, wakihofia kugongwa.

Ndipo napatwa na maswali mengine yanayonijia pasipo majibu, kwa wale wenye kasoro za miili yao, jamii ya walemavu na wazee ni makundi yasiyoweza kukimbia katika kuelekea upande wa pili, wapataje msaada?

Tikija kwa madereva wa bodaboda, nao ni kama vile utamaduni kwamba katika barabara hizo wanakimbiza pikipiki na wakizifanyia mbwembwe kama vile zinataka kuanguka. Hapo nashuhudia madereva hao hawana kofia na kawaida kuwaona wako 'mishikaki.'

Ni kweli tunapenda maendeleo, lakini hili la barabara pamoja na uzuri wake wa lami, inatakiwa mamlaka husika kuweka vizuizi ambavyo vitasaidia watumiaji barabara hiyo kuvuka kwa utaratibu unaofaa, ili kuwapunguzia adha ya hatari kukimbia ovyo.

Katika barabara ya Kiloleli, kuanzia kona ya Bwiru kuelekea njiapanda eneo la Kilielli, kuna kona mpaka liliko eneo la Kiloleli Msikitini, ambako hakuna matuta.

Maeneo ya Montessori, Kiloleni Shule ya Msingi, Matofali na Maduka Tisa, nashauri kwa sasa kinachotakiwa kufanyika, ni kuwapa utaratibu mbadala utakaowawezesha watu kuvuka kwa usalama zaidi.

BARUA & MJADALA

## PSSSF badilikeni

**Ndugu Mhariri**

*NINAKUSHUKURU kunipatia nafasi katika gazeti lako tukufu nitoe dukuduku langu kwa usumbufu na mateso tunayoyapata sisi wastaafu kwa kucheleweshewa kupatiwa mafao yetu ya kuinua mgongo na pensheni kwa muda mrefu sana.*

*Inasikitisha kuona mtu aliyelitumikia taifa kwa miaka kadhaa anacheleweshewa mafao yake kwa kipindi cha kuanzia miezi tisa hadi mwaka mmoja ndipo apate mafao yake. Na mbaya zaidi ikizingatiwa kipindi chote hicho, mstaafu huyu hapokei chochote cha kujikimu maisha yake.*

*Kwa kweli hii ni kero ya muda mrefu sasa na hivyo umefika wakati kwa Mheshimiwa Rais wetu John Magufuli atuondolee shida hii kama alivyofanya katika ziara yake ya Songwe, Katavi, Rukwa na Ruangwa.*

*Ni aibu sana kwa taifa letu tukiwa tunaelekea miaka 58 ya kujitawala kuwa na watendaji wabovu kama hawa wa PSSSF. Inaelekea uongozi wa taasisi hii umelala sana kiasi cha kuwafanya watendaji wake kufanya kazi kwa mazoea.*

*Wakati wawekezaji wanakingiwa kifua wasicheleweshewe vibali vya uwekezaji, na sisi wastaafu tunakuomba Rais wetu utuondolee kero hii. Wewe ni mkombozi wa wanyonge.*

**Ni mimi mstaafu niliyechoka.**

## Wenzetu hawa wanaikwaza jamii

**Mhariri,**

*UKISOMA vitabu vya dini na hata kusikiliza mahubiri na mawaidha ya viongozi wetu wa dini ni dhahiri utapata jinsi ambavyo misahafu na maelekezo ya viongozi hao inavyosisitiza juu ya umuhimu wa kulinda uhai wa binadamu.*

*Inafafanuliwa kwamba uhai wa binadamu ni lazima ulindwe kwa kuwa ndivyo yalivyo maagizo ya Muumba na kwamba hata sheria, kanuni na taratibu mbalimbali katika jamii na makabila zinasisitiza juu ya hilo. Ninaandika katika ukurasa huu kuelezea namna ninavyochukizwa na watu ambao hutupa watoto ovyo jalalani ama kwenye vyoo wakati mwingine na hivyo kukatisha maisha ya watoto wasio na hatia. Tatizo hili kimsingi liko sana kwa wasichana ambao matukio mengi yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara juu yao katika vyombo vya habari.*

*Ninawatahadharisha watu wanaofanya unyama huo wakumbuke kwamba Mwenyezi Mungu anawaona.*


*Ninaomba kwa serikali yetu tukufu iwachukulie hatua kali watu wa aina hii wasiothamini kabisa uhai wa binadamu.*

**Pawa Nkanda- Majimoto**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Mambo safi Musoma Vijijini kujenga zahanati kila kijiji




**Na Sabato Kasika**

HUDUMA ya afya kwa binadamu ni muhimu. Kwa kutambua hilo, serikali iliahidi kujenga zahanati kila kijiji nchini, kituo cha afya kila kata, hospitali kila wilaya na hospitali ya rufani kila mkoa.

Huo unaitwa Mpango wa Maendeleo ya Msingi (MMAM).

Kazi ya ujenzi wa sehemu hizo za kutolea huduma ya afya umekuwa na serikali, ikiwashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wananchi, wakichangia nguvukazi yao kufanikisha ujenzi.

Karibu maeneo yote nchini, zahanati zimekuwa zikijengwa kusogeza huduma ya afya kwenye makazi ya wananchi, ili kuwaondolea usumbufu wa kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo muhimu.

Wakazi wa Jimbo la Musoma Vijijini, mkoani Mara ni miongoni mwa waliounga mkono mkakati wa serikali kujenga zahanati kila kijiji, ni kwa kushiriki kwa hali na mali ujenzi huo.

Ni jimbo lenye jumla ya vijiji 68, zahanati 24 zinazotoa huduma, huku nyingine 13 zikiendelea kujengwa. Zikikamilika, kutakuwapo na jumla ya zahanati 37. Ni kwamba wamevuka nusu ya hitaji, vijiji 29 ndivyo havijajenga zahanati, lakini viko kwenye mchakato wa kuhakikisha kila kijiji kuwa na zahanati yake.

Hatua ya wananchi hao kuunga mkono juhudi za serikali za kujenga zahanati kila kijiji hadi kufikisha zaidi 37, ni wazi kwamba wamedhamiria kuboresha huduma hiyo kwenye maeneo yao.

Wananchi hao, pia wanajenga vituo vya afya vya kata, wakiwa wamekamilisha viwili ambavyo ni vya kata za Mugango na Murangi, ambavyo sasa vinaendelea kutoa huduma ya afya.

Katika kujitolea huko kuhusu ujenzi, hivi sasa wameelekeza nguvu kwenye ujenzi wa hospitali ya wilaya yao, kwa kila kijiji kinachangia shilingi milioni mbili, ili kukamilisha ujenzi.

Kinachofanywa na wananchi hao, kinaonyesha ni jinsi gani wanatambua kazi na mchango mkubwa unaofanywa na serikali katika kuboresha huduma ya afya na hasa ujenzi wa zahanati kila kijiji.

Inaumiza kuona mgonjwa anatembea au kusafiri umbali mrefu kwenda kufuata huduma za afya, ambazo kijiji chake kinengekuwa na zahanati, angeipata bila kuhangaika mbali.

Hivyo uamuzi wa serikali wa kujenga zahanati kila kijiji ni muhimu na kwa wanaotambua umuhimu huo, wameuunga mkono kwa mafanikio.

Wanatambua lengo la serikali ni kuboresha huduma ya afya nchini, ndiyo maana imechukua hatua inayoungwa mkono na wananchi kwenye maeneo mbalimbali, ikiwamo Musoma Vijijini.

Serikali inatambua umuhimu wa afya bora kwa wananchi wake, kwani ni rasilimali muhimu kwa maendeleo, kwani maendeleo ya taifa yataletwa na wananchi wenye afya na uwezo wa kuzalisha mali.

Mwaka 2015 wakati wa ufunguzi wa Bunge la Tanzania, Rais John Magufuli, aliahidi serikali itahakikisha MMAM inatekelezwa kwa vitendo.

Serikali ilifikia hatua hiyo, baada ya kuona wananchi wake wakiteseka kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya afya na kuamua na kutekeleza miongozo ya MMAM kuwa na zahanati kila kijiji.

Uamuzi wa serikali sasa umeanza kuzaa matunda kwenye maeneo mbalimbali nchini, ikiwamo Musoma Vijijini, ambako zimejengwa zahanati 24 zinazofanya kazi, huku nyingine 13 zikiendelea kujengwa.

Ni ishara namna wananchi wa eneo hilo walivyopokea kwa mikono miwili mkakati wa kiserikali.

Inawezekana zahanati zikawa na watumishi wachache, tofauti na mwongozo wa utumishi wa mwaka 2014 unaoagiza kila zahanati kuwa na wahudumu 20, lakini kuwapo kwa zahanati kila kijiji ni hatua nzuri.

Kaulimbiu ya 'maendeleo kwa vitendo' inayotumiwa na wananchi wa eneo hilo katika shughuli za maendeleo, inaweza kuwawsogeza katika hatua kubwa ya maendeleo.

Haijalishi zahanati walizojenga zina watumishi wa kiasi gani, lakini jambo la msingi ni hatu ya kupatikana majengo na vifaa, huku mchakato wa kuongeza wengine ukiendelea.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed





Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijiji Dar es Salaam jana, akilalamikia ukiukwaji wa sheria katika mchakato unaoendelea wa kuwapata wagombea wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kulia ni Mwenyekiti wa Wazee CUF, Taifa, Mohamed Chunga na Mkurugenzi wa Itifaki, Udhibiti na Mafunzo, Masoud Muhina. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mbunge ataka mawaziri wabanwe uhujumu uchumi

**INATOKA UK. 2**

Mbunge wa Misungwi (CCM), Charles Kitwanga, alisema bado nchini kuna

urasimu katika sekta ya uwekezaji kwa kuwa wawekezaji wengi wanashindwa kuwekeza.

"Tupunguze urasimu, kiwanda cha kuunda magari aina ya Voxwagen kimejengwa Rwanda wakati ilipaswa kujengwa Tanzania, niliwaleta mimi wale wawekezaji, ilichukua muda wa miezi sita kujadili hadi wakaondoka. Iliniuma sana, tubadilike jamani," alisema.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Sophia Mwakagenda, alisema asilimia

70 ya Watanzania ni wakulima lakini jambo la kushangaza kwenye bajeti ya mwaka jana, Bunge lilipanga Sh. bilioni 100 ziende katika kilimo lakini zilizotolewa na Sh. bilioni mbili tu.

"Tunapokwenda kwenye uchumi wa viwanda bila kuwekeza kwenye kilimo hatujatenda kitu. Maofisa ugani wapo wachache, kumekuwa na kilio cha pembejeo, mbegu hazioti, mbolea zinakwenda kwa kuchelewa," alisema Mwakagenda.

Alisema kwenye uvuvi bunge lilipitisha matumizi ya Sh. bilioni nne lakini zilizotolewa ni asilimia tatu tu. Mbunge wa Lupa (CCM), Victor Mwambalaswa, alisema serikali inapaswa kutoa kipaumbele kwenye sekta ya kilimo.

"Tuna vyuo vya kilimo vingi, tuna wataalamu kutoka Chuo cha Kilimo cha Sokoine (SUA) ambao wanaheshimika duniani. Naomba tuwatumie wataalamu hawa ili tupate 'blue print' ya kutuwezesha namna ya kutumia ardhi na maji," alisema Mwambalaswa. Naye Mbunge wa Nkenge (CCM), Dk. Diodorus Kamara, alisema wakulima wanapaswa kuwezeshwa kwa kupata viuatilifu na kwamba bandarini kuna viuatilifu vingi vimekwama kwa muda mrefu.

# Sarakasi uchaguzi mitaa zazidi kunoga

**INATOKA UK. 2**

mkuu ujao.

"Tayari uchaguzi wa marudio imethibitisha kuwa serikali ina mkakati wa wagombea wa CCM wapite bila kupingwa. Kwa nini tusiamini kuwa mkakati huu utaendelea kwenye uchaguzi mkuu 2020?" Prof. Lipumba alihoji.

Alisema kutokana na utaratibu huo, wasimamizi wasaidizi wamewaengua wagombea wote wa CUF maeneo ya Misungwi, Nyamagana, Ilemela, Kwimba, Maswa, Ubungo, Kinondoni, Kigamboni, Temeke, Ilala, Bagamoyo, Handeni, Masasi, Ruangwa, Lindi Mjini, Lindi Vijijini, Uyui, Nzega, Urambo, Tanga, Pangani, Mkinga, Chalinze na Same.

"Wamewaengua wagombea wa CUF kwa utashi wao bila kufuata sheria, kanuni wala mwongozo wa uchaguzi huku wakiwateua wagombea wa CCM wapite bila kupingwa. Katika hali kama hii siyo tu unaondosha demokrasia, bali pia unajenga chuki ndani ya jamii.

"Utaratibu huu wa kuwapitisha wagombea wa CCM bila kupingwa unaweza kuondosha ushirikiano wa kijamii na kuchochea uhasama siyo tu wa kisiasa, lakini pia mdororo wa shughuli za kiuchumi katika jamii," Prof. Lipumba alisema.

Alisema kwa mwenendo huo, ni vyema wabunge wa CCM wakaanzisha hoja ya kurudi kwenye mfumo wa chama kimoja ili kuepuka matumizi mabaya ya fedha za umma na uhasama wa kisiasa miongoni mwa Watanzania.

"Ni matumizi mabaya ya fedha za umma, huwezi kufanya maandalizi yote ya uchaguzi, ikiwamo uchapishaji wa nyaraka mbalimbali zinazohusiana na uchaguzi; kanuni na miongozo, ukafanya semina elekezi mbalimbali ili kufanikisha uchaguzi huku mkiwa na mkakati na mkijua kuwa hapatakuwa na uchaguzi na badala yake mtafanya uteuzi wa wagombea wa CCM wapite bila kupigwa.

"Lililotokea ni matumizi mabaya ya fedha na mamlaka ya umma kwa manufaa ya chama kimoja cha siasa na viongozi wake. Ni ufisadi mkubwa. Wanaoendeleza na kusimamia ufisadi huu hawawezi kuwa majemedari wa kweli wa kupambana na ufisadi katika maeneo mengine," alidai.

Distributed via Inmedia

**WANANE MBARONI**

Mkoani Ruvuma Jeshi la Polisi linawashikilia wafuasi wanane wa (Chadema), wakiwamo mwenyekiti wa chama hicho mkoa, Aden Mayala (37) na madiwani kwa kuhuma za kufanya fujo kwenye ofisi ya msimamizi wa uchaguzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alidai tukio hilo lilitokea Novemba 5, mwaka huu majira ya saa nane mchana.

Jijini Dodoma, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Joseph Nyamhanga, jana aliwataka viongozi na wasimamizi wa uchaguzi huo kuhakikisha wanasimamia kwa karibu kanuni, sheria na miongozo iliyowekwa ili uchaguzi huo ufanyike katika mazingira huru na ya haki.

Alisema mchakato uliopo kwa sasa ni uteuzi wa wagombea katika nafasi za wenyeviti wa vijiji, vitongoji na mitaa na nafasi ya wajumbe wa halmashauri za vijiji na wajumbe wa kamati za mitaa.

"Nitoe maelekezo kwa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi, kusimamia kwa weledi zoezi la uwasilishaji wa pingamizi na kutoa uamuzi wa haki kuhusu pingamizi hizo za uteuzi wa wagombea," alisema.

**JELA NUSU MWAKA**

Mkoani Kigoma, Mahakama ya Mwanzo/Ujiji Mkoa wa Kigoma imemhukumu Hussein Hamisi (40), kutumikia kifungo cha miezi sita jela kwa kosa la kumfanyia fujo msimamizi wa uandikishaji wapigakura, Emma Mfinanga, kwenye kituo cha uandikishikishaji cha Shule ya Msingi Businde.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi wa mahakama hiyo, Mbuke James, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Hakimu James alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine.

Alisema upande wa mashtaka ulipeleka mashahidi wanne ambao walithibitisha kuwa mshtakiwa alifanya fujo kwenye kituo cha kujiandikisha wapiga kura.

Uchaguzi wa serikali za mitaa umepangwa kufanyika siku 17 zijazo, ukitarajiwa kushirikisha wapigakura zaidi ya milioni 19.

**Imeandikwa na Joctan Ngelly (KIGOMA), Mary Geofrey (DAR), Paul Mabeja (DODOMA), Gideon Mwakanosya (RUVUMA), Happy Severine (SIMIYU) na Gurian Adolf (Katavi).**

# Benki Azania yazindua huduma za kidigitali

**INATOKA UK. 5**

kuchagua wapi na wakati gani wapate huduma za kibenki. Mawakala wa Azania Plus wanapatikana katika maeneo mbalimbali kote nchini," Itembe alisema.

Aliongeza kuwa huduma hiyo ni mwendelezo wa huduma nyingi zinazotolewa na benki hiyo baada ya wanahisa wake kuongeza mtaji Desemba mwaka jana na utekelezaji wake kufanyika mwaka huu na kufanya rasilimali za benki hiyo kufika Sh. trilioni 1.239. Alisema mtaji wa wanahisa pia umeongezeka na kufika Sh. bilioni 181.

Katika uzinduzi huo, Mwenyekiti wa Bodi ya benki hiyo, Felix Maagi, alisema huduma hiyo ya kibenki kwa njia ya kidigitali, itawezesha wateja wake kupata huduma bora zaidi mahali popote walipo.

Meneja wa Huduma za Kidigitali wa benki hiyo, Vinesh Davda, alisema huduma hiyo inapatikana kwa kupakua programu hiyo inayotumia mfumo wa Android na IOS na kwamba huduma hiyo inapatikana mahali popote panapokuwa na mtandao.

# Abbas afafanua maagizo ya Rais

**INATOKA UK. 3**

za rejea za kisheria na huo ndiyo msingi wa utawala wa sheria.

"Na hapa ndipo Watanzania wengi tunatofautiana, yaani kila mtu anatamani utawala wa sheria, lakini ukimwambia ufuate sheria kila mtu hataki.

"Sasa, niambie kazi ya CAG siyo ukaguzi, sasa achana na watu wanaitwa wachambuzi wa mambo, nenda kwenye sheria, soma usipoelewa maana yake kuna kusoma sheria na kuwa mwanasheria, usipoelewa angalau, wahoji wataalamu wa sheria," alisema.

Dk. Abbas pia alisema kila mhimili nchini unatimiza wajibu wake na kutolea mfano Bunge kuwa huitazama serikali kwa muktadha wa kupitisha bajeti na kufuatilia utekelezaji wake, Mahakama hutafsiri sheria.

"Kuna mtu anasema mihimili isiingiliane, siyo kweli. Someni vizuri Katiba, kuna mambo lazima mihimili iingiliane, upo mwingiliano wa mihimili hii wa kikatiba na kisheria," alisema.

Dk. Abbas akitaja mafanikio ya serikali katika miaka hiyo minne, alisema imeagiza mabehewa ya treni 1,430.

"Katika miaka minne ipo miradi ya maji 1,600 nchi nzima imetekelezwa ambapo ahadi iliyotoa ifikapo 2020 ilikuwa ni kupeleka maji vijijini angalau asilimia 85 na sasa tumefika asilimia 65 kutoka asilimia 50.

"Miradi ya maji zaidi ya 300 inaendelea kwa sasa. Kwa upande wa mjini tuliahidi angalau asilimia 95 na sasa imefikia asilimia 85 na ipo miradi mingi ya zaidi ya Sh. bilioni 700 inafanyika," alisema.

Kuhusu kuhamia Dodoma, Dk. Abbas alisema zaidi ya asilimia 90 ya watumishi waliotakiwa kwenda katika jiji hilo jipya wamesharipoti.

kuhusu Sh. milioni 50 kila kijiji/mtaa, alisema serikali haikusema itapeleka fungu hilo moja kwa moja kwa wananchi kwa kwenda kuwamwagia kwenye vijiji au mitaa yao.

Alisema lengo la serikali ni kupeleka fedha kwa Watanzania kwenye ngazi ya vijiji ili kuhakikisha inawaletea maendeleo.

Dk. Abbas pia alisema mtu hawezi kuipima Tanzania kwenye haki za binadamu kwa sababu kwa sasa watu hawaandamani.

"Kila haki ina wajibu wake, ili uandamane kuna utaratibu wa kukufanya uandamane, waliozifuata wameandamana, waliokiuka hawataandamana milele," alisema.

Alisema katika eneo la rushwa, kazi inaonekana na imefanya Tanzania kujulikana wazi kuwa mtu akiwa kiongozi wa ngazi yoyote, akijihusisha na rushwa hatua zitachukuliwa.

"Nilikuwa mwandishi, tuliwahi kuandika mapapa fulani hawaguswi, katika miaka hii minne mmeona tumekwenda hatua kwa hatua, mpaka sasa wanasiasa wanaomba poo," alisema.

**HABARI KITAIFA**

# Viongozi jumuiya watumia maji kukamatwa

**Na Tiganya Vincent**

MKUU wa Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, John Mwaipopo, ameagizwa kuwakata viongozi wa jumuiya za watumiaji maji wa Nkinga na Matinje kwa tuhuma za kula fedha za mradi zilizotokana na malipo ya watumiaji maji.

Agizo hilo limetolewa na Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, wakati wa ziara yake katika Wilaya ya Igunga ya kukagua miradi ya maji na kukutana na malalamiko ya tatizo la maji katika maeneo hayo ambalo limetokana na matumizi mabaya ya fedha za mradi.

Alisema viongozi wote wa jumuiya ya watumiaji maji wanaotuhumiwa kula fedha ni lazima wakamatwe na wazirudishe ili ziweze kusaidia uimara wa mradi na upatikanaji wa maji kwa wakazi wa maeneo hayo.

Prof. Mbarawa alisema ni kosa kwa viongozi hao kukusanya fedha zinazotokana na mauzo ya maji bila kuziweka benki kwa kuwa vitendo vya aina hiyo ndivyo vimesababisha baadhi ya miradi ya maji kufa kwa sababu ya kukosa fedha pindi unapotakiwa kufanyiwa ukarabati.

Katika hatua nyingine, waziri huyo alisema serikali itahakikisha inapeleka maji ya kutoka Ziwa Victoria katika eneo la Nkinga ili kusaidia kupunguza tatizo la maji katika eneo hilo ambalo lina Hospitali ya Rufani ya Nkinga ambayo inategemewa na wananchi wa kanda hiyo.

Alisema licha ya eneo hilo kuwa na umbali wa kilometa 25 kutoka bomba kubwa la kupeleka maji Igunga, serikali itahakikisha inapeleka maji katika eneo hilo ndani ya miezi isiyozidi minne kwa kuwa fedha za kutekeleza mradi huo zipo.

Prof. Mbarawa amewataka wataalamu wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Tabora (TUWASA) kuhakikisha wanaharikisha kufanya usanifu ili kujua gharama halisi za kupeleka maji katika eneo hilo ili mradi huo uanze haraka.

Wakati huo huo Waziri Mbarawa amesema serikali imeamua kupeleka maji katika Mji wa Bukene wilayani Nzega kutoka Ziwa Victoria kwa gharama isiyopungua shilingi bilioni 8.

Alisema maji hayo yatachukuliwa katika bomba la maji la mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria ambalo liko katika umbali usiopungua kilometa 32.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha wakazi wa Bukene na maeneo mengine mkoani Tabora ambayo yanashida ya maji wanapata haki ya kupata maji safi na salama.

Awali Mbunge wa Jimbo la Manonga, Seif Gulamali, alisema miradi ya maji katika maeneo ya Nkinga na Matinje imekuwa ikisuasua kutokana na viongozi wa jumuiya kukusanya pesa zinazotokana na mauzo ya kila siku ya maji bila kuzipeleka benki.



Kijana aliyekuwa amefungwa minyororo kwa miezi miwili, Shadrack Johanes (26) mkazi wa Old Shinyanga, Manispaa ya Shinyanga, akiwa na mama yake mzazi, Nonja Shadrack Kalala, ambaye alifika juzi, kwa ajili ya kumchukua na kwenda naye mkoani Mwanza, anakoishi na kumpatia matibabu ya tatizo lake la ugonjwa wa akili. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Umeme wa jua kunufaisha visiwa vidogo

**Na Futuna Seleman,** MAFIA

WANANCHI wa Kisiwa cha Chole, Jibondo Bwejuu na Juani, watanufaika na huduma ya usambazaji wa umeme wa jua ambapo tayari serikali imetenga kiasi cha Sh. bilioni 2.8 kwa ajili ya usambazaji wa huduma hiyo.

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alisema huduma ya usambazaji wa umeme wa jua kwa visiwa vilivyopo wilayani Mafia, mkoani Pwani utahusisha pamoja na vijiji vitatu ambavyo havijafikishiwa nishati hiyo.

Aliyasema hayo katika mkutano wa hadhara katika kijiji cha Chemchem kabla ya kukiwashia umeme na kusema kuwa maandalizi ya kutangaza zabuni husika mwezi ujao yamekamilika.

"Baadhi ya visiwa hivyo kuwa ni pamoja na Chole, Ibondo, Juani na Bwejuu, serikali imedhamiria kupeleka umeme nchi nzima hata katika maeneo ambayo hayapitiki kwa urahisi itafanya kazi hiyo ili wananchi wanufaike na huduma hiyo watanzania wote lazma wanufaike na huduma ya umeme," alisema na kuongeza:

"Wakati Rais anaingia madarakani aliahidi kusambaza umeme katika maeneo yote ambayo hayana umeme. Sisi wizara tutahakikisha hilo linatekelezwa."

Aidha, aliwataka wananchi wa kijiji hicho kulinda miundombinu ya umeme ili kupatikana muda wote kwani sekta zote muhimu za utalii na uvuvi zinategemea umeme wa uhakika.

Kadhalika, aliwahimiza wananchi ambao miundombinu ya umeme imepita katika maeneo yao kulipia huduma hiyo ya umeme ili kujikwamua kiuchumi.

Naibu Waziri aliwatoa hofu wananchi ambao wameshalipa pesa kwa ajili ya kuunganishiwa umeme, lakini mpaka sasa hawajaunganishwa na huduma hiyo, kuwa serikali haitapokea mradi ambao una mapungufu na kwamba kabla ya mkandarasi hajakabidhi, mradi utakaguliwa. "Nawataka makandarasi wafanye kazi kwa mujibu wa mikataba."

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Rukia Muhammed Mbottoni, aliishukuru serikali kwa kuwapa unafuu wananchi wa vijijini kwa kuwaletea umeme wa REA ambao kila mwananchi anamudu gharama zake.

Alisema umeme wa REA umewawezesha kujiajiri kwa kufanya biashara ndogo zinazowasaidia kujikwamua kiuchumi.

Mbali na Kijiji cha Chemchem, Naibu Waziri pia alikagua utekelezaji wa miradi ya nishati na kuwasha umeme katika Kijiji cha Marimbani.

Aidha, alitembelea eneo ambalo litajengwa mitambo ya kuzalisha umeme wa upepo na kukagua mitambo ya kufua umeme iliyopo wilayani humo.

# Elimu ya usimamizi misitu vijijini

**Na Christina Haule,** KILOSA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, imeahidi kusambaza elimu ya kuendeleza usimamizi shirikishi wa misitu (USM) katika vijiji 119 vilivyopo ili kurejesha hali ya uhifadhi wa misitu kama ilivyokuwa zamani.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Adam Mgowi, alisema jana kuwa mradi huo kwa wilaya hiyo umefanikiwa kwenye vijiji 20 ambavyo vinatekeleza mradi wa kuleta mageuzi katika sekta ya mkaa Tanzania (TTCS) ambao unahimiza USM ulioanza kutekelezwa tangu mwaka 2012 chini ya Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) na Shirika la Kuendeleza Nishati ya Asili Tanzania (TaTEDO) kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Uswis (SDC).

Mgowi alisema Kilosa ilikuwa na changamoto kubwa ya uharibifu wa mazingira kutokana na uwepo wa rasilimali nyingi za misitu isiyosimamiwa vizuri, lakini baada ya mradi kumekuwa na mpango mzuri wa matumizi bora ya ardhi na uvunaji misitu.

Alisema, pamoja na uhifadhi kuongezeka vijijini, halmashauri na wanavijiji wamekuwa wakinufaika na rasilimali za misitu jambo ambalo ndilo linawasukuma kusambaza mradi huo ili kunufaisha jamii ya Kilosa.

Alisema pia wamenufaika na mpango wa matumizi bora ya ardhi hivyo kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji na wananchi wengine wilayani humo. Mgowi alitoa wito kwa wakazi hao wilayani humo ambao wamefanikiwa kupata hati za hakimiliki za kimila kuzitumia kwa ajili ya kuongeza kwa kuchukua mikopo kwenye taasisi za fedha sambamba na kuzitumia kumaliza migogoro ambayo imeishi ikiwazunguka kwa muda mrefu.

Naye Ofisa Mradi anayeshughulikia maendeleo ya jamii na utawala kutoka TFCG, Michael Nilongo, alisema, katika vijiji 20 vya mradi wilayani Kilosa vimefanikiwa kupata hati za hakimiliki za kimila kwa wanavijiji zaidi ya 800 waliopo katika vijiji vitano wilayani humo. Alivitaja vijiji vilivyonufaika kuwa ni pamoja na Kigunga wamepata hakimiliki 62, Nyali 200, Madizini 200, Dodoma Isanga 200 na Ulaya Mbuyuni 125.

Alisema, utoaji wa hatimiliki hizo za kimila kwa wananchi umezingatia vipaumbele mbalimbali ikiwamo familia zenye mzazi mmoja, familia zenye kipato duni, familia zenye ulemavu.

# Bil. 417/- zalipa wakulima pamba

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema serikali imeshalipa Sh. bilioni 417 kwa wakulima wa zao la pamba nchi nzima na kwamba haitoingilia kupanga bei ya zao hilo ili kuhakikisha mkulima hapati hasara.

Bashe aliyasema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Busega, Raphael Chegeni (CCM), ambaye alitaka kujua mkakati wa serikali wa kuwalipa wakulima wa pamba madeni yao ambayo wanaidai serikali.

Bashe alisema serikali imehimiza kampuni zilizonunua pamba kuwalipa wakulima fedha zao na tayari Sh. bilioni 417 zimeshalipwa na kiasi kinachodaiwa kwa sasa ni Sh. bilioni 50.

Hata hivyo, Bashe alikiri kuwapo kwa baadhi ya wakulima wa pamba ambao bado hawajalipwa fedha zao, na kwamba sababu ya msingi ni kwamba asilimia zaidi ya 80 ya pamba inakwenda nje ya nchi.

Alisema wanunuzi wanakabiliwa na mtikisiko wa bei ambao katika soko la dunia na wao kama nchi walitoa maelekezo ya bei ya kununulia kama serikali, ambayo ni maamuzi ya serikali kwa ajili ya kumlinda mkulima asipate hasara.

"Tayari serikali imezugumza na kampuni zote zinazonunua Pamba ili kuwasaidia namna ya kupunguza riba kwa wanunuzi ili waweze kwenda sokoni kununua pamba kwa bei ya Sh. 1200," alisema Bashe.

Alisema Novemba 14, mwaka huu wanatarajia kukutana na kamati ya wanunuzi na kampuni zote zinazonunua pamba ili kuona mtiririko wa fedha unavyokwenda.

Aliongeza pamba yote iliyokuwa kwa wakulima imeshakusanywa na hivi sasa kilichobaki mikononi mwao ni tani 5,000 tu ambayo wanaamini mpaka kufika mwisho wa mwezi huu, itakuwa tayari imeshaondoka mikononi mwao.

Alibainisha wanaamini kuwa msimu utakapoanza Novemba 25 pamba yote itakuwa imeondoka na kuhusu suala la bei serikali wanajitahidi kupunguza gharama kuanzia msimu huo unaokuja.

Alisisitiza serikali haitaingilia suala la upanga bei, na kwamba bei itaendana na hali halisi ya soko kwa wakati huo, huku jukumu la serikali ni kuhakikisha mkulima hapati hasara ikiwa ni pamoja na kutafuta njia nyingine ya kumlinda kuliko kumwathiri mnunuzi.



Wakuu wa Idara na Taasisi za Wizara ya Fedha na Mipango, wakifuatilia uwasilishwaji wa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/21, Bungeni, jijini Dodoma juzi. **PICHA: WFM**

# Waziri apiga marufuku wateja kununua nguzo za umeme

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amesema ni marufuku mtu yoyote ambaye atahitaji kuunganishiwa nishati ya umeme kununua nguzo, kwani serikali inagharamia kwa asilimia 100.

Dk. Kalemani alitoa kauli hiyo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Halima Bulembo (CCM). Katika swali lake, Halima alieleza kuwapo kwa malalamiko mengi ya wananchi katika Mkoa wa Kagera wakiilalamikia Shirika la Umeme nchini (Tanesco) kuwatoza fedha kwa ajili ya kununua nguzo na hivyo kutaka kauli ya serikali kuhusiana na suala hilo.

Distributed via ipnmedia

Akijibu swali hilo, Dk. Kalemani alisema ni marufuku kwa mtu yoyote yule awe mhandisi au ametoka Tanesco au kibarua kumtoza mtu yoyote fedha kwa ajili ya kununua nguzo.

"Ni marufuku kwa mtu yoyote kununua nguzo awe engineer (mhandishi), awe kibarua au awe ametoka Tanesco ni marufuku kuuza nguzo, kwa sababu serikali imegharamia kwa asilimia 100," alisema Dk. Kalemani. Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum, Benardetha Mushasha (CCM), alisema Mkoa wa Kagera una vijiji 134 ambavyo havijafikiwa na umeme wa REA, Biharamulo vijiji 29, Bukoba tisa, Karagwe nane, Kyerwa 31, Misenyi 5, Muleba 25 na Ngara 27.

Hivyo, Mushasha alitaka kujua ni lini serikali itapeleka umeme wa REA katika vijiji hivyo.

Akijibu, Dk. Kalemani alisema serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inatekeleza mradi wa kupeleka umeme katika vijiji vyote nchini kufikia Desemba, 2021.

"Kwa sasa mkandarasi Nakuroi Investment ltd anaendelea na kazi ambapo kufikia Oktoba 31 mwaka huu vijiji 82 vimefikishiwa umeme katika Mkoa wa Kagera na kazi ya uunganishaji wa wateja inaendelea," alisema Dk. Kalemani.

Aidha, Dk. Kalemani alisema vijiji vyote vitakavyosalia katika Mkoa wa Kagera vitapatiwa umeme kupitia mradi wa REA III mzunguko wa pili unaotarajiwa kuanza Januari, 2020 na kukamilika Desemba, 2021.

# Angalizo wanaokata fedha walengwa Tasaf

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), Mary Mwanjelwa, amewazuia viongozi wanaotoa amri ya kukata fedha za walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) moja kwa moja bila ridhaa yao. Naibu Waziri huyo ametoa angalizo hilo akisema huo si utaratibu sahihi.

Mwanjelwa alitoa agizo hilo jana, bungeni, wakati akijibu swali la Mbunge wa Bahi, Omary Badwel. "Napenda kusisitiza kwamba walengwa wasikatwe fedha zao moja kwa moja bali walipwe stahiki zao na iwapo kuna michango inayotakiwa kama ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya kijiji basi michango hii itozwe kwa wananchi wote wa kijiji husika na sio kukata moja kwa moja kutoka fedha za walengwa wa Tasaf peke yao," alisema Mwanjelwa.

Katika swali lake, Badwel alisema kuwa kwa muda mrefu sasa baadhi ya wananchi wamekuwa wakinufaika na mradi wa Tasaf ambao kwa kiasi umekuwa ukifanya vizuri, aidha, mradi huu umefika vijiji vichache tu na vijiji vingine bado havijafikiwa na serikali iliahidi kuwa vijiji vyote vitanufaika na mradi huo.

Badwel alihoji ni lini serikali itatimiza ahadi yake ya mradi wa Tasaf kufikia vijiji vyote nchi nzima.

Alisema kumekuwa na utaratibu wa baadhi ya viongozi kukata fedha za walengwa wa Tasaf moja kwa moja kwa kuwakatia bima, michango mbalimbali ya vijiji bila ridhaa yao na kuhoji serikali inatoa kauli gani katika jambo hilo?"

Mwanjelwa alisema fedha hizo ambazo ni ruzuku zinatolewa ili kaya iweze kugharamia mahitaji ya msingi kama chakula, gharama za elimu na afya na kuwekeza kwa ajili ya kuanzisha miradi ya kuongeza kipato.

Alifafanua ni maamuzi ya kaya husika kupanga matumizi ya fedha hizo ili mradi hazienda kwenye matumizi ambayo hayasaidii kaya kujikwamua na umaskini.


Alisema katika baadhi ya maeneo, viongozi wa vijiji wanalazimisha kukatwa kwa ruzuku za walengwa ili kukatiwa bima ya afya au kulipia michango mbalimbali, jambo ambalo siyo sawa na halikubaliki.

"Nimalizie kwa kusisitiza kuwa viongozi wote waliokuwa wanatoa amri ya kukata fedha za walengwa wa Tasaf moja kwa moja bila ridhaa yao waache kufanya hivyo kwa kuwa huu sio utaratibu sahihi," alisema. Mwanjelwa.

Alisema mpango wa kunusuru kaya maskini ulipoanza mwaka 2013 uwezo wa fedha uliokuwapo ulitosheleza kufikia vijiji/mtaa 9,986 ikiwa ni asilimia 70 ya vijiji/mitaa vyote nchini.

Mwanjelwa alisema vijiji/mitaa/shehia ambavyo havijafikiwa ni 6,858 na kwamba serikali imeshakamilisha hatua zote za maandalizi ya kipindi cha pili cha mpango huo wa kunusuru kaya maskini ambacho kinatarajiwa kuanza utekelezaji mwishoni mwa mwaka huu baada ya serikali kupata fedha.

Alisema kipindi cha pili ya mpango wa kunusuru kaya maskini kitatekelezwa kwenye halmashauri zote 185 za Tanzania Bara na wilaya zote za Zanzibar katika vijiji/mitaa na shehia zote ikiwa ni pamoja na kufika kwenyevijiji/mitaa/shehia 6,858 ambavyo bado havijafikiwa.




**Habari zote na Gwamaka Alipipi**, DODOMA

## HABARI ARUSHA



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro (wa pili kushoto), akikata utepe kuzindua zahanati katika kijiji cha Losinoni Juu, Kata ya Oldonyowas, katika Halmashauri ya Arusha, juzi. Zahanati hiyo, itasaidia kutatua changamoto ya vifo vya kinamama na watoto, wakati wa kujifungua, vilivyokuwa vikisababishwa na ukosefu wa huduma hiyo kijijini hapo kwa miaka mingi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

Distributed via ippmedia

# Vijana 554 wakopeshwa mamilioni

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Monduli kwa kushirikiana na Shirika la Kuwajengea Uwezo wa Kimaendeleo Vijana (YEDI) imewasaidia vijana wa Monduli kutambua fursa za kiuchumi na kati yao, 554 wamekopeshwa Sh. milioni 206.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Monduli, Rose Mhina, alisema kupitia progamu za kuwezesha vijana kwa kushirikiana na mashirika kadhaa, likiwamo YEDI, halmashauri hiyo imevitambua vikundi 42 na kuvipatia mikopo.

"Tumekuwa na ushirikiano na mashirika kadhaa ikiwepo YEDI ambao wanafanya kazi kubwa kuelimisha vijana na kuwaunganisha na halmashauri kupitia mapato ya ndani ya mwaka 2018/19, tumewapa mikopo isiyo na riba vijana 554," alisema.

Mkurugenzi wa YEDI, Neema Mgendi, akizungumza na wananchi wakati wa kufanya tathimni juu ya miradi ya vijana wilayani Monduli, alisema vijana waliofikiwa wamepewa elimu ya ubunifu wa biashara, ushiriki katika baraza la uongozi na kutambua fursa ili kukabiliana na tatizo la ajira.

"Malengo yetu kuwafikia vijana 850 na hadi sasa tumewafikia vijana 332 na tuliwatafutia mshauri elekezi juu ya kutambua fursa za kibiashara na tulichambua fursa 32 na kati ya hizo ikabainika kuna fursa sita ya kiuchumi ambayo vijana wa Monduli zinaweza kuboresha maisha yao," alisema.

Alisema miongoni mwa fursa hizo ni biashara ya kuuza na kunenepesha mifugo, kuuza maziwa, kuku, mboga, kutengeneza viatu, kusindika vyakula na kujiajiri katika ujasiriamali.

Hamida Omar, ni mfugaji wa kuku na ng'ombe, alisema kabla ya kupata elimu alikuwa na ng'ombe mmoja wa kisasa na kuku wawili lakini sasa ana ng'ombe wawili na kuku 43 wa kienyeji na amekuwa akiuza maziwa na mayai.

Samweli Gitu alisema kutokana na elimu ambayo amepata hivi sasa ameanzisha kiwanda kidogo cha chaki na kuzalisha maboksi matano hadi manane kwa siku na tayari ameanza kupata wateja wa uhakika katika shule zilizoko wilayani Monduli.

Kimani Nyangusi ambaye ni mfugaji alisema kutokana na kupewa elimu na YEDI na kupata mkopo halmashauri, amekuwa akinunua

# RC aagiza msako wanaoua na kubaka

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa Arusha, Mrisho Gambo, ameiagiza kamati ya ulinzi na usalama kufika katika kata ya Olasiti na kushughulikia tatizo la mauaji kwa kinamama na watoto linaloendelea.

Gambo alitoa agizo hilo jana katika ziara yake ya kikazi ya siku mbili ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ya Jiji la Arusha.

Katika ziara hiyo, alikagua mradi wa elimu katika Shule ya Sekondari Burka iliyoko Kata ya Olasiti na kupokea madawati na viti 170 kutoka Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini na mifuko 50 ya saruji, kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo iliyotolewa na Kanisa la EAGT mkoani Arusha.

Akizungumza na wananchi, Gambo alisema kuwa tukio la kinamama na watoto kuuawa na kubakwa, linasikitisha kwa kuwa serikali haiwezi kuvumilia kuona matukio hayo yakiendelea.

"Naagiza kamanda wa polisi njooni eneo hili mfanye uchunguzi na kukamata wote wanaohisiwa kufanya matukio hayo kwa sababu wananchi wanawataja. Anzeni na hao," alisema.

"Haiwezekani matukio kama hayo yanatokea zaidi ya mara mbili na bado wanaofanya matukio haya wapo. Lazima vyombo vya dola vifanye kazi na kuwapata watu hao ili kuwashughulikia," alisisitiza.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, alisema amesikitishwa kuwapo kwa suala hilo, huku akiwataka wananchi kuwa na subira na uvumilivu kwa kuwa serikali inashughulikia tatizo hilo kwa haraka.

Awali, Diwani wa Kata hiyo, Alex Martin, alisema wana changamoto kubwa katika kata yao juu ya mauaji na ubakaji, huku kukiwa na watu wanahisiwa kufanya unyama huo kwa muda mrefu bila kukamatwa.

Alisema tatizo hilo limekuwa likiwajengea hofu wakazi wanaoishi katika maeneo hayo kutofanya shughuli za uzalishaji mali kwa uhuru.

"Matatizo hayo yameanza toka mwaka 2015 hadi 2018 waliuliwa watoto wawili na baada ya miezi mitatu aliuawa mwanamke mmoja pia," alisema.

Alisema hivi karibuni mwanamke mwingine aliuawa huku msichana akibakwa na wanaohisiwa kufanya kitendo hicho aliwajua na kuwataja lakini kinachosikitisha walifikishwa katika kituo cha polisi na kuachiwa jambo ambalo limekosesha amani wananchi.

Diwani huyo aliomba serikali kwa kutoa ushirikiano na kuwasaidia wakazi wa eneo hilo kwa kuwatia mbaroni watu wote wanaosababisha matukio hayo, ili kutenda haki kwa makosa waliyoyafanya.

# Halmashuri zaagizwa kuongeza makusanyo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

HALMASHAURI saba za Mkoa wa Arusha zimeagizwa kutafuta vyanzo vipya vya mapato ya ndani ili kumudu kulipa mishahara ya watumishi wao.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na watumishi mbalimbali wa Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Alisema kwa sasa halmashauri hizo zimekuwa zikikusanya mapato amabayo hayakidhi hata kulipa mishahara watumishi wake na kuipa mzigo serikali kuu.

"Rais anajikuta akibeba mzingi huu wa kulipa mishahara watumishi wote wa halmashauri zetu, wakati tungeweza kukusanya mapato ya ndani na kulipa watumishi wake," alisema.

Gambo alisema Halmashauri ya Jiji la Arusha, ilikisia kukusanya mapato ya ndani ya Sh. bilioni 20 huku mishahara ya watumishi ikiwa Sh. bilioni 37.1 na Halmashuri ya Ngorongoro makisio ni Sh. bilioni 2.3 huku mishahara ni Sh. bilioni 12.5.

Halmashuri ya Arusha DC, alisema makisio ni kukusanya Sh. bilioni 5.7 huku mishahara ikiwa Sh. bilioni 33.4 na Meru makisio yao Sh. bilioni 3.4 huku mishahara ya watumishi ikiwa Sh. bilioni 35.3.

Alisema hata barabata za Jiji la Arusha zinajengwa kwa Sh. bilioni 26 huku mapato yakiwa Sh. bilioni 20.

Gambo alisema pasipo kuongeza jitihada za ukusanyaji mapato, hakuna halmashuri itakayoufanya miradi ya maendeleo.

"Hapa tumshukuru Rais anayetuwezesha mishahara na miradi mbalimbali tunayoitekeleza. Ni vyema kila mmoja ajitafakari tuongeze mapato yetu," alisema.

# Ujerumani yafadhili milioni 139/- upandaji miti

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

RAIS wa Jiji la Kiel nchini Ujerumani, Hans Werner Tova, amezindua rasmi kitalu cha miti cha Himo ambacho kimetengewa zaidi ya Euro 58, sawa na Sh. milioni 139.2 za Tanzania kwa ajili ya kutekeleza mkakati wa kuisuka Moshi kuwa ya kijani.

Akizungumza baada ya kuwasili mjini hapa, Tova alishauri mpango huo wa upandaji miti uwe wa kudumu na kuwataka viongozi na wananchi wa wilaya hiyo kuipokea kampeni hiyo kwa mikono miwili, huku akitoa kila aina ya ushirikiano ili kufikia lengo zuri lililokusudiwa.

Mradi huo wa miti ni mradi wa pamoja kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi na Jiji la Kiel, ambao unafadhiliwa na serikali ya Ujerumani.

"Kitumieni kitalu hiki kwa ajili ya mpango mahsusi unaolenga kuboresha mazingira ya Moshi na kuanzia sasa ni vyema mkayahifadhi maeneo yote yasiyo na miti ili kuepuka wavamizi ambao wanataka kuharibu mazingira yenu kwa shughuli zao binafsi hasa za kiuchumi," alisisitiza Tova.

Wakati wa mkutano wake na wananchi wa Himo, Rais huyo wa Jiji la Kiel, alipongeza kazi inayoendelea kufanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, huku akiahidi kudumisha uhusiano wa miji hiyo miwili kwa kuongeza nguvu zaidi katika kitalu hicho, kwa kukifanya kuwa shamba darasa la mfano mkoani Kilimanjaro.

Kabla ya ushauri huo wa Tova, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Michael Kilawila, alimweleza mgeni wake kuwa mpaka sasa mradi huo unaendelea vizuri kwa asilimia 77 na fedha zote za mradi zilizotolewa zimekwisha tumika.

Kwa mujibu wa Kilawila, ndani ya mradi huo ipo miradi mingine midogo midogo kama vile ujenzi wa ofisi ya wafanyakazi wa mradi na wageni watakaofika kutembelea mradi huo ambao umekwisha kamilika pamoja na ujenzi wa bwawa la samaki.

"Kimsingi kupitia mpango huu, jumla ya miti 9,000 inatarajiwa kupandwa katika kitalu hiki, ambapo upandaji unafanyika kwa awamu. Awamu ya kwanza imehusisha jumla ya miti 4,000 katika 'shade' mbili ambapo kila moja ina miti 2, 000," alisema.

Pia alisema miti inayopandwa ni miti ya asili na matunda na kwamba miche hiyo ikiwa tayari itagawanywa kwa wananchi.

Pamoja na mambo mengine, alisisitiza kuwa lengo mahususi la mpango huo ni kutunza mazingira kwa kuhamasisha watu kupanda miti na kutunza vyanzo vya maji.




Gari la kubebea wagonjwa la Kituo cha Afya cha Shimbwe, kilichopo Halmashauri ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, likitumika kubeba samani za ofisi, juzi, ikiwa ni zoezi la kuhamishia halmashauri hiyo katika majengo ya iliyokuwa shule ya Sekondari ya Kolila, kutii agizo la Rais Dk. John Magufuli la kutaka halmashauri zote kuhamia katika eneo lao la kiutawala. **PICHA: PAUL WILLIAM**

# Wapinzani wakata rufani uchaguzi mitaa

**Na Paul William,** MOSHI

WIMBI la vyama vya upinzani katika mkoa wa Kilimanjaro kudaiwa kushindwa kuchukua na kurejesha fomu za wagombea wa nafasi ya uenyekiti wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji katika Wilaya za Mwanga, Rombo na Moshi Vijijini limeendelea kuripotiwa, huku kukiwa na taarifa kwamba vyama hivyo vimeamua kukata rufani kupinga hali hiyo.

Katika Wilaya ya Mwanga, Msimamizi wa Uchaguzi, Erick Kaaya, alisema wilaya hiyo yenye vijiji 72 na vitongoji 282, wagombea 49 wa nafasi ya uenyekiti wa wa vijiji wamepita bila kupingwa na wagombea 224 wa vitongoji kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamepita bila kupigwa.

Alisema sababu za kupita kwa wagombea hao bila kupigwa ni kutokana na wanachama wa vyama vya upinzani kutojitokeza kuchukua fomu, huku wengine wakishindwa kurejesha.

Katika Jimbo la Rombo, Msimamizi wa Uchaguzi, David Rubibira, alisema wagombea vijiji 63 na vitongoji 293 wamepita bila kupigwa na wote hao ni wa CCM.

Kwa mujibu wa Rubibira, wilaya hiyo ina vijiji 68 na vitongoji 312 na kwamba zoezi la uchukuaji na urejeshaji wa fomu kwa wagombea kwa kufuata kanuni za uchaguzi wa mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa halmashauri ya kijiji na mwenyekiti wa kitongoji, linafanywa kwa mujibu wa kanuni ya 17, kanuni ndogo ya (1) na ya (2).

Kuhusu suala la udhamini wa vyama vya siasa kwa wagombea, kwa mujibu wa mwongozo wa uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2019 umezingatia kwamba, kila chama kina utaratibu wake wa kuteua au kutoa udhamini kwa wagombea wake.

Kwa upande wa Jimbo la Moshi Vijijini, Msimamizi wa Uchaguzi, Juma Tukosa, alisema eneo hilo lina vijiji 157 na vitongoji 700.

Alisema katika jimbo hilo, wagombea wa nafasi ya uenyekiti wa kijiji waliopita bila kupingwa ni 57 na vitongoji ni 201 na wote wanatoka CCM.

## Wavuvi haramu wapewa salamu

**Na Paul William,** MWANGA

SERIKALI imesema kuanzia sasa, haitawatoza tena faini wavuvi watakaokamatwa wakiendesha shughuli za uvuvi haramu katika Bwawa la Nyumba ya Mungu liliko kati ya mikoa ya Kilimanjaro na Manyara, badala yake itawaburuza kortini.

Uamuzi huo ulitangazwa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Thomas Apson, ikiwa siku moja baada ya kunaswa kwa vyandarua vya kuzuia malaria vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 39.3 ambavyo vilikuwa vitumike kuvua mazalia ya samaki wachanga.

"Kwa sasa serikali tumejipanga kuhakikisha tunakomesha biashara hii ya uvuvi haramu na njia pekee tutakayokuwa tukiitumia kwa sasa tunapowakamata hatutawatoza tena faini, bali tutawafikisha mahakamani ili mkahukumiwe kutumikia kifungo jela. Uamuzi huu tunaamini kwamba utasaidia kukomesha biashara hii," alisema.

Katika operesheni Jodari na Sangawe zinazoendelea katika bwawa hilo, makokoro 12 na vyandarua vya malaria vilikamatwa na kuteketezwa.

Apson alisema uvuvi haramu katika eneo linalozunguka Bwawa la Nyumba ya Mungu umekuwa ukishika kasi na hii ni kutokana na wavuvi hao haramu wanapokamatwa hutozwa faini na kisha kuachiwa huru.

Mkuu huyo wa wilaya alisema wananchi ambao wamekuwa wakifanya uvuvi haramu wamekuwa wakilitisha Jeshi la Polisi pindi wanapotekeleza majukumu yao ya kuzuia biashara hiyo na kwamba mpaka sasa watu 14 wanashikiliwa kwa tuhuma hizo.

Alisema endapo wananchi watafanya uvuvi kwa kufuata sheria, serikali itawasaidia kupata soko la uhakika la uuzaji wa samaki ndani na nje ya nchi lengo likiwa ni kuinua maendeleo ya wananchi wanaozunguka bwawa hilo na taifa kwa ujumla kwa kulipa kodi.

Alisema Nyumba ya Mungu ni bwawa la thamani sana, lakini limekuwa likitumika vibaya kwa shughuli haramu na kudai kuwa kwa sasa serikali inataka kuja na mpango wa kutafuta wawekezaji watakaojenga hoteli za kitalii katika eneo la bwawa hilo ili litumike kama sehemu ya utalii.

Ofisa Tarafa ya Lembeni, Gikila Maduhu, alisema nyavu hizo haramu zilikamatwa baada ya kufanyika kwa msako wa kushtukiza wa nyumba kwa nyumba katika vijiji vinavyozunguka bwawa hilo kwa upande wa Wilaya ya Mwanga.

Maduhu alisema lengo la msako huo ni kuhakikisha wanalinda maslahi ya bwawa hilo kwa kizazi cha sasa na kichokuja ambapo wamekuwa wakipitia kipindi kigumu kwa kutishiwa na wananchi wanaofanya biashara za uvuvi haramu.

ama
ALHAMISI NOVEMBA 7, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

## Mazoezi Yoga sasa hatari kwa afya



Robi: Sioni haya kusema nimekeketwa Ukurasa 16



Ukurasa 19

## Ukatili unavyoweka njiapanda hatima afya za watoto wengi

Distributed via ippmedia



# Mabingwa walia hatari kiharusi kwa wazee, vijana hadi vichanga

Ukurasa 18

# Mazoezi Yoga sasa hatari kwa afya

**Na Mwandishi Wetu**

MAZOEZI ya viungo vya mwili, hivi sasa inashika kasi duniani. Washiriki wake wakiwa wa idadi ya mamilioni, hasa kupitia mchezo wa Yoga, ambao pia unaendana imani katika baadhi ya jamii .

Kiafya, Yoga manufaa yake inatajwa pia inajumuisha kuuweka mwili kwa usawa. Lakini kama usemi unavyonena duniani 'kizuri hakikosi kasoro' sasa inatajwa kuwapo walakini kiafya, pindi mhusika anaopojikita zaidi katika mchezo huo.

Mkufunzi na Mtafiti, Benoy Matthews, kutoka nchini Uingereza, anasema sasa kumeonekana idadi kubwa ya kundi katika umma wanaokutwa na madhara kutokana na kushiriki Yoga.

Anasema, kadri mtu anavyojikita zaidi kuvuta na kunyoosha sehemu za mwili, miili yao inaingia katika hatari ya kuathirika, hata wanalazimika kufanyiwa upasuaji wa mwili.

Mkufunzi Matthews, aliyebobea kitaalamu katika masuala ya maozezi ya viungo vya binadamu, anasema hadi sasa kuna kati ya walimu wanne hadi watano walioathirika kiafya kutokana na ushiriki wao katika mafunzo ya mazoezi hayo kila mwezi.

Anasema, katika kundi hilo zaidi ya nusu wanahitaji zaidi ushauri tu, namna ya kufanya mazoezi ili kuondokana na madhara hayo ya kimwili, kwani kuna aina ya mazoezi viungo vinalazimishwa yasiyowezekana, mathalani kujikunja sana katika baadhi ya viungo visivyokunjika.



Mtu akifanya mazoezi ya Yoga. **PICHA: MTANDAO**

AFYA

SIKU 54 ZA BILA FAINI...

# Ujenzi wa vyoo kitendawili kigumu kwa wakazi Kahama

## • Tozo laki tano, papo kwa hapo




Wananchi wa Kahama wakimsikiliza Mkuu wa Mkoa, Zainabu Tellack, alipotoa maagizo kila nyumba kuwa na choo bora.

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHOO ni sehemu muhimu kwa binadamu. Inapaswa kuangaliwa kwa karibu zaidi hasa makazi, ili kujikinga na magonjwa ya kuambukiza yatokanayo na shughuli zinazofanyika katika sehemu hiyo.

Serikali nchini imekuwa ikitumia zaidi ya Sh. bilioni 400 kutibu magonjwa yanayotokana na watu kukosa vyoo bora. Bado kuna kundi kubwa katika jamii ambalo halina vyoo bora, mjini na vijijini.

Fedha ambazo zingeelekezwa kwenye sekta ya maji kupunguza ukosefu wake na kutekeleza mkakati wa Rais Dk. John Magufuli, kumtua mwanamke ndoo.

Inaelezwa mbali na malaria, kuna magonjwa yanayosababishwa na maji, ikiwamo kipindupindu yako juu kwa jamii katika maeneo mbalimbali.

> "Mkoa wetu ndugu zangu ni tajiri sana kwa kuwa una rasilimali nyingi za madini ya dhahabu, almasi na mazao mbalimbali.

Kundi lisilo na vyoo lina tabia ya kujisaidia vichakani, kutiririsha majitaka wakati wa mvua ama kwenye mifuko na kutupa ovyo na wakati wa mvua, uchafu wote huelekea kwenye vyanzo vya maji vinavyotumiwa na wananchi. Hicho kinatajwa kuwa chanzo kikuu kukithiri magonjwa ya mlipuko.

Ongezeko la magonjwa yanayotokana ya uchafu na kuligharimu Taifa fedha nyingi kuyatibu, inaathiri utekelezaji wa dhana ya Tanzania ya Viwanda, pia Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu, hususan ya tatu na sita la uboreshaji afya, ustawi wa jamii na upatikanaji huduma za maji safi na salama na usafi wa mazingira.

Kumeshuhudiwa maeneo mengi vijijini, kuna nyumba zisizo na vyoo, hali inayowafanya wananchi wengi kujisaidia vichakani, wakiishia na mlipuko wa magonjwa ya kuhara, asilimia kubwa ni watoto wadogo.

### HATUA ZINAZOCHUKULIWA

Hivi sasa mijini kumeanzishwa huduma za vyoo vya kulipia, lengo lake kubwa ni kuondokana na uharibifu wa mazingira unaoweza kujitokeza kwa watu kujisaidia ovyo, hivyo kuwapo uwezekano wa kuibuka magonjwa hatari.

Pia, serikali ililiona na kuanzisha kampeni ya kitaifa iitwayo: 'Nyumba ni Choo Usichukulie Poa' ilipitia katika mikoa, wilaya, halmashauri tofauti hadi vijijini lengo ni kutoa elimu ya umuhimu wa kuwa na vyoo bora na kujikinga na maradhi yanayopatikana.

Pia, kutokuwapo vyoo bora kunaleta madhara yasiyoishia kwa mwenye nyumba tu, bali majirani na hasa wakati wa mvua, vyoo hujaa na kuleta kero kubwa kwa umma, pindi inapotiririsha majitaka kwa wananchi na kusababisha kuibuka magonjwa.

### MKUU WA MKOA

Zainabu Telalck, ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga. Anaahidi kuchukulia hatua za kisheria kaya zitakazobainika kukosa vyoo bora, kwa kuwatoza faini ya kiasi cha Sh. 500,000. Muda uliotolewa kujirekebisha ni hadi Desemba 31, mwaka huu.

"Mkoa wetu ndugu zangu ni tajiri sana kwa kuwa rasilimali nyingi za madini ya dhahabu, almasi na mazao mbalimbali. Hivyo, ni aibu kusikia bado kuna kaya ambazo hazina vyoo na wananchi mkiendelea kujisaida vichakani," anasema Tellack.

Mkuu wa Mkoa, anasema serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka, bajeti ya kupambana na maradhi yanayotibika kutokana na athari hizo, huko wananchi wasiojenga vyoo wanaendelea kutumia dawa za kutibu maradhi ya kujitakia.

Anasema dawa zingine zinazotumiwa zina madhara na anawasihi wananchi kuepuka matumizi ya dawa, kwa matatizo yanayotokana na uchafu utokanao na ukosefu wa vyoo.

Mkuu wa Mkoa anawataka wakuu wa shule za msingi na sekondari mkoani kwake kuhakikisha wananunua sabuni na ndoo za kuwekea maji, wanafunzi wanawe mikono wanapotoka chooni, ili kuzuia magonjwa ya mlipuko kama vile kuhara damu.

Pia, anawaasa walimu kuwaelimisha wanafunzi umuhimu wa kuwa na vyoo bora katika familia, ili wageuke mabalozi kwenye familia na jamii zao, hali itakayowafanya wazazi kujenga vyoo, kupitia elimu kutoka kwa watoto wao.

### KATIBU TAWALA

Timoth Ndaya, ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, anasema Halmashauri ya Mji wa Kahama, ina jumla ya kaya 55,708 na kati yao wenye vyoo bora ni asilimia 75 na zisizokuwa na vyoo ni asil-

AFYA

# Ujenzi wa vyoo kitendawili kigumu kwa wakazi Kahama

imia 0.2.

Ndaya anasema, katika Halmashauri ya Msalala, kuna kaya 40,920 kaya zenye vyoo bora, ambayo ni asilimia 57.3 na kaya zisizokuwa na vyoo asilimia 4.4

Pia, Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ina jumla ya kaya 49027, kati yao wenye vyoo ni asilimia 2.9 na kaya zisizo na vyoo, zinachukua asilimia 5.1.

**MRATIBU MAZINGIRA**

Mratibu Mkuu wa Kampeni ya Usafi na Mazingira kitaifa, Anjitike Mwakatalima, anasema wamezitembelea Halmashauri 43; kata 181; na vijiji 877 kati ya 4,400 vilivyopo katika mikoa ya Mara, Mwanza, Geita, Simiyu, Shinyanga na wakatoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa choo.

Anasema, kila siku kuna watu 6,000 wanaokula kinyesi kulingana na mazingira waliyopo na watoto chini ya miaka mitatu ndio wanaoongoza kuwa na magonjwa yanayotokana na ukosefu wa vyoo au kutokuwa na choo bora.

Ni takwimu anazoelekeza mbali kwamba, kila dakika kuna vifo vinne katika maeneo hayo, kutokana na madhara hayo na havitolewi taarifa.

"Mkoa wa Songwe ulikuwa wa pili kutoka chini kati ya mikoa isiyokuwa na vyoo bora na kaya zisizokuwa na vyoo kabisa, lakini kwa sasa wapo katika mikoa mitano yenye vyoo bora na kutokana na kuendelea kuwahimiza wananchi juu ya umuhimu wa vyoo," anasema Mwakatalima.

Anaongeza kuwa, katika kila watu 100, kuna 20 kati yao wanakula bila ya kunawa mikono kwa majisafi na sabuni na wengine hunawa baada ya kumaliza kula.

Mwakatalima anawataka kuhakikisha wananawa mikono baada ya kutoka chooni na kabla ya kuanza kula, ili kujikinga na maradhi.

**DIWANI MAJENGO**

Benard Mahongo, ni Diwani wa Kata ya Majengo katika Halmashauri ya Mji Kahama, anasema jiografia ya eneo lake lipo bondeni, hivyo mvua zinapoanza kunyesha, wananchi hutiririsha maji ya vyoo na hali inyakuwa mbaya kwa wakazi wa huko na maeneo jirani.

Mahongo anasema, Wilaya ya Kahama ina wakazi wengi wanaojenga nyumba kila kukicha, lakini miundombinu ya vyoo imekuwa sio rafiki kwa wanaoishi katika maeneo yao.

Anasema, agizo la kisheria kwa wananchi wa Wilaya ya Kahama, kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Zainab Telack, ni kwamba hadi ifikikapo Desemba 31 mwaka huu, kaya itakayobainika haina choo bora itatozwa faini.

Mahongo anawataka wakazi wa eneo la Majengo kuhakikisha wanajenga vyoo bora na kuvifanyia usafi wa kila mara, hali inayosaidia kuondoa magonjwa ya mlipuko kwa watoto wadogo, wakijengewa tabia ya kunawa, pindi wanapotoka na kuingia chooni.

Anaeleza matarajio yake ni kuona Kata ya Majengo inakuwa ya kwanza katika Halmashauri ya mji wa Kahama na vyoo bora.

Rai ya diwani hiyo kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, kuwasisitiza wahusika wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini Tanzania (Tarura), kuwajengea miundombinu mizuri ya maji, ili mvua zinaponyeshea maji, yasiweze kwenda katika makazi ya watu.

**MIFUMO MAJITAKA**

Mahongo aliiomba Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (Kuwasa), kuharakisha kuwekwa kitengo cha majitaka, ili kuondoa kero za uzoaji majitaka, ambazo kwa sasa zimekuwa zikishikiliwa na kampuni ya watu binafsi, inayowatoza wananchi bei kubwa.

"Kama Kuwasa itaanzisha kitengo cha maji taka, hii inaweza ikawa msaada mkubwa kwa wananchi wa Mji wa Kahama, kwani kwa sasa wanalazimika kutozwa kiasi kikubwa cha fedha na kampuni ambayo yanajihusisha na unyonyaji maji hayo, huku watu wengi wasiweze kumudu gharama zake," anasema Mahongo.

Anasema kuwa, kutokuwa na kitengo cha maji taka katika Mamlaka hiyo ni moja ya changamoto kubwa kwao kwani wananchi wamekuwa wakitiririsha maji machafu ovyo kutoka katika majumba yao hasa wakati wa mvua za masika.

Mahongo anasema, wamiliki wa magari ya maji taka wanawatoza wananchi kiasi kikubwa cha fedha kuanzia kiasi cha Sh. 60,000 hadi 80,000 tofauti na Mamlaka hiyo ingekuwa na kitengo hicho ingekuwa ni gharama nafuu.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Tellack, akizungumza na wakazi wa Halmashauri ya Mji Kahama, wakati wa kufunga kampeni ya nyumba ni choo, iliyofanyika katika viwanja vya Kata ya Majengo, mjini hapa. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

> **Dawa zingine zinazotumiwa zina madhara na anawasihi wananchi kuepuka matumizi ya dawa kwa matatizo yanayotokana na uchafu utokanao na ukosefu wa vyoo.**



Mratibu Mkuu wa kampeni ya Usafi na Mazingira Kitaifa, Anjitike Mwakatalima, akiwaeleza wananchi wa Halmashauri ya Mji Kahama, umuhimu wa choo bora, wakati wa kufunga kampeni ya nyumba ni choo.

AFYA

# Robi: Sioni haya kusema nimekeketwa

**Na Sabato Kasika**

• Kilichomkuta rafiki yake hakisahauliki • Mke mwenye watoto, askari vita ukeketaji

KUNA baadhi ya waliofanyiwa ukatili wa kukeketwa na hawako tayari kusema hadharani, kuwa wamefanyiwa ukatili huo. Wana sababu mbalimbali za kunyamaza huko.

Lakini kwa Robi Samwel ni tofauti kabisa. Yuko wazi na haoni aibu kusema kwamba amefanyiwa ukatili huo, ambao sasa anapingana nao kwa nguvu zake zote ili kuhakikisha unakoma kwenye jamii yake.

Huyu si mwingine, bali ni Mkurugenzi wa Shirika la Matumaini kwa Wanawake na Wasichana Tanzania au kwa Kizungu 'Hope For Girls And Women Tanzania' lenye maskani yake, Mugumu Serengeti, mkoani Mara.

Shirika hilo linafanya kazi ya kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya ukeketaji, pia lina vituo kwa ajili ya wasichana wanaokimbia kutoka nyumbani, kukwepa kukeketwa.

Wasichana hao wanaokimbia kukwepa kukeketwa wakiwamo hata watoto wadogo wanaookolewa na wadau mbalimbali, wamekuwa wakitunzwa katika vituo vya shirika hilo viitwavyo 'Nyumba Salama' ilivyopo Mgumu na Butiama, mkoani Mara.

Robi mwenye mume na watoto watatu; wawili ni mabinti, anasema haoni sababu inayomzuia kutamka hadharani kwamba amekeketwa, wakati ukweli unasimama kwamba amefanyiwa kitendo hicho.

"Kwa nini nifiche wakati nimekeketwa? Ninafanya kazi ya kupingana na vitendo hivi, kwa hiyo ni lazima niwe wazi kwa umma ili ujue madhara ya ukeketaji na kuachana na mila hizo potofu," anaasema Robi.

Robi ambaye kitaaluma ni mwalimu, anasema pamoja na kwamba amekeketwa, lakini watoto wake hawajafanyiwa ukatili huo, kwa vile yeye na mume wake wamewalea katika mazingira yasioendana na mila potofu.

### HARAKATI ZAKE

Anasema, yeye ni mwalimu wa shule msingi aliyetihimu katika Chuo cha Ualimu Bunda, mkoani Mara mwaka 1993 na kutunukiwa cheti cha ualimu, lakini hakushika chaki. Aliamua kuwa mpambanaji wa mila potofu za ukeketeji.

Katika simulizi hiyo, anasema alikataa kushika chaki kwa sababu yeye ni miongoni mwa waathirika wa ukeketaji, aliona ni bora ajikite zaidi kutoa elimu inayohusu madhara ya ukeketaji.

Anasema kulikuwapo madai utotoni, kwamba huenda hata anayefariki kwa kukeketwa hazikwi, badala yake anatelekezwa, jambo ambalo Robi anasema liliwakaa sana mabinti.

"Kwanza kabisa, enzi hizo nikiwa darasa la tano mwaka 1984 nilikuwa na rafiki yangu ( jina tunalo) , ambaye alifariki dunia baada ya kukeketwa na kutokwa damu nyingi. Tukio hilo liliniuma sana tena sana." Robi anasimulia.

Anaendelea huku akionyesha hisia za kuumia nafsi, anasimulia:



Vijana wanaolelewa katika Kituo cha Nyumba Salama, mjini Mugumu, Serengeti, wakifanya mapitio ya baadhi ya kazi zitokanazo na malezi yao.

> **Juhudi zangu za kukataa mila hizo potofu hazikuzaa matunda, ndipo nikakeketwa na kuzimia kwa zaidi ya saa nne, baada ya kutokwa damu nyingi, ikaifanya sherehe yao kugeuka msiba.**



Robi Samwel akiwa na watoto wanaolelewa katika kituo chake.



Robi Samwel akiwa ofisini kwake, mjini Mugumu, Serengeti. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

"Tukio hilo lilinikaa moyoni hadi leo, kwani... ndiye mwanafunzi pekee kijijini kwetu aliyefaulu kwenda sekondari, lakini tayari alishafariki baada ya kukeketwa."

### ZAMU YAKE

Robi anasema mwaka 1986 alipohitimu elimu ya msingi, alipokuwa anasubiri matokeo, mama yake alimwambia ni zamu yake kukeketwa, hali iliyomuongezea machungu.

Anasimulia alivyotapatapa kumpinga mama yake katika hoja hiyo, lilimjia wazo la kutoroka nyumbani, lakini akakosa mahali pa kukimbilia. Alilazimika kubaki nyumbani akisubiri matokeo ya mtihani wa darasa la saba.

"Baadaye nilikwenda kwa shangazi kumweleza jinsi ninavyoambiwa na mama kwamba 'ni lazima nikeketwe, cha ajabu shangazi naye akaungana na wazazi kuwa ni lazima nikeketwe," anasema.

Anasema baada ya kukwama kwa hilo, hakuwa na jinsi, alirudi kwa wazazi wake na ndipo siku ya kukeketwa ikafika. Walikusanywa wasichana 16 na ngariba wawili, lakini mmoja alikuwa maalum kwa ajili yake (Robi).

"Juhudi zangu za kukataa mila hizo potofu hazikuzaa matunda, ndipo nikakeketwa na kuzimia kwa zaidi ya saa nne, baada ya kutokwa damu nyingi, ikaifanya sherehe yao kugeuka msiba," anasema.

Robi anasema, pamoja na matokeo ya mtihani alipochaguliwa kwenda sekondari, alikutana na vipingamizi vikiwamo vya kuambiwa aache shule, ili aolewe wazazi wapate mali.

### ELIMU SEKONDARI

Robi anasema, matokeo ya mtihani wa darasa la saba yalitoka akiwa amechaguliwa kwenda Sekondari ya Maswa Girls mkoani Shinyanga, tayari akiwa ameshakeketwa.

"Pamoja na kufaulu, babu yangu alitaka niolewe kwa vile nimeshakeketwa, huku baba akidai hana fedha za kunisomesha, lakini sikukubaliana na hilo na ndipo (baba) mwishowe akakubali nisome," anasema.

Anasema alianza kidato cha kwanza mwaka 1987 na kuhitimu kidato cha nne mwaka 1990 na kufaulu kuendelea na kidato cha tano, lakini baba yake akabadilisha akasome ualimu.

"Nilipata nafasi nne, zikiwamo za (vyuo) Ufundi Mbeya, Kilimo na Mifugo Nyegezi na Chuo cha Ualimu Bunda, akasema niende chuo cha ualimu, kwa madai nitasoma bure yeye hana fedha za kunisomesha," anasema.

Robi anasema, baada ya miaka kadha ya ubishani nyumbani, mwaka 1992 alijiunga cha Chuo Ualimu Bunda na akahitimu ngazi ya cheti ya ualimu shule ya msingi, mwaka 1993.

Anasimulia, mwaka 1994 alijiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), kambi ya Buhemba kwa kipindi cha miezi sita na anaendelea:.

"Mwaka 2000 nilianza (masomo) Foundation Course (Mafunzo Cheti cha Msingi) katika Chuo Kikuu Huria tawi la Musoma na kupata alama za kuniwezesha kujiunga na chuo kikuu (Huria) na kuanza masomo na kuhitimu digirii ya Utawala wa Biashara na Elimu," anasema.

Mkurugenzi huyo anazieleza jitihada zake zina mafanikio, kwani amefanikisha yote binafsi aliyonuia, sambamba na harakati za umma za kurudi nyumbani (Mugumu) kupambana na ukeketeji aliofanyiwa, pia kumdhuru rafiki yake, utotoni wakiwa shule ya msingi.

### ALIANZA VITA SHULENI

Robi anasema, alianza harakati za kupambana na ukeketaji muda mrefu alipokuwa shuleni na kwenye jamii kuelimisha madhara ya ukeketaji, na kuitikiwa vizuri.

"Mwitikio ulikuwa mzuri, kwani baadhi ya watoto walikuwa wakinitafuta na kutaka niwachukue nikae nao, ili wasikeketwe. Hii ilikuwa ni changamoto kwangu, kwa sababu sikuwa na sehemu ya kuwaweka," anasema.

Anasema, alilazimika kupita nyumba za wazazi wenye watoto hao na kuwaeleza madhara ya kukumbatia mila hizo zilizopitwa na wakati na wapo waliomuelewa na kuachana nayo.

"Mwaka 2017 nilianzisha shirika hili na tumekuwa tukishirikiana na wadau mbalimbali kuanzia ofisi ya Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Serengeti, dawati la jinsia na wadau wengine," anasema Robi.

> **Mwaka 2000 nilianza (masomo) Foundation Course (Mafunzo Cheti cha Msingi) katika Chuo Kikuu Huria tawi la Musoma..**

Anasema, juhudi hizo zimesaidia kuokoa watoto zaidi ya 600 na bado wanaendelea kutoa elimu ili kuhakikisha mila hizo potofu zinakoma wilayani Serengeti na kuwafanya watoto wa kike wawe huru.

Robi anasema aliamua kutoa elimu hiyo nyumbani kwao Wilaya ya Serengeti, alikoamua kuweka kambi ya kudumu kushirikiana na wadau wengine, kutokomeza mila.

Katika mikakati iliyoko, anasema shirika limepania kuhakikisha watoto wanaookolewa na kutunzwa katika vituo vya shirika hilo, wanasoma na wengine kufundishwa ufundi wa nguo na ujasiriamali, wajitegemee.

## Saratani Matiti bado janga, kinababa nao...




Mkurugenzi wa Huduma ya Kinga ya Saratani katika Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dk.Crispian Kahesa, **PICHA: YASMINE PRTOTACE**

**Na Yasmine Ptotace**

SARATANI ya matiti ni aina ya ugonjwa unaosababisha ukuaji chembehai za binadamu, zinakua bila ya utaratibu maaaum. Dalili ya awali inayotambulisha ni kuwapo uvimbe

Hiyo ndio inatajwa inaufanya umma kujenga utamaduni wa kuangalia afya zao kila mara na endapo mtu angundulika kuwa na tatizo, iko wazi kwamba kunahitajika jitihada za matibabu ya haraka, kumsaidia mgonjwa arudie hali yake ya zamani.

Pamoja na matamko mbalimbali kuitaka jamii kujenga utamaduni wa kuchunguza afya, bado kuna makundi mawili; upande mmoja wamekuwa wakifanya hivyo na wengine wamekuwa wanasuasua.

Kimsingi, kuchunguza afya kunaelezwa kuna faida kubwa na mtu anapogundulika kuwa na tatizo hilo mapema ni rahisi kusaidiwa.

Pia kuna angalizo kwa wanaokuwa na tabia ya kuficha matatizo, mara nyingi hujikuta wanaishia katika kuharibikiwa na hata wanapoenda kupata tiba bila kuchukua hatua walishapata matatizo makubwa.

Hivyo basi, hapo ndipo kunaelezwa kuzaa haja ya hitaji la ushauri unatolewa na hata panapokuwapo huduma za bure, jamii inapotakiwa kwenda kupata huduma hizo, wanajenga utamaduni wa kujitolea kuchunguzwa afya, inayoishia kumsaidia mtu kujifahamu tatizo lake.

Mtu anaweza kuhisi ana tatizo, lakini pale unapoenda kuchunguzwa afya, inamfugulia picha pana na mtu anapogundulika anaumwa anaweza kudhibiti hatari ya kutumia fedha nyingi kujitibu.

Mkurugenzi wa Huduma za Kinga ya Saratani, katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI) Dk. Crispian Kahesa, anasema mgonjwa anapogundulika mapema kinachomsibu mara nyingi matibabu yake hayachukui muda mrefu.

Hivyo basi, anaasa magonjwa yanayohusu saratani ya matiti, tukio kama uvimbe katika matiti, anaitaka jamii isikimbilie maduka ya dawa au mbadala mwingine, bali kinachotakiwa ni kufika hospitali kuanza huduma za matibabu .

Imeelezwa, endapo hatua zisipochukuliwa za saratani ya matiti kudhibitiwa, inaweza kuongezeka na kushika nafasi ya juu katika magonjwa yenye madhara makubwa kitaifa.

Dk. Kahesa alitamka hayo, alipozungumzia mwezi wa uhamasishaji, uelimishaji na uchunguzi wa saratani unaoadhimishwa kila mwezi Oktoba.

Anafafanua: "Idadi ya saratani ya matiti inaonekana kuongezeka nchini ambapo hivi sasa wanawake wenye umri kuanzia miaka 20 na kuendelea nao wanagundulika kuugua ugonjwa huu."

Dk. Kahesa anatahadharisha, endapo hatua zisipochukuliwa, saratani hiyo itazidi kuwa tishio akidokeza idadi kubwa ya wagonjwa wanaofika hospitalini kwake wanatoka katika maeneo ya mjini, Mkoa wa Dar es salaam ukiwa kinara.

"Tathimini ya miaka 10 iliyopita, saratani hii ilikua inashika nafasi ya tano. Hivi sasa ni ya pili kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa, zamani tulikuwa tunawaona wagonjwa kuanzia miaka 55 kashuka hadi miaka 50 na sasa tunaona hadi wenye umri miaka 20," anasema.

Dk. Kahesa anaongeza, kwa mwaka huu pekee wameona wanawake 1,443 na kati yao 342 wamekutwa na uvimbe 170 walikuwa na dalili za awali za saratani.

Kwa upande wa saratani kwa wanaume, Dk. Kahesa anasema inaathiri asilimia moja ya wanaume, hata hivyo kwa upande wao ni hatari zaidi, endapo isipogundulika inaweza kuathiri mapafu yao kwa haraka.

"Saratani hii huathiri wanawake zaidi kuliko wanaume kwa asilimia 99 na wanaume asilimia moja tu. Dalili kwa wanaume ni tofauti kidogo na wanawake, hivyo kwa mwanaume ni rahisi kugundua kuliko mwanamke kwa kuwa kifua chake kina mafuta mengi,' anaeleza.

Pia, anaongeza kati ya wanawake 170 waliofanyiwa vipimo, zaidi ya 68 waligundulika kuwa na uvimbe ambao ni wa saratani.

Nchini hivi sasa, inaelezwa saratani ya shingo ya kizazi inaongoza, zinafuatia saratani za: Matiti, njia ya chakula na tezi dume na saratani aina nyingine zinazoathiri mfumo wa kinga.

AFYA

# Mabingwa walia hatari kiharusi kwa wazee, vijana hadi vichanga

## • Daktari: Kitambi chako ni salamu • Mlo, pombe, sigara, 'no'mazoezi



Bingwa wa magonjwa ya mishipa ya fahamu, ubongo na uti wa mgongo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Patience Njenje, alipozungumza kuhusu siku ya kiharusi inayoadhimishwa kila Oktoba 29 ya mwaka. Kulia ni mtaalamu wa fani hiyo kwa watoto, Dk. Zameer Fakih na kushoto, Dk. Mohammed Mnacho mwenye fani inayofanana na mzungumzaji. **PICHA: TOVUTI YA MNH.**

**Na Romana Mallya**

MABADILIKO ya maisha yanayochangiwa na matumizi ya pombe, sigara, kula bila mpangilio, uzito mkubwa kupita kiasi ni sababu zinazotajwa na wataalam wa afya kusababisha kuwapo ongezeko la wagonjwa wa kiharusi.

Takwimu za dunia zinakitaja kiharusi kwa sasa inashika nafasi ya pili kusababisha vifo kwa asilimia 11.8, baada ya magonjwa ya moyo.

Pamoja na hali kuwa mbaya na kiharusi kuwa tishio kwa makundi yote yaani watoto, vijana, watu wazima na wazee, hadi sasa Tanzania haijafanya utafiti wa kuwezesha kupata takwimu sahihi zinazoonyesha idadi kamili wanaougua nchi nzima.

Wataalam wa afya wanasema, takwimu hazipo kwa sababu kiharusi ni miongoni mwa magonjwa yasiyoambukiza, ambayo kwa muda mrefu yalikuwa yameachwa nyuma ingawa sasa ndiyo yanayoongoza kwa kuua.

### DAKTARI BINGWA

Daktari bingwa wa mishipa ya fahamu, ubongo na uti wa mgongo, kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, (MNH), Patience Njenje, anasema shida ya ugonjwa wa kiharusi inazidi kuongezeka kila siku inayopita.

Anasema zamani watu walishughulika na magonjwa ya kuambukiza, yakiwamo malaria, ukimwi na yakasahaulika magonjwa yasiyoambukiza.

"Kusahau huku ni katika ngazi zote kuanzia juu hadi chini na huku chini, tunafikiri kwamba ugonjwa wa kiharusi ni wa kurogwa. Watu watambue kuwa kisababishi kikubwa ni mfumo wa maisha.

"Zamani shida hii ilikuwa ikijitokeza nchi za Ulaya, huku tulikuwa na magonjwa mengine ya kuambukiza, lakini sasa kiharusi kinakuja kwa kasi, kwa sababu ya mfumo wa maisha," anasema

> Endapo mtoto akiwahishwa hospitalini chini ya saa sita, matibabu huwa rahisi zaidi na anapocheleweshwa kunahitajika upasuaji.

Anafafanua kwamba, ugonjwa huo unachochewa na mfumo wa maisha kwa sababu watu wanatumia magari muda mrefu, bila ya kufanya mazoezi na kula ovyo.

"Mtu hafanyi mazoezi, anatumia gari wakati wote, anakula chipsi na vyakula vingine vinavyosababisha mwili kuongezeka kupita kiasi na mwisho wa siku kupata shinikizo la juu la damu, ambalo matokeo yake ni kiharusi. Tiba kubwa ya kiharusi ni kuzuia mtu asiupate."

### KULIVYO MUHIMBILI

Dk. Njenje anasema kwa siku, hospitali hiyo imekuwa ikipokea kati ya wagonjwa watatu hadi watano wenye kiharusi.

Ni kauli yake katika maadhimisho ya Siku ya Kiharusi Duniani, ambayo inafanyika kila mwaka Oktoba 29, akifafanua kwamba ugonjwa huo unashika nafasi ya tatu katika kusababisha ulemavu duniani; asilimia 4.5 ya walemavu wote duniani.

"Tafiti nyingi zimefanyika kwa magonjwa ya kuambukiza, hivyo tuna takwimu chache sana kwa magonjwa kama kiharusi hasa Tanzania hatuna takwimu. Nyingi tulizo nazo ni zile za kuwaona wagonjwa wanaokuja hospitali kwa siku.

"Kwa siku watu wazima wanapokelewa hospitali ya Muhimbili, huwa tunapata wagonjwa watatu mpaka watano wenye kiharusi," anasema.

### KINAPATIKANAJE?

Dk.Njenje anaeleza kuwa, mtu anapata kiharusi pale ubongo wake unapokosa hewa na chakula ambacho ni damu inayosafirishwa kupitia mishipa. Anafafanua:

"Kuna wakati mishipa hii huziba au hupasuka, mtu akipata hiyo hali anaweza kukosa nguvu upande mmoja. Kama imepasuka upande wa kushoto, utakosa nguvu upande wa kulia, madhara makubwa ni kifo au kupata ulemavu."

Aidha, anasema takwimu za sasa duniani zinaonyesha kiharusi kinashika nafasi ya pili katika kusababisha kifo, lakini zamani kilikuwa nafasi ya mbali kidogo.

"Maana yake, kiharusi kinazidi kusogea na hatuombei, kinaweza kuvuka na kupita magonjwa ya moyo. Wengi wanafikiri mtu akipata kiharusi amerogwa, lakini tunataka kuwaelimisha wananchi kuwa matatizo haya yapo na ni jukumu la kila mmoja kuchukua tahadhari kwenye mfumo mzima wa maisha.

"Zamani, matatizo ya kiharusi yalikuwa zaidi nchi za Ulaya, lakini sasa inakuja kwa sababu watu wameiga maisha ya Ulaya, tusiporudi tulikotoka kwa mfumo mzima wa maisha hali itazidi kuwa mbaya," anasema.

Dk. Njenje anasema awali ugonjwa huo ulikuwa ukiwapata watu wenye umri kuanzia miaka 65 na kuendelea, lakini sasa wenye wa miaka 45 kushuka chini nao wanaupata.

Mtaalamu huyo anaendelea kwamba, licha ya sababu za ugonjwa huo kuwapo, lakini baadhi ya watu bado wanaamini unasababishwa na mambo ya kishirikina, ambalo Daktari Njenje analipinga vikali, kwamba siyo sahihi.

"Ugonjwa huu unatibika. Tuondoe imani potofu, tuelimishe wananchi ugonjwa huu hausababishwi na nguvu tofauti, ni ugonjwa kama yalivyo magonjwa mengine," anasema.

### WATOTO HATARINI

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto, Zameer Fakih, anasema kiharusi kwa watoto kinaweza kutokea kabla ya kuzaliwa, wakati wa kuzaliwa na baada ya kuzaliwa.

"Takwimu zinaonyesha kati ya watoto 4,000 wanaozaliwa, mmoja anapata kiharusi wakati akizaliwa. Chini ya umri wa miaka 18 kila mwaka watoto 2,000 wanapata kiharusi kutokana na sababu mbalimbali. Hizi ni tafiti za kidunia," anasema.

Dk. Fakih anaeleza endapo mtoto anayezaliwa akakosa hewa (oksijeni), ana uwezekano wa kupata kiharusi katika siku za baadaye.

"Anaweza kupata degedege ikahusisha upande mmoja wa mwili au mwili mzima au akapata ulemavu upande mmoja, akawa anakakamaa upande mmoja. Anaweza kuonyesha dalili za kushindwa kunyonya au kula sawasawa na wakubwa ambao wanaweza kupata dalili za kukata kauli," anasema.

Pia, anasema endapo mtoto akiwahishwa hospitalini chini ya saa sita, matibabu huwa rahisi zaidi na anapocheleweshwa kunahitajika upasuaji.

Dk. Fakih anabainisha kwamba, watoto wanaoweza kupata kiharusi, ni wale wenye matatizo ya kinachoitwa 'seli mundu' ikifuatiwa na wale wenye matatizo ya 'valvu za moyo.'

"Takwimu za wagonjwa wa ndani hospitali ya Muhimbili zilizoanzia Julai 2018 hadi Julai 2019 zinaonyesha jumla ya watoto waliogundulika kuwa na kiharusi chini ya miaka 14 ni 23.

"Kwenye kliniki ya selimundu inaonekana kila kliniki kati ya mtoto mmoja au wawili wanakuja na tatizo la kiharusi na huwa tayari wameshaanzishiwa dawa," alisema.

Daktari bingwa wa magonjwa ya ubongo na mishipa ya fahamu, Mohamed Mnacho, anasisitiza umuhimu wa kufanyika utafiti zaidi, ili kupata takwimu sahihi kuhusu hali hiyo kwa wakati huu.

Dk. Mnacho anasema utafiti uliofanyika Tanzania na duniani unaonyesha kwa kiasi kikubwa matatizo ya shinikizo la juu la damu,

INAENDELEA UK.20

AFYA

# Ukatili unavyoweka njia panda hatima afya za watoto wengi

• Wakubwa wao pia wana mazito yao

Na Romana Mallya



Mtoto katika umri wa kwenda shule akishiriki kuomba barabarani katika mazingira magumu na hatarishi. **PICHA: MTANDAO**

UBAKAJI, mimba za utotoni, ulawiti, shambulio na kujeruhiwa ni vitendo vya ukatili ambavyo sasa vinawaweka watoto kwenye mazingira hatarishi.

Hayo yanatokea, huku jukumu la uangalizi watoto hao na malezi, baadhi ya wazazi wamewabebesha zaidi wasaidizi wa ndani.

Asilimia kubwa ya familia nyingi hasa kwenye miji na jiji, inatokana na majukumu ya utafutaji fedha na malezi ya watoto kwa kiasi kikubwa yamehamishiwa kwa wasaidizi wa ndani, bila kujali aliyebebeshwa jukumu hilo ana historia gani ya malezi mahali anakotoka.

Imegundulika, idadi kubwa ya wasaidizi wa ndani huchukuliwa kutoka kwenye familia kwa lengo la kusaidia kazi za ndani na wengi wao wana historia za kupitia maisha ya hila na manyanyaso, kukosa elimu na kuingia kwenye ngono wakiwa na umri mdogo.

Bila kujali machungu waliyonayo, ama kwa kujua au kutojua, wazazi na walezi kutokana na majukumu mengine waliyonayo kwa asilimia kubwa, wanawakabidhi wasaidizi hao majukumu ya uzazi, kukaa muda mrefu na watoto kuliko wazazi wenyewe.

### ASEMAVYO WAZIRI

Takwimu za taarifa ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, zinabainisha kwamba vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto, vimeongezeka kutoka matukio 13,457 vya mwaka 2017 na kufikia 14,417 mwaka jana.

Ummy anataja vitendo vinavyoongoza ni Ubakaji, jumla yake matukio 5,557; vikifuatiwa na mimba 2,692; kulawiti 1,157; shambulio la 965 na majeruhi ina matukio 705.

Hotuba ilitolewa na waziri Oktoba 31 mwaka huu, katika mafunzo ya waandishi wa habari na wahariri kuhusu ajenda ya kitaifa inayozungumzia Wajibu wa Wazazi na Walezi katika Malezi na Matunzo ya Familia (Akiwamafa) 'Familia Bora, Taifa Imara'.

Akisoma hotuba hiyo kwa niaba yake, Mkurugenzi Idara Maendeleo ya Watoto, Mwajuma Magwiza, ana alibainisha mikoa inayoongoza ni Tanga, Mbeya, Mwanza, Arusha na Tabora.

Waziri Ummy anasema, kuna ongezeko la mmomonyoko wa maadili katika jamii na familia na hiyo inachangiwa na baadhi ya wazazi kutobeba jukumu lao la malezi.

"Tumekuwa tukishuhudia watoto wakifanyiwa ukatili wa aina mbalimbali huku wanaofanya vitendo hivyo kwa kiasi kikubwa wakiwa ni watu walio karibu na watoto, familia, ndugu, jamaa na marafiki.

"Kwa mujibu wa takwimu za Jeshi la Polisi za mwaka 2018, vitendo vya ukatili kwa watoto vinaongezeka kutoka matukio 13,457 mwaka 2017 hadi matukio 14,419 mwaka 2018 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 6.6," anaeleza.

> **Kwa sasa baba ni mtafutaji na mama naye ni mtafutaji. Kwa hiyo kwa ujumla, malezi ya watoto kwa kiwango kikubwa wanaobeba ni wasaidizi wa ndani, ambao nao wana changamoto zao walikotolewa.**

Waziri anavitaja vitendo hivyo vya ukatili kuwa ni pamoja na ulawiti na ubakaji, mimba, ndoa za utotoni, vipigo na ukeketaji.

Anasema, utafiti uliofanywa na wizara kwa kushirikiana na wadau kwa kipindi cha mwezi Desemba 2017 hadi Januari 2018, katika Halmashauri 12: Ilala, Kinondoni, Temeke, Kigamboni, Ubungo, Arusha, Iringa, Mbeya jiji na wilaya, Dodoma, Nyamagana na Ilemela, kulibainika watoto 6,393 wanaoishi na kufanya kazi mitaani.

"Kati yao wasichana ni 1,528 na wavulana ni 4,865. Ilibainika watoto 1,385 kati ya hao waligundulika kufanya kazi za usiku mitaani, wasichana ni 410 na wavulana ni 975.

"Uwepo wa watoto hawa maeneo ya mitaani kwa kiasi kikubwa unatokana na kutowajibika kwa familia katika kumudu majukumu yao ya kutunza na kulea watoto."

Pia, anasema taarifa ya utafiti wa afya ya mama na mtoto na viashiria vya malaria ya mwaka 2015/16, inaonyesha asilimia 25 ya kaya za mjini na asilimia 27 ya zile zilizopo vijijini zina watoto ambao hawaishi na wazazi wao japo mzazi mmoja au wote wapo hai.

Ummy anasema takwimu za wizara zinaonyesha migogoro katika ndoa imeongezeka kutoka 13,382 mwaka 2018 hadi 16,832 kufikia mwezi Juni iliyopota, ikiwa ni ongezeko la asilimia 26.

Magwiza anasema, kitendo cha wazazi kutumia muda mwingi kutafuta fedha, kimeathiri familia nyingi hasa kwenye malezi ya watoto.

"Kwa sasa baba ni mtafutaji na mama naye ni mtafutaji. Kwa hiyo kwa ujumla, malezi ya watoto kwa kiwango kikubwa wanaobeba ni wasaidizi wa ndani, ambao nao wana changamoto zao walikotolewa," anaeleza.

Magwiza anakumbusha wazazi na walezi kuwa pamoja na kufuta pesa za malezi ya watoto, bado wana jukumu la malezi yao na msingi wa maendeleo ya kiuchumi na ustawi, viko katika mikono ya wazazi na walezi na siyo kwingineko.

"Mfano tukiangalia familia nyingi ambazo ni maskini, zinawapa watoto wao mazingira yenye upendo na malezi mema licha ya hali duni ya maisha waliyonayo.

### KAYA TAJIRI

"Tukirudi kwenye kaya zilizo tajiri zaidi, watoto wanaweza kupata huduma bora zaidi za afya na shule na mahitaji mengine muhimu na mara nyingi wazazi wana shughuli nyingi mno, kiasi cha kukosa nafasi ya kuwa karibu na watoto wao," anasema.

Kwa mujibu wa Magwiza, wizara hiyo inayohusika na afya, kwa kushirikiana na wadau wengine wa kimataifa, wamelenga kuifikisha ajenda hiyo kwa makundi mbalimbali katika jamii, ili kukumbusha wajibu wa kila mmoja kuwa na familia bora na taifa imara.

Magwiza anaeleza, hisia za watoto zinapobaini hawapendwi au kutelekezwa, zinaweza kuwa na madhara sawa na kutopata lishe sahihi.

"Ili kujenga familia imara, baba na mama hawana budi kushirikiana katika vipengele vyote vya malezi bora yaani matunzo, kinga na mawasiliano.

"Baba wa Kitanzania wanapaswa kuwasaidia wenzi wao katika kipindi chote kuanzia ujauzito hadi kujifungua. Baba na mama wanaojenga uhusiano wa karibu wa kusaidiana pamoja na watoto wao katika maisha yao, yote watasaidiana katika maendeleo ya kimwili, kijamii na kihisia," anabainisha.

Anasema kupitia tabia na maelekezo yao, wazazi wawili wanawasaidia watoto kujifunza haki na wajibu wao, ili waweze kuwa raia wenye uwezo, dhamira na mchango bora kwa mahitaji ya taifa.

### MAKUNDI WASHAWISHI

Magwiza anataja makundi mengine kwenye jamii, yanayoweza kuhamaisha ajenda ya kuwa na 'Familia Bora, Taifa Imara' ni wabunge wenye ushawishi majimboni, wanaoweza kutumia nafasi zao kutunga sera na kupitisha bajeti zitakazowanufaisha wazazi na walezi.

INAENDELEA UK.20

AFYA

# Mabingwa walia hatari kiharusi kwa wazee, vijana hadi vichanga

**INATOKA UK.18**


kisukari, magonjwa ya moyo (valvu za moyo), selimundu na moyo kutanuka inachangia kwa kiasi kikubwa mtu kupata kiharusi.

"Baadhi ya wanawake wakati wa ujauzito hupata kiharusi, ugonjwa huu unatibika kama mgonjwa atafika hospitali kwa wakati," anasema.

Daktari bingwa wa magonjwa ya ubongo, mishipa ya fahamu na uti wa mgongo upande wa upasuaji, Mugisha Clement, kutoka Hospitali ya Aga Khan, jijini Dar es Salaam, anasema vijana wapo hatarini kupata kiharusi kwa sababu wanakiuka mengi katika maisha yao.

Wengi wanaelezwa kuvuta sigara, wamepitiliza unywaji pombe, ulaji uliopitiliza au mpangilio, wana uzito mkubwa na wanatumia dawa zinazohatarisha maisha yao ya kila siku.

"Vyote vinasababisha mtu kupata shinikizo la damu, ukiwa na shinikizo la damu katika umri mdogo unauwezekano wa kupata kiharusi," anasema.



Mgonjwa wa kiharusi akitibiwa. **PICHA: MAKTABA**

Distributed via ippmedia

### MAZOEZI DAWA & SIGARA SUMU

Dk. Clement anaeleza takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaonyesha kati ya watu wanne, mmoja atapata kiharusi, anaitaja kaulimbiu ya mwaka huu 'Angalia usiwe ni wewe' na akiwasisitiza Watanzania kuhakikisha wanafanya mazoezi, kwa sababu inasaidia kupunguza mafuta mwilini.

Dk. Clement anakumbusha sema mazoezi ni dawa na anawashauri watu kwa kila wiki angalau wayafanye mazoezi mara kadhaa; mara mbili au tatu.

Anavitaja viashiria vya kupata kiharusi ni mtu kuwa na uzito mkubwa kuliko kiwango anachostahili na anawataka watu wapunguze wanga mwilini na waongeze matumizi ya mboga za majani.

"Vijana wengi wana vitambi na hii ni moja ya hatari ya kupata kiharusi, kwa sababu mwili unakuwa na mafuta mengi kwenye damu ambayo hujiweka kwenye kuta za mishipa ya damu, baadaye huziba na kupasuka," anasema.

> **Alinieleza kuna uwezekano baadhi ya viungo vya mtoto (kupitia ultrasounds) havitakuwapo.**

Kwa wanaotumia sigara, anawakumbusha kwamba inasababisha uharibifu kwenye kuta za mishipa ya damu na kuifanya ikakamae.

Naye Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mishipa ya Ubongo kutoka hospitali hiyo, Philip Adebayo, anasema zipo aina mbili za kiharusi ambazo ni mishipa kuziba damu kushindwa kupita kama kawaida na ya pili, mishipa ya kupitisha damu inapasuka.

"Kila mtu yupo hatarini kupata kiharusi. Tuitunze miili yetu, tufanye mazoezi kwa sababu matukio ya ugonjwa wa kiharusi yanaongezeka hasa nchi zinazoendelea," anasema.

PICHA YA KIHARUSI

Dalili zake:

- Kuchanganyikiwa, shida ya kuongea na kuelewa mtu anachoambiwa.
- Maumivu ya kichwa yanakwenda pamoja na kupoteza fahamu kwa vipindi na kutapika.
- Ganzi katika viungo vya uso, mkono na mguu na hasa vikiwa vya upande mmoja wa mwili.
- Kupata shida ya kuona jicho moja au yote.
- Kupata shida ya kutembea vikichanganyika na kizunguzungu na kukosa mpangilio wa matendo ya mwili

Madhara yanajumuisha:

- Msongo wa mawazo.
- Maumivu kwenye mikono na miguu yanayoongozeka baada ya viungo hivyo kufanya kazi au kutokea mabadiliko ya hali ya hewa.
- Kupooza au udhaifu upande mmoja wa mwili.
- Kupata shida katika kufanya matendo ya kuonyesha hisia za mwili.
- Kushindwa kumudu matumizi ya kibofu cha mkojo au viungo vya njia ya haja kubwa.

Tiba zake

Kuna aina kuu mbili za kiharusi; Ischemic na Hemorrhagic. Kila moja ina chanzo kilicho tofauti, kila moja inahitaji tiba iliyo tafauti na ya aina nyingine. Ni sharti kujua aina gani ya kiharusi kwani tiba ya aina moja inaweza kuwa na madhara kwa kiharusi kingine.

Kiharusi Ischemic; hutokea mishipa ya damu inapoziba au kupungua kipenyo, hivyo tiba ya tatizo hilo ni kuhakikisha damu ya kutosha inaufikia ubongo. Tiba huanza kwa kutoa dawa za kuyeyusha damu au mafuta yaliyoganda na kuzuia hali hiyo isitokee tena. Jamii ya aspirin yatajwa inaweza kutumika au sindano ya mishipa iitwayo 'Plasminogen Activator' (TPA). Tiba Hemorrhagic: Huanza damu inapovuja ndani ya ubongo, hivyo tiba yake italenga kuzuia damu isiendelee kuvuja na kupunguza mgandamizo wa damu, iliyovuja juu ya ubongo.

Tiba huanza kwa kutoa dawa za kupunguza mgandamizo kwenye ubongo, kupunguza msukumo wa damu kwa ujumla na kuzuia kusinyaa ghafla mishipa ya damu. Upasuaji unaweza kutumika kurekebisha mishipa ya damu iliyopasuka .

Namna ya kujilinda:

- Kutotumia dawa haramu
- Kula chakula chenye mboga na matunda kwa wingi na chenye cholesterol kidogo
- Kufanya mazoezi kila wakati
- Kuhakikisha unadhibiti blood pressure
- Kuhakikisha unadhibiti kiwango cha sukari mwilini
- Kuwa na uzito unaofaa
- Kunywa pombe kwa kadri au kuacha kabisa

## Ukatili unavyoweka njia panda hatima afya za watoto

**INATOKA UK.19**

Pia anataja lingine ni viongozi wa dini, ambao jamii inawaheshimu na wana ushawishi wa kuhamasisha malezi bora ya watoto kwenye jamii.

Anasema vyombo vya habari aina zote, navyo vina mchango katika utoaji elimu, kubadilisha jamii kutoka kwenye hali ya sasa na kutengeneza jamii yenye vijana wajao wenye malezi bora.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa wizara inayohusika na afya, Mkurugenzi Msaidizi wa Malezi na Elimu ya Familia, Tausi Mwilima, anasema wamejipanga kuhakikisha elimu inawafikia wadau wote wakiwamo waandishi wa habari, ambao wanapewa mafunzo.

"Wizara imeandaa ajenda hii ya kitaifa ambayo inaweka msisitizo katika maeneo makuu ambayo ni mafunzo, ulinzi, mawasiliano, kujenga familia na upendo. Maeneo haya yakifanyiwa kazi watoto na vijana watakuwa salama," anasema.

### MWANASAIKOLOJIA & VICHANGA

Mwanasaikolojia Betty Humplick, anasema 'Familia Bora, Taifa Imara' litatokana na wazazi au walezi watakapobeba jukumu la malezi kwa asilimia 100 ya kuhakikisha mtoto analindwa, anatunzwa na wanazungumza naye.

"Kabla ya kubebesha jukumu hili kwa makundi mengine kwenye jamii, lazima wazazi yaani baba na mama walibebe kila mmoja kwa nafasi yake kuhakikisha anashiriki kwenye malezi bora ambayo yatamjenga mtoto kuanzia akiwa tumboni hadi anapozaliwa ili tuwe na taifa imara," anasema.

Betty anasema, mtoto kabla na baada ya kuzaliwa, anahitaji mapenzi ya baba na mama kwa pamoja, kuanzia lishe ya mama mjamzito, kuzungumza na mtoto aliyeko tumboni na kucheza.

"Mtoto akiwa tumboni anahitaji upendo wa baba na mama, anahitaji kusemeshwa kwa sababu ana hisia na anasikia, mama na baba wanatakiwa kuanza malezi ya mtoto kumjengea upendo tangu yupo tumboni," anasema.

Mwanasaikolojia huyo anasema mtoto hadi umri wa miezi sita, anahitaji mapenzi ya wazazi, kunyonya maziwa pekee ya mama, kupata muda wa kupumzika, kuimbiwa na kuzungumza naye.

"Baada ya umri huo, anahitaji vyakula vya kumjenga mwili na upendo wa wazazi, mtoto akihisi anapendwa na wazazi anakua kiakili na mwenye furaha kwenye jamii.

"Lakini kama wazazi watakuwa watafutaji tu wa fedha na kuhamisha jukumu hili kwa msaidizi wa ndani, kuna uwezekano mkubwa, akajifunza tabia nyingi ambazo siyo za familia husika," anasema Betty.



# Wanawake waonywa kutumika kisiasa

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WANAWAKE jijini Mbeya, wametakiwa kuepuka kutumiwa na wanasiasa hasa kipindi cha uchaguzi kama madaraja ya kuwavushia na badala yake kuwashawishi wanasiasa kuwainua kiuchumi.

Rai hiyo ilitolewa juzi na mdau wa maendeleo mkoani Mbeya, Ndele Mwaselela, alipokuwa akizungumza na wananchi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya huku akisema mara nyingi wanasiasa wamekuwa wakiwatumia wanawake kujinufaisha. Alisema endapo kundi hilo muhimu kwa taifa litaendelea kukubali kutumiwa na wanasiasa, litazidi kudidimia katika lindi la umaskini na kulalamikia hali ngumu ya maisha huku wanasiasa wakizidi kuchanua.

Mwaselela aliwaonya wanasiasa wanaowatumia wanawake kipindi cha kampeni za kisiasa na kuwaacha baada ya kupata wanachokitaka, kuacha tabia hiyo. Alisema badala ya kufanya hivyo, wawape mbinu za kuwawezesha kiuchumi.

"Mkiendelea kutumika na wanasiasa mtaendelea kuwa maskini wakati wenzenu wanazidi kuwa matajiri kupitia migongo yenu. Nawashauri mwendelee kufanya shughuli zenu kwa maslahi ya familia zenu. Wakitaka waje wawasaidie mitaji," alisema Mwaselela.

Pia aliwataka wanawake kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi kwa kuhakikisha wanawekeza kwenye uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zenye ubora ili kuunga mkono juhudi za serikali za kufikia uchumi wa viwanda.

Sambamba na hilo, aliwataka wanawake kuwa mstari wa mbele kuwekeza hata kama wana umri mkubwa kwa kuwa kundi hilo ndilo lenye jukumu kubwa la kulea watoto.

Ili kuhakikisha wanafanikiwa katika hayo, aliwataka wanawake hao kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha wanazopata ili kuendeleza biashara badala ya kuwa na matumizi makubwa kuliko kile wanachozalisha, hatimaye kusababisha kufilisika. Meya wa Jiji la Mbeya, David Mwashilindi, alisema miongoni mwa vikwazo vinavyowakabili wanawake ni mtaji unaosababisha washindwe kuanzisha biashara zao.

Alisema licha ya kikwazo cha mtaji kwa wanawake, bado mwitikio ni mdogo kujiunga kwenye vikundi ambavyo vitawasaidia kukopesheka na taasisi za kifedha na halmashauri.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya (kulia), akisalimiana na mmiliki wa Kiwanda cha Malumalu cha Malmo E Granito, Imlan Jesa, wakati jopo la mawaziri wanne wakiongozwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi (hayupo pichani), walipotembelea mgodi wa kuchimba chokaa katika Kijiji cha Nanyala, Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, mwishoni mwa wiki, kwa ajili ya kutatua mgogoro uliopo kati ya wananchi na kiwanda. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wakulima karoti walia bei ya pembejeo

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAKULIMA wa karoti katika kata ya Iganjo, Halmashauri ya Jiji la Mbeya wameiomba serikali katika msimu ujao wa kilimo kupunguza bei ya pembejeo za kilimo ili kuongeza uzalishaji.

Ombi hilo walilitoa juzi wakati wa kikao na Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ambaye aliwatembelea wakulima hao kwa lengo la kusikiliza matatizo yao ili kuwasaidia.

Wakulima hao ambao ni zaidi ya 400 walisema wanatamani msimu ujao wa kilimo pembejeo za kilimo kwenye karoti ziwe bei nafuu ili wanufaike na kilimo hicho ambacho walisema kinaendesha maisha yao.

Mmoja wa wakulima hao ambaye anatoka kikundi cha G20, Nicolas Mwampeta, alisema kilimo cha karoti kimeshikilia maisha yao kwa kuwa kinawasaidia kuendesha maisha yao na kupata akiba ya kusomesha na kufanya shughuli zingine za maendeleo.

"Sisi ni vijana ambao tumeamua kujiajiri na kujikita katika zao hili kwa sababu lina faida ukilinganisha na mazao mengine. Tatizo linalotukabili ni gharama kubwa ya pembejeo za kilimo jambo ambalo linakwamisha jitihada za kuongeza uzalishaji," alisema Mwampeta.

Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, alifurahishwa na jitihada wanazofanya vijana hao hasa kuamua kujikita kwenye shughuli za kilimo.

Alisema vijana hao ambao mbali na kulima karoti lakini wanahakikisha wanazitoa shambani na kuziosha mtoni jambo ambalo linawaingiza fedha nyingi kwa sababu huwarahisishia kazi wateja.

Kutokana na hali hiyo, alisema taasisi yake ya Tulia Trust itakisaidia kikundi cha G20 mkopo wa Sh. milioni moja ili kukamilisha jengo lao.

## Ufugaji samaki wapigiwa debe

**Na Grace Mwakalinga,**
RUNGWE

JAMII imeshauriwa kuchangamkia fursa ya ufugaji samaki kama jitihada za kuboresha upatikanaji wa lishe, maendeleo ya viwanda na kujiongezea kipato.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mkurugenzi wa Shamba Samaki, lililoko katika Kata ya Kiwira, Rungwe mkoani Mbeya, Kenny Nyambacha alipozungumza na mwandishi wa habari hii.

Alisema ufugaji wa samaki una faida kubwa kulinganisha na ufugaji wa aina yoyote pamoja na mazao mengine ya biashara.

Nyambacha alisema ametengeneza zaidi ya mabwawa 20 kwa ajili ya uzalishaji wa samaki na kwamba ndoto yake kubwa ni kuzalisha samaki wengi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya ndani na nje ya nchi ili kuliingizia taifa fedha za kigeni.


"Ufugaji wa samaki kwa sasa ni dili kubwa kwani uhitaji ni mkubwa. Mbali na kutumika kama chakula kwa sasa tunaweza kusafirisha kupeleka mataifa mengine kuuza. Nawashauri wananchi wenzangu kuchangamikia fursa hii. Natamani kunufaika zaidi na mipango yangu ni kufungua kiwanda cha kuchakata samaki," alisema.

Nyambacha alisema kwa sasa amezalisha zaidi ya vifaranga 100,000 na kwamba wakazi wanaozunguka eneo hilo walijengewa uwezo wa namna ya ufugaji bora wa samaki.

Aliongeza kuwa shamba la mradi wa samaki limesaidia ajira kwa wanawake na vijana na hilo linatumika kama sehemu ya kukuza shughuli za utalii wa ndani kwa wageni wanaofika kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania.

Mmoja wa wananchi wanaojihusisha na ufugaji wa samaki katika kata ya Kiwira, Lupakisyo Amos alisema kupitia ufugaji amepiga hatua kubwa ya maendeleo kwani ana uhakika wa kupata mboga na fedha za kujikimu kila siku.

Amos aliwashauri wananchi wengine kujiingiza kwenye ufugaji wa samaki wa kisasa ili kujikwamua kiuchumi kwa sababu samaki ni chakula kinachopendwa na watu wengi.



# Ujenzi maghala wasuasua kisa fedha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI Mkazi wa Kampuni ya Feerum Spolka Akcyjna kutoka Poland, Mikolaj Kucia, ameiomba serikali kukamilisha malipo ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa maghala ya chakula utakaosaidia wakulima na serikali kuhifadhi nafaka katika sehemu salama.

Mradi huo unatakelezwa kwa ushirikiano baina ya serikali ya Tanzania na Poland kwa gharama ya dola za kimarekani milioni 33 (bilioni 76) unalenga kuhakikisha uhifadhi wa nafaka nchini unalisaidia taifa kupunguza uharibifu wa mazao.

"Tayari serikali ya Poland imeshatoa fedha na utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 65 lakini shughuli zimesimama hadi serikali ya Tanzania itakapotulipa Dola za Kimarekani milioni 1.8," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kampuni yake ina hofu kuwa ucheleweshaji wa malipo unaweza kuzorotesha kukamilika kwa ujenzi huo na hata kupotea kwa ajira 500 za Watanzania.

Kampuni hiyo ina uzoefu mkubwa kwenye shughuli za huduma za teknolojia ya uhifadhi wa mazao ya kilimo na miongoni mwa mradi mkubwa ilioufanikisha hivi karibuni ni ujenzi wa ghala kubwa nchini Ukrain lenye uwezo wa kuhifadhi tani 800,000 za chakula.

Alisema katika jitihada za kuunga mkono maendeleo ya ekta ya kilimo nchini, a, Feerum ilianza kujenga maghala ya kuhifadhia chakula matano katika maeneo ya Songea, Makambako, Mbozi, Shinyanga na Dodoma mwaka jana. Ujenzi wa maghala hayo ilikuwa sehemu ya mradi wa kujenga maghala manane ya kuhifadhia chakula nchi nzima.

Katika mradi huo, lengo kuu ni kujenga maghala ambayo yatakuwa na uwezo wa kuhifadhi tani 250,000 za mazao ya chakula, hususani mahindi.

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) chini ya Wizara ya Kilimo ndiye msimamizi wa mradi.

Akizungumzia mwenendo mzima wa mradi huo, mkurugenzi huyo alibainisha kuwa teknolojia ya kisasa inayotumiwa na kampuni yake ujenzi wa maghala hayo ina manufaa makubwa ikiwamo kupunguza upotevu wa mazao.

"Sababu kubwa ya upotevu wa mazao ya chakula ni pamoja na uwapo wa maghala machache ya kuhifadhia chakula, matumizi ya teknolojia iliyopitwa wakati ya kuhifadhia chakula kama vile kwenye viroba na karakana na kuendelea kuzorota kwa mbinu za kiufundi za kuyatunza maghala hayo," alisema.

"Katika karakana hakuna mpangilio mzuri, kunaweza kuwapo kwa maji, bakteria na wadudu vitu ambavyo vinaweza kuyafikia mazao, kuleta magonjwa, uchafu na ukungu kuenea kwa haraka kwenye mazao, hivyo kusababisha kutoweza kutumika tena," aliongeza.



Distributed via ippmedia

Wananchi wakiangalia magari mawili madogo yaliyogongano, katika barabara kuu ya Dodoma-Manyara, eneo la Kijiji cha Ndoroboni, Wilaya ya Chemba, mkoani Dodoma juzi. Hakuna vifo wala majeruhi katika ajali hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Wakumbushwa kuchangamkia fursa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

VIJANA na kinamama wamekumbushwa kufanya kazi kwa bidii na kuchangamkia fursa za kiuchumi pindi zinapojitokeza.

Wito huo ulitolewa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, Jailosi Sinene, wakati alipokuwa akizungumza na makundi hayo jana jijini hapa.

Sinene aliwataka kinamama na vijana kuchangamkia fursa za kiuchumi pamoja na kufanya kazi kwa bidii ili kuinua uchumi wao.

"Ndugu zangu nawasihi tufanye kazi kwa bidii na kuchangamkia fursa za kiuchumi zilizokuja hapa makao makuu. Rais wetu John Magufuli ametuletea fursa ya kipekee kutokana na kuhamishia makao makuu hapa na yeye mwenyewe kuhamia hapa. Sasa tushindwe wenyewe," alisema.

Alizitaja fursa za uchumi ambazo wananchi wa Dodoma wanaweza kuzichangamkia ili kujiongezea uchumi kuwa ni ufugaji kuku, ng'ombe wa maziwa, kilimo cha mboga na matunda.

Sinene aliongeza fursa zingine kuwa ni kujiunga na vikundi ili kunufaika na mikopo kutoka taasisi za kifedha na asilimia 10 ya mapato inayotengwa na halmashauri kwa ajili ya makundi hayo.

Pia alisema mikopo hiyo ya halmashauri haina riba, hivyo wachangamkie fursa hiyo kwa sababu ni msaada wa serikali kuyainua makundi hayo kiuchumi.

Kadhalika, Sinene aliyataka makundi hayo kujiunga katika Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa ili kuwasaidia kupata matibabu wakati watakapougua.

Alibanisha kuwa huduma hiyo ni gharama nafuu kwa familia kwa sababu unalipa Sh. 30,000 kwa mwaka na inahudumia watu sita katika familia moja.

"Serikali iliamua kuiboresha bima hii ili kuwasaidia wananchi wengi kwa gharama nafuu msisahau huduma ya bima ya afya ni muhimu kwa sabau hujui ni lini utapata ugonjwa," alisema.

# Waziri ambana mkandarasi mradi umeme

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amesema serikali haitaraji kuongeza muda wa utekelezaji mradi wa kituo cha kupooza umeme cha Zuzu jijini hapa, hivyo kumtaka mkandarasi kufanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha ndani ya muda uliopangwa.

Kalemani pia ametoa miezi sita kwa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) Mkoa wa Dodoma kuhakikisha linawaunganishia wananchi umeme katika maeneo yote ambao walilipia gharama za huduma hiyo.

Alitoa maagizo hayo jana baada ya kutembelea mradi wa kituo cha kupooza umeme cha Zuzu na Kata ya Nala ambako wananchi wake hawajaunganishwa na huduma ya nishati ya umeme.

Waziri alisema serikali haitaongeza muda wa utekelezaji wa mradi huo na kumtaka mkandarasi anayetekeleza mradi huo, kampuni ya KEC International Ltd kuongeza wafanyakazi na kufanya kazi usiku na mchana.

"Nilikuja hapa kuangalia maendeleo ya utekelezaji wa mradi huu, lakini nimeagiza ukamilike ndani ya muda uliopangwa. Mnaweza kuongeza wafanyakazi ili kufanya kazi usiku na mchana kuhakikisha mnakamilisha kwa wakati uliopangwa," alisema Dk. Kalemani.

"Msijisumbue kuwapitishia ombi lao la kutaka waongezewe muda kwani maombi yakitufikia hatutaruhusu kuongeza muda. Wasimamieni wamalize kazi kwa wakati, kama vifaa vinavyosubiriwa vinapatikana hapa nchini vitumike vya hapa nchini ili mradi viwe halisi na imara," aliongeza.

Waziri alisema ni vyema mradi huo ukakamilika kwa wakati ili kuongeza megawati 600 na hatimaye kulifanya Jiji la Dodoma kuwa na umeme wa kutosha wa megawati 648.

"Kituo chetu kinazalisha megawati 48 na matumizi ni megawati 32 na kuwa na ziada ya megawati 15, hivyo tunataka jiji liwe na umeme wa uhakika kwani hatuwezi kutegemea ziada kidogo iliyopo.

Naye Mhandisi wa Umeme wa KEC International Limited, Nagarajan Rajendiran, alisema tayari vifaa vinavyotakiwa vimeshawasili na kukamilisha taratibu za kuvitoa bandarini na vinatarajia kuwasili eneo la mradi ifikapo Desemba 8, mwaka huu.





# Kampuni yajitosa kusaidia wazee

**Na Hawa Abdallah**, ZANZIBAR

KAMPUNI ya kudai madeni sugu Zanzibar (IRA), imesema imejipanga kupita vijijini kuona matatizo yanayowakabili wazee wasiojiweza na yatima ili kutoa msaada unaostahili.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake mjini hapa, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Issa Haji Khamis, alisema mpango huo utaanza na kutekelezwa kupitia kwa masheha ili kuwapeleka katika nyumba ambazo zitakuwa na watu hao.

Khamis alisema katika misaada yao, wanatarajia kutoa vitu mbalimbali vikiwamo fedha, nguo na vyakula.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kuondoa matatizo madogo magogo yanayowakabili wananchi wao wakiwamo wazee, yatima na watu wanaoishi katika mazingira magumu.

Alisema kutokana na kampuni hiyo inafanya kazi kwa kushirikiana na serikali basi hawanabudi kutoa mashirikiano ya pamoja ili kufikia malengo ya serikali yao kwa jamii.

"Sisi IRA si kama tuna pesa au mataraji. Tunafanya hivi kuisaidia serikali yetu. Tunaona baadhi ya watu katika jamii wanakumbwa na changamoto nyingi katika maisha yao ya kila siku. Tulicho nacho hatuna budi kuwasaidia ili na wao angalau waishi kama wanavyoishi watu wengine," alisema.

Aidha, alizitaka kampuni zingine kuwa na msimamo kama walio nao huku akiamini kuwa wanaposaidia jamii watakuwa wameisaidia serikali yao.

Mkurugenzi huyo alisema kampuni hiyo inajishughulisha na kazi mbalimbali na si kushughulikia madeni peke yake, hivyo watahakikisha wanachokipata kinafika kwa jamii.

Kazi ya kupita vijijini kwa ajili ya kuwasaidia wazee na yatima inatarajiwa kuanza katika kuelekea shamra shamra za sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar.



Distributed via ippmedia

Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Mahmoud Thabit Kombo (kulia), akizungumza kabla ya kumkaribisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (hayupo pichani), kuzungumza na wafanyakazi wa Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), mjini Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Shein awapa matumaini watumishi ZBC

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema azma ya serikali ya kuliimarisha Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) pamoja na kuzingatia maslahi mazuri ya wafanyakazi wake bado iko pale pale.

Dk. Shein aliyasema hayo jana alipokutana na uongozi na wafanyakazi wa ZBC katika mkutano uliofanyika katika ukumbi wa shirika hilo Mnazi Mmoja, mjini hapa.

Alisema ZBC ni shirika jipya lililoundwa miaka sita iliyopita, hivyo lazima kutakuwapo na changamoto mbalimbali na kuwataka wafanyakazi kufahamu ulazima wa mambo hayo katika hatua ya mafanikio.

Serikali, alisema imetumia fedha nyingi katika uundaji wa shirika hilo na kulipatia mitambo mipya ili kuondokana na matumizi ya mfumo wa analojia kwenda wa digitali ambao unatumika buniani katika kurusha matangazo.

Aidha, alisema kuna umuhimu kwa shirika hilo kujiendesha katika mambo mbalimbali lakini kutokana na kutofanikiwa kufikia hatua hiyo, bado linategemea ruzuku kutoka serikalini.

Naye Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahamoud Thabiti Kombo, alisema atasimamia kikamilifu kuhakikisha wafanyakazi wanaojitolea kipindi kirefu wanaajiriwa awamu kwa awamu pamoja na wale wenye ulemavu.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa ZBC, Chande Omar, aliahidi kufanya juhudi kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazolikabili shirika hilo, ikiwamo suala la ajira, mafunzo kwa wafanyakazi na usafiri kwa ajili ya vifaa na wafanyakazi wanapokwenda kutimiza majukumu yao.

# Kifo mtoto aliyebakwa chamzindua Waziri

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kazi, Uwezeshaji, Wanawake, Wazee na Watoto, Moudline Castico, ametaka wanaume kujenga imani na mapenzi ya kuwalea watoto badala ya jukumu hilo kuwaachia kinamama pekee.

Castico alitoa wito huo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari wakati wa ziara aliyoifanya katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja kutokana na tuhuma za tukio la kubakwa kwa mtoto wa 10 na kusababisha kufariki dunia.

Alisema baadhi ya wanaume wamekuwa hawashiriki malezi ya pamoja na badala yake wamekuwa wakiwaachia mzigo mkubwa kinamama jambo ambalo linaondosha mapenzi ya mtoto dhidi ya baba.

Licha ya baadhi ya wanaume kuonekana kuwa kiungo cha familia, alisema hivi sasa kuna baadhi ya wanaume wamekuwa wakiwafanyia udhalilishaji watoto wao wenyewe wa kuwazaa jambo ambalo halikubaliki katika jamii na katika mustakabili mzima wa maisha.

Alisema wanaume wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika malezi ya watoto wao badala ya shughuli zote za uangalizi wa mtoto kuwaachia kinamama.

Kutokana na tabia hiyo kumeibuka matukio ya udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya kinamama na watoto.

"Malezi ya pamoja yanatakiwa yawapo kati ya baba na mama na juhudi zinatakiwa za pamoja katika kutokomeza vitendo hivi vya udhalilishaji vinavyowakumba watoto wetu katika maeneo tunayoishi. Hii ni hatari kubwa jamii kwa pamoja tushikamane na jambo hili lituume kiundani kabisa basi tutafanikiwa," alisema.

Naibu Waziri Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Shadiya Muhamed Suleiman, alisema ni vyema kwa wazazi na walezi kujitahidi katika kuwalea watoto wao kwa lengo la kuwaepusha na ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. "Wizara tutaendelea na jitihada zetu ili kuhakikisha kwa pamoja tunafanikiwa katika kupinga na kuondosha vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ambavyo vinatia doa nchi yetu. Jambo hili ni hatari kwa usalama wa watoto wetu," alisema.

Naye msemaji wa Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, Hassan Makame Mcha, alisema kitendo alichofanyiwa mtoto huyo ni ukatili ambao unastahili kukemewa na jamii nzima.

# Sababu wajawazito kupata madhara makubwa wakati wa kujifungua hizi

**Na Anthony Gervas,**
MWANZA

UTUMIAJI wa dawa za kienyeji kwa wajawazito, umeelezwa na wataalamu wa afya kuwa ni moja ya tatizo linalochangia kupata madhara makubwa wakati wa kujifungua.

Akizungumza jana na Nipashe jijini hapa, mratibu wa huduma za afya ya uzazi na mtoto Mkoa wa Mwanza, Secilia Mrema, alisema wajawazito wengi wamekuwa wakitumia kwa kificho bila kujali madhara yake.

"Tunapompima mjamzito wakati wa kujifungua tunakuta amechanika mfuko wa kizazi, anatokwa damu nyingi na mtoto amefia tumboni, wakati vipimo vinaonyesha hana magonjwa ya aina yoyote yaliyoweza kusababisha madhara hayo," alisema.

"Lakini tunapomhoji anakiri kutumia dawa za kienyeji ambazo hazina kipimo na kusema wanatumia mizizi na majani ya mmea wa bangi, mgagani na magome ya miti shamba kwa madai zinaongeza uchungu aweze kujifungua haraka," alisema Mrema.

Hivyo alisema baadhi yao wamekuwa wakikamatwa na wataalamu wa afya katika vituo vya afya na hospitali wakiwa na dawa hizo wakitumia kwa kujificha wanapokuwa wamelazwa wodini wakisubiri kujifungua.

Mrema alisema katika Mkoa wa Mwanza tangu Januari mwaka huu hadi sasa, idadi ya kinamama 139 walifariki dunia kutokana na madhara ya dawa hizo wakati wa kujifungua.

Alisema kati yao, kinamama 39 walifariki dunia kwa kutokwa damu nyingi na kumi wamefariki dunia kutokana na kuchanika mfuko wa kizazi.

Mratibu huyo alisema watoto waliokuwa wamefia tumboni wakati wa kujifungua ni zaidi ya 500, huku akiongeza kuwa magonjwa mengine yanayochangia madhara hayo ni ya zinaa, presha, malaria na kisukari.

"Tunapowakamata wodini wakiwa na dawa hizo, na wanakiri hapo hapo tunachukua hatua ya kuwanyang'anya na kuanza kuwaelimisha kufuata taratibu za huduma bora za afya ikiwamo kuhudhuria kliniki kupitia vituo vyetu au hospitali," alifafanua.

Mratibu huyo alieleza zaidi kuwa wanapokamatwa na kuhojiwa walikozipata huwataja bibi, shangazi, wakunga wa asili na waganga wa kienyeji kuwa ndiyo huwapatia.

Hata hivyo, alisema wataalamu wa afya wamekuwa wakitoa elimu kwa kinamama kuachana na matumizi ya dawa za kienyeji kupitia vyombo vya habari, vikao vya halmashauri, misibani, vikao vya kata, vituo vya afya, zahanati, wakunga na waganga wa kienyeji.

Aliwataka kuacha kutumia dawa hizo badala yake kufuata ushauri wa daktari au mtaalamu wa afya kutoka katika vituo vya afya na hospitali.



Meneja wa Huduma kwa Wateja na Uendeshaji wa Benki ya Exim, tawi jipya la Mkwepu, jijini Dar es Salaam, Brian Bennet (kushoto), akimkaribisha mmoja wa wateja aliyefika kwenye tawi hilo, ili kupata huduma jana. Tawi hilo jipya ni mkakati wa benki hiyo kujitanua zaidi baada ya kukamilisha taratibu za umiliki wa iliyokuwa Benki ya UBL Tanzania. **MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi wajijengea shule 9 kupunguza msongamano

**Na Sabato Kasika**

WAKAZI wa Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, kwa kushirikiana na serikali na wadau wengine wa elimu, wanajenga sekondari tisa za kata na vijiji ili kupunguza msongamano wa wanafunzi kwenye shule zilizopo sasa.

Shule ni za Ifulifu, Seka, Busambara, Busamba, Kigera Etuma, Nyasaungu, Nyegina, Busamba, Nyang'oma na Dan Mapigano Memorial, ambayo inatarajiwa kuanza kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka ujao.

Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vicent Anney, alisema, Sekondari ya Dan Mapigano iko Kata ya Bugoji yenye wanafunzi 141 waliofaulu kwenda sekondari mwaka ujao. "Kwa muda mrefu wanafunzi wa kata hiyo wanaofaulu wamekuwa wakisoma katika Sekondari ya Kata ya Nyambono ambayo ndiyo ipo jirani na kwao, lakini kule nako wamefaulu wanafunzi 149 wanaotarajia kuanza kidato cha kwanza mwaka kesho," alisema Dk. Anney. Alisema, kwa hali hiyo bila kuharakisha ujenzi wa Sekondari ya Dan Mapigano, kutakuwa na msongamano mkubwa wanafunzi, katika Sekondari ya Nyambono, hivyo hatua mbalimbali zinachukuliwa kuikamilisha Dan Mapigano ili ianze kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka ujao.

Dk. Anney alisema, katika kuharakisha ujenzi huo, hadi sasa vyumba vipya vitano vya madarasa vimeshakamilika, kuna madawati 200, ofisi mpya mbili za walimu zimekamilika

"Ujenzi wa vyoo matundu 10 ya wanafunzi na mawili ya walimu utakamilika ndani ya wiki moja ijayo, na ujenzi wa maabara tatu za Fizikia, Kemia Baiolojia unaenda kwa kasi kwani msingi umeshajengwa na matofali yanafyatuliwa...ujenzi utakamilika mwezi ujao," alisema.

Alisema, mifuko 290 na nondo 100 vimenunuliwa kwa fedha za Mfuko wa Jimbo, na hatua hiyo imeongeza kasi ya ukamilishaji majengo ya shule hiyo na kwamba hata ujenzi wa nyumba ya walimu utakamilika mwezi ujao.

"Maktaba ya kisasa itajengwa hapo shuleni hapo mwaka ujao, ambapo mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo ameahidi kuendesha harambee ya ujenzi huo na pia ataweka vitabu katika maktaba hiyo," alisema.

Aidha, mkuu huyo wa wilaya aliwataka wadau waliotoa ahadi ya kuchangia ujenzi wa Shule ya Sekondari Dan Mapigano Memorial watimiza ahadi zao ili kusaidia kuharakisha ujenzi wa shule hiyo.

Kwa mujibu wa DC Anney, Musoma Vijijini kuna vijiji 68 na vitongoji 374 na sekondari 18 za kata na pia mbili za binafsi zinazomilikiwa na madhehebu ya dini.

# Taratibu za umiliki wa benki UBL zakamilika

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim Tanzania imesema imekamilisha taratibu za umiliki wa iliyokuwa Benki ya UBL Tanzania.

Hayo yalibainishwa jijini Dar es Salaam na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu, baada ya kufungua rasmi tawi lake jipya katika mtaa wa Mkwepu kufuatia benki hiyo kukamilisha taratibu za umiliki wa iliyokuwa Benki ya UBL Tanzania.

Matundu alisema hatua hiyo inafanya Benki ya Exim Tanzania kuwa ya kwanza miongoni mwa benki za sekta binafsi nchini zilizofanikiwa kuunganisha benki nyingine, hivyo kuifanya kuwa miongoni mwa benki tano kubwa hapa nchini ikiwa na ukwasi wa kiasi cha Sh. trilioni 1.7.

Kwa mujibu wa Matundu, hatua hiyo inakwenda sambamba na msimamo wa Rais John Magufuli ambaye amekuwa akisisitiza juu ya umuhimu wa kuwa na benki kubwa zaidi na ndogo nchini kwa kuwa ni hatua muhimu kwa afya ya kifedha katika ukuaji wa uchumi hususani katika kutoa huduma kamili na zenye ubunifu kwa wateja.

"Tanzania ina benki nyingi ukilinganisha na mataifa mengine ikiwamo Afrika Kusini na Nigeria. Sekta ya benki imekuwa ikishuhudia uunganishwaji wa benki ambao mwisho wa siku utaziacha benki zikiwa na uwezo wa kusukuma ukuaji wa uchumi kikamilifu, " alisema.

"Dar es Salaam ni soko muhimu kwa Benki ya Exim na hivyo uwepo wa tawi jipya la Mkwepu ambalo lenye teknolojia, ubunifu na muundo ambao utawawezesha wateja kukutana na maofisa wa benki kwa njia ambayo inawafaa na katika mazingira ambayo ni yanafikika kwa wote," aliongeza.

Aidha, Matundu alisema mchanganyiko wa benki binafsi na zile za umma zilizosambaa kote nchini utahakikisha kuwa kuna mtiririko mzuri wa huduma za kifedha.

Ujio wa tawi hilo jipya unaifanya benki ya Exim Tanzania kuwa na jumla ya matawi 33 kote nchini.

## HABARI KIMATAIFA

# Udukuzi WhatsApp waleta hofu

**NEW DELHI,** India

BAADA ya mtandao wa kijamii wa WhatsApp kuthibitisha kuwa programu yake ilitumika kudukua simu za wateja, kumekuwa na hofu miongoni mwa watumiaji kadhaa ikiwamo India.

Mtandao wa WhatsApp umethibitisha kuwa baadhi ya watumiaji wake walengwa na wadukuzi.

Baadhi ya watu wameelekeza lawama zao kwa serikali na kudai kuwa inahusika na udukuzi huo, ikizingatiwa kuwa kundi la NSO linalodaiwa kuunda programu hiyo ya udukuzi, limeripotiwa kuuzia nchi pekee.

WhatsApp imeishtaki kampuni hiyo kufuatia madai hayo, jambo ambalo limepingwa vikali na Serikali ya India pamoja na kupinga madai hayo.

Baadhi ya watu wamekuwa wakitafuta App tofauti na WhatsApp, ikiwa ni pamoja na Signal au Telegram, wakiamini kuwa ziko salama.

**Simu yako ikidukuliwa kila kitu kilichopo ndani kinaweza kufikiwa au hata vitu vinavyokufikia kupitia kamera au kipaza sauti viko hatarini.**

Lakini, wataalamu wanasema kuwa WhatsApp, ni app inayotumiwa na watu karibu bilioni 1.5 katika nchi 180 na milioni 400 nchini India, ambayo imelengwa na wadukuzi japo kampuni hiyo inasema kuwa sio kosa lake.

Wakati hatari katika programu ya kupiga simu ya WhatsApp iliruhusu kupitisha bila kuingilia kati kwa watumiaji, mwishowe ilichukua simu kwa sababu ya mapungufu kwenye mifumo ya uendeshaji wa simu.

"Wadukuzi walilenga udhaifu uliopo katika mfumo wa operesheni, iwe ni ya Android au Apple," Vinay Kesari, Wakili wa Teknolojia aliyejikita katika masuala ya faragha ya mawasiliano ya simu alisema.

"Simu yako ikidukuliwa kila kitu kilichopo ndani kinaweza kufikiwa au hata vitu vinavyokufikia kupitia kamera au kipaza sauti viko hatarini," Prasanto Roy mwandishi wa masuala ya teknolojia alisema.

WhatsApp imekuwa ikijinadi kama mtandao "salama" wa mawasiliano kwa sababu ujumbe wake ni wasiri na kwamba hakuna mtu anaweza kuufikia isipokua wale wanaowasiliana.

Hii inamaanisha ni yule aliyetuma ujumbe na anayepokea pekee ndiyo wanaweza kuusoma.

"Lakini hali ilivyo sasa, haijalishi kama ujumbe ni wa siri, baada ya simu yako kushambuliwa na wadukuzi wanaweza kufikia kila kitu kwa sababu ujumbe uko wazi unaweza kusomwa," Kesari alisema na kuongeza:

"Huenda pengine umeifungua simu yako," aliongeza. "Lakini cha msingi ni kuwa shambulio kama hilo linafichua jinsi mifumo ya uendeshaji ulivyo hatarini."

Pia alisema: "Linapokuja suala la ishara, kuna safu ya uwazi iliyoongezwa kwa sababu wanatoa nambari yao kwa umma kwa hivyo ikiwa wewe ni mtaalamu wa masuala ya teknolojia unaweza kufikia mifumo ya mawasiliano japo kampuni inasema imeshughulikia suala hilo."

"Hii haimaanishi app hiyo inaiona safu iliyoongezwa ya kinga dhidi ya shambulio kama hilo."

Roy aliambia BBC kuwa shambulio hilo liliendа zaidi ya app hiyo.

"Kwa wale ambao simu zao zimeathiriwa, ujumbe wao uko hatarini, siyo kwa WhatsApp pekee," Roy alisema.

Kufikia sasa hakuna sababu ya kuamini kuwa WhatsApp "Sio salama" ikilinganishwa na app, nyingine. **BBC**

## Marekani kusuluhisha mgogoro wa Mto Nile

**WASHINGTON,** Marekani

MAWAZIRI wa mambo ya nje kutoka Misri, Ethiopia na Sudan, wako Marekani kwa ajili ya mazungumzo kuhusu ujenzi wa bwawa kubwa la maji kando ya Mto Nile.

Bwawa hilo linalojengwa kaskazini mwa Ethiopia, litakuwa kituo kikubwa cha kuzalisha umeme barani Afrika.

Wakati, Misri ambayo inategemea maji ya mto Nile kwa asilimia 80, nchi hiyo ina hofu kuwa bwawa hilo litaathiri mfumo wa usambazaji maji ambao nao una changamoto kadhaa.

Mazungumzo haya yatasimamiwa na Marekani kama msuluhishi baada ya msimamo uliotolewa na Misri na Ethiopia kwenye mazungumzo yaliyopita ambayo hayakuzaa matunda.

Ethiopia inataka kutekeleza mpango huo kwa kipindi cha miaka sita, Misri ikipendekeza muda wa miaka kumi ikihofu mradi huo utafanya Ethiopia kudhibiti maji ya mto Nile.

Mara baada ya kukamilika kwa bwawa hilo litakalogharimu paundi bilioni tatu, litakuwa na uwezo wa uzalisha megawati 6,000.

Ujenzi huo umeathiriwa na ucheleweshaji na haijafahamika kama litaanza kufanya kazi baada ya muda wa mwisho uliowekwa na serikali mwaka 2021.

Misri, Ethiopia na Sudan zilitia saini mkataba wa kwanza kuhusu ugavi wa maji katika mto Nile unaopitia mataifa hayo yote matatu.

Mkataba huo unafuatia ujenzi unaoendelea wa bwawa kubwa linalojengwa na Ethiopia katika mto huo. Ujenzi huo ulizua mzozo mkali wa kidiplomasia kati ya Misri na Ethiopia. Viongozi wa mataifa hayo matatu, walikutana jijini Khartoum Sudan kwa sherehe ya kutia saini mkataba huo ambao umetajwa kama hatua ya kwanza katika kutatua mzozo huo. **BBC**



Shimo lenye upana wa sentimita 55 au inchi 22, ambalo washukiwa wa mauaji walilikata na kulitumia kupenya kwa kutambaa katika gereza la kaunti ya Monterey. **PICHA: MTANDAO**

# Watoroka jela kupitia shimo

**CALIFORNIA,** Marekani

POLISI wametoa picha zinazoonesha washukiwa wawili wa mauaji wakivunja kizuizi cha gereza katika jimbo la California na kufanikiwa kutoroka.

Santos Fonseca (21) na Jonathan Salazar (20), walitambaa na kupenya katika shimo la inchi 22 ambalo walilitoboa katika choo cha jela katika mji wa Salinas, Kusini mwa San Francisco.

Ofisi ya Mkuu wa Kaunti ilisema kuwa vijana hao walitumia eneo ambalo walitambua kuwa "Watu hawawezi kuwaona" wakitoroka.

Wawili hao walikuwa wanasubiri mashtaka mawili tofauti dhidi yao walipoamua kutoroka siku ya Jumapili.

"Tumesikitika sana kwamba kuna watu waliokuwa wanashtakiwa kwa mauaji ambao hawapo tena katika gereza letu," alisema Msemaji wa Ofisi ya Mkuu wa Kaunti ya Monterey, Jonathan Thornburg.

Maofisa wanawasaka washukiwa hao, wanaoaminiwa kuwa wana silaha na ni hatari.

Ofisi ya Kaunti imetangaza kutoa zawadi ya pound 5,000 kwa yeyote atakayetoa taarifa kuhusu ni wapi walipo washukiwa hao. Washukiwa hao walichimba shimo katika choo ambapo walinzi wa gereza wasingewaona, maofisa wamesema.

Shimo hilo lilikuwa na upana wa kutosha kwa Fonseca na Salazar, wote wakiwa na urefu wa mwili wa futi tano na inchi saba (1.7m) kuweza kupanda na kupenya.

Eneo walilochimba lilikuwa na shughuli za ukarabati zilizofanya kujaa mabomba na nyaya.

Washukiwa walitambaa kupitia eneo hili ambalo linasemekana lilikuwa na upanda wa inchi 11 hadi walipofika kwenye mlango wa chuma, ambao waliusukuma hadi ukafunguka na kutoroka.

"Mlango wa chuma ulikuwa nyuma ya gereza, ambako hakuna uzio wa usalama uliozungushwa kwa waya," walisema maofisa.

Pia walisema washtakiwa hao wawili walikamatwa na kushtakiwa mwaka jana kuhusiana na kesi mbili tofauti za mauaji.

Fonseca anashutumiwa kumuua Lorenzo Acosta (37) na Ernesto Cruz (27) siku nne tofauti za mwezi Juni, mwaka 2018.

Naye, Salazar anashutumiwa kwa kumpiga risasi Jaime Martinez (20) mwezi Oktoba mwaka 2017.

Kwa mujibu wa gazeti la Los Angeles Times, washtakiwa wote wawili walikana mashtaka dhidi yao. **BBC**

## Waunga mkono mkataba wa Paris

**BEIJING,** China

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron na Rais wa China, Xi Jinping wametoa taarifa ya pamoja kusisitiza kuunga mkono Makubaliano ya Paris kuhusu mabadiliko ya tabia nchi ambayo Marekani imetangaza kujiondoa rasmi wiki hii.

Marekani imetangaza kuanza rasmi mchakato wa kujiondoa kwenye makubaliano hayo ya Paris.

Nchi hizo mbili zimesema muafaka huo wa mazingira ni mchakato usioweza kubatilishwa na wanasayansi wanaonya kuwa mabadiliko ya tabia nchi yanaweza hivi karibuni kufikia katika kiwango ambacho hakiwezi kubadilishwa tena.

Kwa mujibu wa ripoti mpya ya Universal Ecological Fund (UEF) ambao ni mfuko wa kuhifadhi mfumo wa ikolojia, karibu asilimia 75 ya ahadi katika makubaliano ya Paris yameamuliwa bila kutosha katika kupunguza kasi ya mabadiliko ya tabia nchi. **DW**

# Jafo azisisitiza kamati za rufani kutenda haki uchaguzi S/mitaa

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais-Tamisemi, Selemani Jafo, amerudia tena kuzitaka kamati za rufani nchini kushughulikia malalamiko yote ya wagombea bila kujali chama chochote, badala yake haki itendeke kwa kila mtu.

Jafo alitoa maelekezo hayo jana mjini Babati wakati akizungumza na kamati za rufani za mkoa wa Manyara ukiwa ni mwendelezo wa maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 24.

"Kamati za rufani nchi nzima hakikisheni mnatenda haki kwa wagombea wote wenye malalamiko maana nyie tunawategemea sana ili uchaguzi huu uende vizuri kwa kila mtu," alisema Jafo.

Aidha, alizitaka kamati hizo kutokumwonea mtu yeyote badala yake watende haki kwa kuwa vilio vyote vya kukata rufani vinatakiwa kufikishwa kwao na kuvitolea uamuzi.

"Kamati za rufani ninyi mmepewa nafasi ya kurudisha wagombea walioenguliwa baada ya kusikiliza malalamiko yao na kuyatolea maamuzi bila kuangalia mtu yeyote au kushindikizwa na mtu yeyote ili demokrasia iweze kutamalaki uchaguzi huu," alisisitiza.

Waziri huyo aliwataka kutenda haki kwa kufuata sheria na taratibu zinasemaje ili wagombea wapate haki zao.

Vile vile alisema wagombea waliochukua fomu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) nchi nzima ni asilimia 99, Chadema asilimia 68 huku vyama vingine vya upinzani akisema vimechukua fomu kwa zaidi ya asilimia 50.

Jafo alisema yeye hamna lalamiko analolidharau linalotolewa badala yake anawapatia jukumu timu za kushughulikia malalamiko nchi nzima ili kuyafanyia kazi kwa wakati na haki kutendeka.

Aliyataja maeneo yaliyokuwa na changamoto ni Mbozi, Liwale, Arusha na Kilimanjaro.

Hata hivyo, alisema ni changamoto za kawaida ambazo hazitaharibu demokrasia ya nchini.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, akisoma taarifa kwa waziri huyo, alisema mkoa wake umejipanga vizuri kufanya uchaguzi huo, huku akisema watu waliojiandikisha ni zaidi ya 500,000 sawa na asilimia 79 ya watu waliolengwa.

Mnyeti alisema jumla ya Sh. milioni 187 wameshazipokea kwa ajili ya kuendesha zoezi la uchaguzi huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Fortunatus Fwema, alisema maandalizi ni mazuri.




Meneja wa NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango (wa sita kulia), akikabidhi msaada wa bati 175 kwa Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema, aliyepokea kwa niaba ya Shule ya Msingi Ndelenyuma, katika Halmashauri ya Madaba wilayani humo, mkoani Ruvuma hivi karibuni. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ujenzi wa madarasa wapigwa jeki

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

KAMPUNI ya usambazaji wa mbolea ya Petrobena East Ltd imetoa mifuko 100 ya saruji na mifuko 10 ya mbolea katika Manispaa ya Tabora ikiwa ni kuunga mkono juhudi serikali za ujenzi wa madarasa na utunzaji wa mazingira.

Msaada huo ulikabidhiwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Peter Kumalilwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Komanya Kitwala.

Alisema kuwa kampuni hiyo imefurahishwa na juhudi za serikali za kuboresha elimu nchini zinazoendelea hivyo wameamua kushiriki katika kuhakikisha wanafunzi wanapata mazingira mazuri ya kujifunzia.

Kumalilwa alisema sambamba na utoaji wa saruji hiyo, wameamua kutoa mbolea mifuko 10 kwa ajili ya kukuzia miti ambayo imepandwa katika maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Tabora ili kulinda mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa upande wake, DC Kitwala alisema msaada huo utasaidia kuunga mkono jitihada zao za kuboresha miundombinu ya elimu katika Manispaa ya Tabora kwa kuweka mazingira mazuri ya wanafunzi kupata elimu ikiwamo kuwapunguzia kutembea umbali mrefu kutafuta elimu.

Alisema mifuko 50 itakwenda kata ya Uyui na iliyobaki 50 itapelekwa Kata ya Ifucha ili kusaidia ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Kitwala alisema wako katika kampeni ya kuhakikisha kuwa inaondoa tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa na kujenga hosteli kwa ajili ya wanafunzi ili kuwasaidia kutembea umbali mrefu kutoka kwao hadi shule, jambo linalodhoofisha ufaulu wa wanafunzi.

Aidha, alisema wana mpango wa kujenga sekondari katika Kata ya Ifucha ambayo haina sekondari.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tabora (Uyui), Said Ntahondi, alishukuru kampuni hiyo kwa kutoa msaada huo ambao sehemu ya mifuko hiyo itasaidia kujenga vyumba vya madarasa katika shule shikizi.

Alisema shule shikizi zinasaidia kupunguza tatizo la watoto kutembea umbali mrefu kutafuta haki yao ya kupata elimu.

# Majaliwa awashukuru waliomfariji msiba wa kaka

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewashukuru watu wote waliojitokeza katika mazishi ya kaka yake Mzee Bakari Majaliwa (78), aliyefariki Jumatatu nyumbani kwake katika kijiji cha Chimbila 'B' wilayani Ruangwa, Lindi.

Alitoa shukrani hizo jana wakati wa ibada ya mazishi iliyofanyika kijijini Nandagala wilayani Ruangwa, na kusema hayo ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu na kila mtu atapita kwenye njia hiyo.

"Tulikuwa 12 na sasa tumebaki watano, wanaume wawili na wanawake watatu. Msiba huu kwetu ni mkubwa, umepunguza idadi ya watoto wa Mzee Majaliwa, lakini hatuna namna ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu, wajibu wetu ni kuendelea kumwombea. Nawashukuru wote mlioacha shughuli zenu na kutukimbilia, familia imethamini sana ujio wenu jambo hili limetokea ghafla."

Waziri Mkuu pia alimshukuru Rais John Magufuli kwa salamu za pole alizozitoa. "Jambo hili pia limemgusa Mheshimiwa Rais wetu ambaye ametutaka tuwe watulivu katika kipindi hiki kigumu, na kwamba kila mmoja kwa dhehebu lake aendelee kumwombea marehemu ili Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema."

Alisema alipata taarifa za msiba huo wakati akijiandaa kwenda wilayani Ruangwa kwa ajili ya kushiriki mazishi ya mwanasiasa mkongwe na Mwenyekiti wa zamani wa CCM wa Wilaya ya Ruangwa, Kaspar Selemani Mmuya.

Kwa upande wake, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali, Venance Mabeyo, akitoa salamu za pole kwa niaba ya maofisa na askari wa vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama na kusema anajua uzito wa msiba pamoja na majonzi waliyonayo kwa kuondokewa na mpendwa wao, na kwamba wamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa ndiye anayetoa na anayetwaa. "Hakuna namna ya kurekebisha maamuzi ya Mwenyezi Mungu, tuendelee kumsindikiza kaka yetu kwa sala Mwenyezi Mungu ampokee kwa amani."

Naye, Mwakilishi wa Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Sheikh Othman Kaporo, alisema amewataka wananchi wajiandae na kifo kwa kufanya ibada. "Ni kawaida kwa binadamu kujisahau, lakini Mwenyezi Mungu ametuwekea vitu vya kutukumbusha juu ya uwepo wake ikiwamo kifo, hivyo tuyatekeleze yale yaliyokuwa ya wajibu kuyatekeleza."

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA 2 ENEO MOJA ZINAUZWA** Zipo Ukonga Mombasa. Ya mbele mjengo wa kisasa vyumba 4 nyingine chumba na sebule 4 kiwanja robo eka. Za kupaua. Bei maelewano. Piga simu: 0719 619444 / 0782 574669.

**VIWANJA VITATU VINAUZWA,** NO.1-1341-1890 SQM NO. 2-1342- 1391 SQM NO.3 1343- 1556 SQM BLOCK A KISUKURU-TABATA. SIMU. 0754 857523/0786 857523

## NAFASI ZA KAZI


**Wanahitajika wanaume wenye umri kuanzia miaka 30 hadi 45** kwa nafasi za udereva (Ikiwemo Class C, C1, C2 na C3). Wanahitajika wanawake wenye umri kuanzia miaka 25 hadi 35 kwa nafasi za mauzo (sales za bidhaa). Mshahara wa kuvutia utatolewa. Wahi sasa kupata nafasi nzuri. Kwa mawasiliano zaidi, tafadhali piga simu kwenye namba 0714 634 046. Tafadhali piga simu mda wa kazi tu (kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni).

## 2 ACRE YARD FOR RENT

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku


## KUPOTEA KWA CHETI



**MICHAEL W. KILELE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.2549-0664** kilichotolewa na ALPHA SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/448450/2019.**

115505002

## KUPOTEA KWA CHETI



**KELVIN KAROLI WANJARA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S4706/0038** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shule ya Sekondari FAMGI. Yeyote atakaekion atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MWA/NYA/RB/389037/2019**

115505302

## KUPOTEA KWA CHETI



**GRACE NENELWA PHILIPO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.5090/0008** kilichotolewa na **KAKUBILO SEKONDARI** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHA/RB/429494/2019.**

115504802

**JAMUHURU WA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya Mwanzo Dodoma Mjini
Usimamizi ya Mirathi 76/2019

Ombi la **MTEMI RAMDHAN MANGI**
Kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya
Marehemu **RAMADHAN MANGI**

KWA YEYOTE ANAHUSIKA TANZANIA BARA
Watu wote wanaodai kuwa mahusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 5/12/2019 kabla ya huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakami waweza kukaguliwa.

Tarehe 01/11/2019

115505102

## KUPOTEA KWA KADI

**HAMISI HASSANI SHEMDOE** anatangaza kupotea kwa kadi ya Gari aina ya TOYOTA HINO yenye usajil wa namba T441 ALB iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

**Yeyote atakaeion atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: TAN/RB/442752/2019**

215504902


## KUPOTEA KWA VYETI



**CHARLES IBRAHIM GULEN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0507/0033** kilichotolewa na **ITENGULE SEKONDARI** mwaka 2016. Result slip ya kidato cha sita index namba **S0150/0889** iliyotolewa na SAME SEKONDARI mwaka 2019. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHA/RB/429477/2019/ DAR/CHA/RB/429484/2019.**

115504702

## KUPOTEA KWA CHETI



**GIDEON FURMENZI BONIFACE anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.3646-0046 kilichotolewa na ST. MARY'S DULUTI SEKONDARI mwaka 2016.**

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Control No. 9910810599463.**

115504502

## KUPOTEA KWA CHETI

Distributed via ippmedia




**RAMADHANI JUMA CHOMOKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1022-0471 kilichotolewa na KAMBANGWA SEKONDARI mwaka 2010.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:

DAR/MSI/RB/445952/2019.

115504002

## KUPOTEA KWA CHETI



**YERIKO PILLA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.1674/0160 kilichotolewa na PHILIP MANGULA SEKONDARI mwaka 2013.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**MZU/RB/125/2019.**

115503702

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**ARUSHA**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 22 LA MWAKA 2019**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**
**HENRY BEATUS TESHA............MAREHEMU**
**NA**
**THADEUS BEATUS TESHA......WAOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia maombi haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 9 mwezi wa 11 mwaka wa 2019.

Imewasilishwa Arusha leo tarehe 09 Mwezi wa kumi mwaka wa 2019.

115503902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

Telegram:UHAMIAJI
Tovuti: www.immigration.go.tz
Barua Pepe: rioarusha@immigration.go.tz
Simu: 027-2545249

Ofisi ya Uhamiaji Mkoa,
S.L.P. 236,
Arusha

Kumb:AR/DN/18599 TAREHE 01/11/2019

**HII NI TAARIFA KUWA:**
**BIBI FIONA NGIAMBAKIHA KOMBE**



Ambaye picha yake imeoneshwa hapo, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi. Yeye ni raia wa Kenya Kazi/shughuli zake ni Mwalimu Anuani ya mwajiri wake ni 14628, ARUSHA Ameishi nchini tangu 2009.

Pia amewahi kuishi mikoa ya Kilimanjaro, Arusha.
Mtu yeyote mwenye sababu za kupinga mwombaji asipewe uraia,atume taarifa yake ya maandishi iliyosainiwa kwa KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI S.L.P,512 ,DAR-ES-SALAAM .

Kny: KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI.

115504302

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**RUTH KARLO SENDWA** anatangaza kupotelewa na Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba S.0360/0570 iliyotolewa na KIBASILA SEKONDARI mwaka 2019.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Control No. 9910810594432.

115503502

## KUPOTEA KWA CHETI



**NANCY ALFRED KIGOLA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0268/0024 kilichotolewa na BETHEL SABS SEKONDARI mwaka 2016.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**MOR/MOR/RB/423771/2019.**

115502802

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0767 223311***

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati ya mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MADRID YAJITOSA TENA KUMWANIA SANCHO




**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imeingia kwenye mbio za kuwania saini ya kinda wa Uingereza, Jadon Sancho ambaye kwa sasa anakipiga pale Borussia Dortmund nchini Ujerumani.

Madrid sasa inaingia kwenye mbio moja za kuwania saini hiyo pamoja na Manchester United na Paris Saint Germain ambazo nazo zimeonyesha nia ya kuwania kumsajili.

Hata hivyo, Dortmund yenyewe imeshaweka wazi kuwa bei ya Sancho mwenye umri wa miaka 19 kuwa ni kiasi cha pauni milioni 100.

Hii ni mara ya pili Madrid kumtaka Sancho kwani iliwahi kumtupia ndoano akiwa Manchester City.

Sancho amejiweka sokoni Ulaya licha ya kuwa na umri mdogo baada ya kucheza kwa kiwango bora akiwa Borussia Dortmund tangu alipojiunga nayo mwaka 2017 akitokea City.

Dortmund imeanza mchakato wa kusaka mrithi wa winga huyo ikiamini hawezi kubaki Ujerumani msimu ujao.

Msimu huu Sancho amecheza mechi nane, amefunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho mara sita katika Ligi Kuu.

Katika mechi za Ligi ya Mabingwa Ulaya amecheza mechi tatu. Mchezaji huyo amecheza mechi 14, amefunga mabao manne na kutoa pasi za mwisho mara saba.

Distributed via

# Son afutiwa kadi nyekundu

**LONDON,** England

BAADA ya klabu ya Tottenham Hotspurs kubainisha kwamba, itakata rufani kupinga kadi nyekundu aliyoonyeshwa mchezaji wao Son Heung-min, sasa imefutwa rasmi.

Kadi ya Son iliibua mjadala kabla ya Spurs kupeleka malalamiko kupinga adhabu hiyo kwa Chama cha Soka England (FA).

Son alipewa kadi nyekundu ambayo ingemlazimu kutumikia adhabu ya kukosa mechi tatu kabla ya FA kuifuta.

Mchezaji huyo alionekana akimkwatua mguuni kiungo Andre Gomes wa Everton katika mchezo wa Ligi Kuu England ambayo ilichezwa Novemba 3.

Gomes alivunjika kifundo cha mguu wa kulia na tayari amefanyiwa upasuaji ambao utamuweka nje ya uwanja kwa muda mrefu.

Son ameruhusiwa kucheza mechi tatu zijazo za mashindano baada ya adhabu hiyo kutenguliwa.

"Heung-min Son atakuwapo katika mechi tatu zijazo za Ligi Kuu ambazo Tottenham Hotspurs itacheza baada ya kuifuta kadi yake nyekundu," alisema msemaji wa FA.

Uamuzi wa kutengua adhabu hiyo umetokana na marudio ya mkanda wa video ambayo haionyeshi moja kwa moja kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Korea Kusini alikuwa na dhamira ya kumuumiza Gomes.

Hata hivyo mguu wa Serge Aurier umeonekana ukimkanyaga mchezaji huyo katika eneo la kifundo cha mguu.

Kocha wa Spurs Mauricio Pochettino amesema Son amepata huduma ya saikolojia na yuko tayari kwa mechi zinazofuata ikiwamo ya mwishoni mwa wiki hii dhidi ya Sheffield United.






# *Xhaka avuliwa rasmi unahodha Arsenal*

**LONDON,** England

HATIMAYE Granit Xhaka amevuliwa unahodha na aliondolewa katika safari ya kuifuata Vitoria Guimares katika mchezo wa Kombe la Ligi ya Europa.

Kocha wa Arsenal, Unai Emery, sasa amempa kitambaa cha unahodha, Pierre-Emerick Aubameyang. Pia Xhaka ameondolewa kabisa katika orodha ya wachezaji watano ambao ni manahodha wa Arsenal.

Xhaka aliibua mzozo na mashabiki katika mchezo wa Ligi Kuu ambao Arsenal ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Crystal Palace. Emery alimwambia Xhaka hatakuwa nahodha kufuatia tukio hilo hatua inayomweka katika mazingira magumu kuhusu mustakabali wake ndani ya Arsenal.

Xhaka aliwatolea maneno yasiyofaa mashabiki wakati akienda kwenye benchi baada ya kuzomewa.

Pamoja na kuonyesha utovu wa nidhamu, Xhaka hakuomba radhi kwa mashabiki hadi Alhamisi iliyopita ambapo alifanya hivyo.

Mchezaji huyo alipigiwa kura ya unahodha na wachezaji wanzake baada ya Emery kutaja majina ya mastaa watano wanaostahili kuvaa kitambaa hicho.

"Nilizungumza naye asubuhi na kumwambia kuanzia sasa haumo katika orodha yangu ya manahodha," alisema Emery akiwaambia waandishi wa habari.

HABARI MICHEZO

# Conte awajia juu mabosi Inter Milan

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte amesema "pengine alijiaminisha sana" wakati kocha huyo wa Inter akiwajia juu mabosi wa klabu hiyo kutokana na mipango ya kikosi chake baada ya juzi Jumanne kufungwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Inter licha ya kuongoza kwa mabao 2-0 katika kipindi cha kwanza, lakini walijikuta wakipokea kichapo cha mabao 3-2 ugenini kwa Borussia Dortmund, na kumfanya Conte abwatuke wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

Mabao kutoka kwa Lautaro Martinez na Matias Vecino yalisawazisha kipindi cha pili wakati, Achraf Hakimi alipofunga mawili na Julian Brandt akafunga la tatu kuipa ushindi Dortmund kwenye mechi ya Kundi F.

Conte hasira zake akazielekeza kwenye Bodi ya Inter baada ya mchezo huo, huku akishutumu mpango wa miamba hao wa Serie A, kushindwa kuwa na mipango mizuri ya kikosi kwa msimu, wakati akifanya mahojiano na Sky Sport Italia.

Na kocha huyo wa zamani wa Chelsea, Conte aliendelea kubwatuka zaidi kwa waandishi wa habari ambapo sasa Inter imeachwa nafasi ya tatu kwenye kundi hilo, ikipitwa pointi tatu na Dortmund kwenye mbio za kuwania kufuzu hatua ya mtoano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Nilikuwa sehemu ya mpango pamoja na viongozi wa timu, mara zote nasema na narudia tena hapa," alisema Conte, ambaye kikosi chake kilimsajili Romelu Lukaku kwa ada iliyoweka rekodi, pamoja na Alexis Sanchez, Stefano Sensi, Nicolo Barella, Diego Godin na Valentino Lazaro tayari kwa ajili ya msimu wa 2019-20.





# LAMPARD: SIWEZI KUELEZEA SARE NA AJAX

**LONDON,** England

FRANK Lampard amebainisha yeye "hawezi kuelezea" sare ya Chelsea ya mabao 4-4 dhidi ya Ajax baada ya timu yake kupigana kutoka nyuma ya mabao matatu dhidi ya wapinzani wao waliokuwa wamebakiwa na wachezaji tisa uwanjani.

Tammy Abraham na Kepa Arrizabalaga walijifunga, huku Jorginho na Quincy Promes wakifunga, wakati Chelsea iliporuhusu kufungwa mabao matatu kipindi cha kwanza kwa mara ya kwanza kwenye mashindano hayo.

Ajax ilijikuta ikiongoza kwa mabao 4-1 ndani ya dakika 10 kipindi cha pili kwenye mchezo huo uliopigwa kwenye dimba la Stamford Bridge na walikuwa mbele kwa 4-2 wakati Cesar Azpilicueta alipofunga.

Chelsea walirudi mchezoni baada ya Jorginho kufunga kwa penalti na Reece James akafunga zikiwa zimesalia dakika 16 mpira kumalizika.

Chelsea sasa wana pointi saba sawa na Ajax na Valencia kwenye Kundi H huku mechi mbili zilikiwa zimesalia na kocha, Lampard alionyesha kuridhishwa na sare hiyo mjini London.

"Siwezi kuelezea mchezo huu," alisema BT Sport." Kwa kila kitu kilichotokea kinaelezea kila kitu kuhusu mchezo wenyewe.

Distributed via ippmedia

# *Valverde apuuzia kelele za mashabiki wa Barca*

**BARCELONA,** Hispania

ERNESTO Valverde hana tatizo na kikosi chake cha Barcelona kupigiwa kelele na mashabiki pale Camp Nou, na kocha huyo amewataka wachezaji kujibu kwa kuonyesha kiwango mchezoni, wakati wakitoka sare ya bila kufungana na Slavia Prague kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, juzi Jumanne.

Barca ilishindwa kupata ushindi baada ya kutoka kufungwa mabao 3-1 na Levante kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania, La Liga, wikendi iliyopita na hivyo kuongeza presha kwa Valverde.

Lionel Messi aligonga mwamba na wachezaji wenzake walijaribu mara kadhaa kumtungua golikipa wa Slavia, Ondrej Kolar, ambaye alionekana kuwa kwenye kiwango bora.

Slavia walionekana kucheza kwa kujituma zaidi na kujilinda kwenye mchezo huo wa Kundi F na kuiacha Barca bado kuwa na kazi ya kuweza kufuzu hatua ya mtoano.

Akizungumza na Movistar, Valverde alisema: "Siku ile tulipoteza dhidi ya Levante na hilo haliwezi kutuondoa kutoka kwenye ukweli kwamba, mechi mbili zilizopita hatukuwa kwenye ubora wetu.

"Tunajua kwamba, kuna presha kubwa kwa timu kutakiwa kujibu kwa kuonyesha kiwango cha juu."

Alipoulizwa kuhusu kupigiwa kelele na mashabiki, aliongeza: "Ni sawa kwa sababu wanataka timu yao ipate matokeo."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



Distributed via ippmedia

# WENGER AFUNGUKA KUITAMANI BAYERN

●●● Mfaransa huyo akiri muda aliopumzika tangu alipoondoka Arsenal ni mwingi...

**LONDON,** England

ARSENE Wenger ameamua kuweka wazi kwamba yuko tayari kupewa jukumu la kuiongoza Bayern Munich, baada ya aliyekuwa kocha wa timu hiyo kutimuliwa.

Mfaransa huyo amekuwa hana kazi tangu mwaka jana alipoondoka Arsenal, lakini kila siku amekuwa akisisitiza kwamba yuko tayari kurejea kwenye kazi hiyo mahali ambapo kuna hadhi ya juu, na pia ameweka wazi kwamba yuko tayari kuanza mazungumzo na mabosi wa klabu hiyo ya Bundesliga.

"Ndio," alijibu kocha huyo wa zamani wa Gunners wakati alipoulizwa kama anaweza kufanya kazi katika klabu hiyo ya Allianz Arena.

"Kufundisha ndio jukumu nililonalo katika sehemu yote ya maisha yangu mpaka sasa. Unaweza kukumbuka mambo ambayo ni mazuri na ambayo si mazuri, pia unaweza kukumbuza historia. Ninafurahia vitu ambavyo siwezi pia kuvikumbuka sana...

"Lakini katika upande mwingine, mechi za soka, kupata ushindi katika mechi mbalimbali, kuandaa timu kwa ajili ya mechi, na pia kuridhishwa na kile unachokihitaji na kushirikiana katika hisia mbalimbali. Hii ndio vitu ambavyo utavikumbuka.

"Kwa hiyo nasema ndiyo, nimekuwa katika majukumu haya tangu nikiwa na umri wa miaka 33 na nimefundisha hadi nimefikisha miaka 69 bila ya kuingiliwa. Na katika ngazi ya juu.

"Nimefanya kazi miaka 36 bila ya kusimama. Hata kama ninaikumbua, kukaa pembeni bila ya kuwa na hofu kwangu ni jambo baya. Watu ambao wananijua mimi vizuri, wanasema nimepumzika sana na ni kweli."

Wenger alidumu Arsenal kwa muda wa miaka 21, na akiwa hapo ameshinda mataji matatu ya Ligi Kuu England na saba ya Kombe la FA.

Bayern inasaka kocha mpya baada ya kumfukuza Niko Kovac kutokana na kupata kichapo cha mabao 5-1 dhidi ya Eintracht Frankfurt.

Kwa sasa iko katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi ya Bundesliga, pointi nne nyuma ya vinara wa ligi hiyo, Borussia Monchengladbach.

Mbali na Wenger, gazeti la Guardian limeandika kuwa Ralf Rangnick (61) ni mmoja wa makocha ambao wako kwenye orodha ya kutua katika klabu hiyo.

Kovac alitua Bayern katika kipindi cha majira ya joto mwaka jana na alishinda mechi mbili za kwanza za ligi ya ndani kwenye msimu wake wa kwanza akiwa hapo Allianz Arena.

## ZISIKUPITE

### HAALAND DAU JUU

KLABU ya Red Bull Salzburg imesema kuwa thamani ya mshambuliaji wake raia wa Norway, Erling Braut Haaland (19), ni pauni milioni 89. Nyota huyo anawania na timu mbalimbali za Ulaya. ***(Tuttosport - in Italian)***

### BARCA, MADRID VITANI

VIGOGO wa Hispania, Barcelona na Real Madrid zimeweka wazi nia yao ya kusaka saini ya mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Norway na Red Bull Salzburg, Erling Braut Haaland. ***(Marca - in Spanish)***

### JUVE YAMFUATA HAALAND

MABINGWA wa Ligi Kuu Italia, Juventus wametuma mawakala wake kwenda kumwangalia mshambuliaji wa Red Bull Salzburg, Erling Braut Haaland wakati klabu yake inacheza dhidi ya Napoli katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi Jumanne. ***(Calciomercato)***

### ARSENAL KUMUUZA XHAKA

MABOSI wa Arsenal wanajipanga kuangalia uwezekano wa kumuuza kiungo wake raia wa Uswiswi, Granit Xhaka, katika dirisha dogo la Januari baada ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 kukosa nafasi ya kuwa nahodha. ***(Mirror)***

### DENNIS ANUKIA EPL

LEICESTER City imeweka wazi kwamba inataka saini ya straika wa Club Bruges na Timu ya Taifa ya Nigeria, Emmanuel Dennis, ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 20. ***(Mirror)***

### MBAPPE AITAMANI MADRID

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amesema kuwa straika wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe, ana ndoto ya kuichezea klabu hiyo ya Bernabeu. ***(AS - in Spanish)***

### VILLA WAIGOMEA UNITED

MABOSI wa Aston Villa wamesema watakataa ofa yoyote itakayotolewa na Manchester United kwa ajili ya kumwania kiungo wake raia wa Scotland, John McGinn, ambaye ana umri wa miaka 25. ***(Birmingham Mail)***

### LIPPI AMTAJA ALLEGRI

KOCHA wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri, anatajwa kuwa anafaa kuiongoza Manchester United, maneno hayo yamesemwa na Marcello Lippi, ambaye aliipa Italia taji la Kombe la Dunia. ***(Mail)***

### STOKE YAMWANIA CLARKE

STOKE City imeanza mchakato wa kumwajiri Kocha wa Timu ya Taifa ya Scotland, Steve Clarke, ambaye aliajiriwa katika timu hiyo Mei mwaka huu. ***(Sun)***

### MOUNT KUONDOKA CHELSEA

KIUNGO wa Chelsea, Mason Mount (20), amemwandikia ujumbe wa maneno mchezaji mwenzake wa zamani, Mitchell van Bergen, kuwa anatarajia kujiunga na Real Madrid au Barcelona. ***(Express)***

### MADRID, RUIZ WATETA

REAL Madrid inaendelea na mazungumzo na kiungo wa Napoli Mhispania Fabian Ruiz, ambaye ana umri wa miaka 23, kwa ajili ya kutaka kumsajili mchezaji huyo katika msimu ujao. ***(ESPN)***

## HABARI MICHEZO

# Zanzibar Queens yataja silaha zake

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka Taifa ya Wanawake ya Zanzibar (Zanzibar Queens), Mohammed Salah, ametangaza kikosi cha wachezaji 20 kitakachoshiriki katika mashindano ya kuwania ubingwa wa Kombe la Chalenji yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Novemba 14 hadi 23 mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Zanzibar Queens imepangwa Kundi A pamoja na wenyeji Timu ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Queens), Burundi na Sudan Kusini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Salah, alisema kuwa wachezaji hao 20 wamepatikana baada ya kufanya mchujo ambao ulikuwa unajumuisha wachezaji 30 ambao walikuwa wakijiandaa na mashindano hayo.

Salah aliwataja nyota hao watakaopeperusha bendera ya Zanzibar kuwa ni Khadija Saleh, Mwajuma Abdallah, Hafidha Juma, Sabahi Hashim, Neema Machano, Siwazuri Mrisho, Iptisam Salum, Warda Khalidi, Riziki Abdallah, Riziki Abubakar, Warda Abdulhakim, Neema Suleiman, Pili Suleiman, Farida Khamis, Hawa Ali, Khajra, Aziza Mwadini, Nasrini Mohammed na Marry Charles.

Kocha huyo alisema kuwa hana wasiwasi na timu walizopangwa nazo katika hatua ya makundi na anawaahidi Wazanzibar kuwa watakwenda Dar es Salaam kushindana na si kushiriki.

"Nina matumaini makubwa ni kuona timu hii inasonga mbele katika michuano hiyo na ndio maana kikosi chetu tumekiandaa vizuri kuhakikisha kinafanya vema, wachezaji wanahamasa kubwa na hamasa ya wachezaji ndio kitu pekee kitakachotufanya tupate matokeo mazuri katika michezo yetu," alisema Salah.

Aliongeza kuwa kikosi chake kitaendelea kujiimarisha na wanawaomba wadau wa soka kuwaunga mkono ili waweze kwenda kutimiza malengo yao ya kutwaa ubingwa wa michuano hiyo kwa mara ya kwanza.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 8 | 7 | 0 | 1 | 16 | 3 | 21 |
| 2. Tanzania Prisons | 10 | 4 | 6 | 0 | 13 | 8 | 18 |
| 3. Kagera Sugar | 9 | 5 | 2 | 2 | 12 | 7 | 17 |
| 4. Lipuli | 9 | 4 | 3 | 2 | 13 | 9 | 15 |
| 5. Ruvu Shooting | 10 | 4 | 3 | 3 | 8 | 8 | 15 |
| 6. Polisi Tanzania | 8 | 4 | 1 | 3 | 9 | 9 | 13 |
| 7. Namungo | 9 | 4 | 1 | 4 | 7 | 7 | 13 |
| 8. Mtibwa Sugar | 10 | 3 | 3 | 4 | 9 | 11 | 12 |
| 9. Coastal Union | 9 | 3 | 2 | 4 | 8 | 8 | 11 |
| 10. Alliance | 9 | 2 | 5 | 2 | 7 | 7 | 11 |
| 11. Mbao | 10 | 2 | 5 | 3 | 8 | 9 | 11 |
| 12. Mwadui | 10 | 2 | 5 | 3 | 7 | 9 | 11 |
| 13. Azam | 6 | 3 | 1 | 2 | 5 | 3 | 10 |
| 14. JKT Tanzania | 8 | 2 | 3 | 3 | 5 | 7 | 9 |
| 15. Kinondoni MC | 7 | 2 | 2 | 3 | 4 | 6 | 8 |
| 16. Biashara United | 9 | 2 | 2 | 5 | 5 | 9 | 8 |
| 17. Mbeya City | 9 | 1 | 5 | 3 | 7 | 15 | 8 |
| 18. Young Africans | 4 | 2 | 1 | 1 | 5 | 4 | 7 |
| 19. Ndanda | 8 | 1 | 4 | 3 | 6 | 8 | 7 |
| 20. Singida United | 10 | 0 | 4 | 6 | 3 | 10 | 4 |

# MKWASA, WACHEZAJI YANGA WATAMBA KUIMALIZA NDANDA

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI kikosi cha Yanga kikitua salama mkoani Mtwara kwa ajili ya kuwakabili wenyeji Ndanda FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho, kocha wa muda, Boniface Mkwasa, amesema kuwa jukumu alilopewa la kuiongoza timu hiyo ni zito.

**Mkwasa ametangazwa kuchukua mikoba ya Mkongomani Mwinyi Zahera, ambaye alitupiwa virago vya kuifundisha Yanga hapo juzi.**

Akizungumza na Nipashe jana, kabla ya kuelekea Mtwara, Mkwasa, alisema kuwa baada ya kupewa jukumu hilo, alipata nafasi ya kuzungumza na wachezaji ili kwa pamoja kupanga mikakati ya kuhakikisha wanafanya vizuri katika mechi za Ligi Kuu msimu huu.

"Nilivyopata taarifa hizo nilikutana na kuzungumza na wachezaji, wamenielewa na tumekubaliana kufanya kazi kwa ushirikiano ili tuweze kuipa mafanikio timu yetu, huku uongozi ukiendelea kuwatafutia kocha wa kudumu,"alisema Mkwasa.

Alisema kuwa jana jioni alitarajiwa kuiongoza timu hiyo katika mazoezi na leo asubuhi wataendelea kujiimarisha kuelekea mchezo huo ambao kwake utakuwa ni wa kwanza.

"Sasa hivi (jana asubuhi), ndio tunajiandaa kuelekea Mtwara, tukifika tu, nitawapa wachezaji mazoezi ya jioni halafu na kesho (leo) asubuhi tutafanya tena mazoezi kwa ajili ya kufanya wachezaji kuwa fiti kukabiliana na Ndanda FC, ambayo ni moja ya timu ngumu," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa msimu huu una ushindani mkubwa na kuweka wazi kwamba anawaheshimu wapinzani wao, huku akiwaomba mashabiki wa klabu hiyo kumpatia ushirikiano pamoja na kujitokeza kwa wingi uwanjani kila Yanga inapokuwa inacheza.

Naye Mwenyekiti wa Yanga, Mshindo Msolla, alisema kuwa anamwamini kocha huyo kutokana na uzoefu aliokuwa nao na hawana wasiwasi wowote baada ya kumpa jukumu la kuiongoza timu yao.

"Tunamwamini Mkwasa, ndio maana tukampa kazi ya kuinoa timu yetu huku tukiwa tunaendelea na mchakato wa kumtafuta kocha mkuu ambaye tunatarajia kumtangaza siku chache zijazo, tutakuwa tunawafahamisha kila kinachoendelea," alisema Msolla.

Yanga imeamua kuachana na Zahera ikiwa ni siku chache baada ya kuondolewa katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Pyramids ya Misri kwa jumla ya mabao 5-1.



Wachezaji wa Fountain Gate ya jijini Dodoma wakishangilia baada ya timu yao kupata ushindi dhidi ya The Mighty Elephant ya Songea, katika mchezo wa Ligi Daraja la Pili uliochezwa Jumatatu kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro. Fountain Gate ilishinda mabao 2-1. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Ndayiragije ataja watakaoivaa Guinea*

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije, ametaja kikosi cha wachezaji 27 kikiongozwa na nahodha, Mbwana Samatta kwa ajili ya kuivaa Equatorial Guinea, katika mchezo utakaochezwa Novemba 15, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Samatta amerejea katika kikosi hicho, baada ya kukosa mchezo wa kirafiki dhidi ya Rwanda (Amavubi), kutokana na sababu za kifamilia zilizokuwa zinamkabili kwa wakati huo.

Kocha Mkuu wa Stars, Ndayiragije, aliwataja wachezaji watakaojiandaa na mchezo huo wa kuwania tiketi ya kucheza fainali zijazo za Kombe la Mataifa Afrika kuwa ni pamoja na Juma Kaseja, Metacha Mnata, David Kisu, Salum Kimenya, Hassan Kessy, Mohammed Hussein (Zimbwe Jr), Gadiel Michael, Erasto Nyoni, Bakari Nondo, Kelvin Yondani na Dickson Job.

Wachezaji wengine ni Jonas Mkude, Abdul-Aziz Makame, Simon Msuva, Eliuter Mpepo, Iddi Suleiman (Nado), Salum Aboubakari, Ditram Nchimbi, Shabani Iddi, Mzamiru Yassin, Frank Domayo, Farid Mussa, Miraji Athumani, Hassan Dilunga, Kelvin John na Ayoub Lyanga.

Naye Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema kuwa kikosi hicho kitaingia kambini mapema wiki ijayo kwa ajili ya kujiandaa na mchezo huo wa kwanza wa Kundi L.

Ndimbo alisema kuwa kiingilio cha chini katika mchezo huo kimepangwa kuwa ni Sh. 3,000 wakati cha juu ni Sh. 5,000.

TFF ilimpa mkataba wa mwaka mmoja Ndayiragije, ikiwa ni siku chache baada ya Mrundi huyo kuipa Tanzania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezani wa Ndani (CHAN).

# Michezo

Alhamisi Novemba 7, 2019

Nipashe



Wenger afunguka kuitamani Bayern

UKURASA 30



Mshambuliaji wa KRC Genk, Mtanzania Mbwana Samatta (jezi nyeupe), akiruka juu na kuifungia timu yake bao pekee katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Kundi E iliyochezwa kwenye Uwanja wa Anfield juzi usiku. Liverpool ilishinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# Zahera achomoa betri

## Aanika namna alivyogeuka mfadhili wa Yanga na alivyomkataa Mkwasa kuwa msaidizi...

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI wengi wakiamini kutimuliwa kwa Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, ni kutokana na timu hiyo kutolewa katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi Pyramids, kocha huyo amefunguka kilichopo nyuma ya pazia.

**Juzi uongozi wa Yanga ulitangaza kuvunja mkataba na Mkongomani Zahera pamoja na benchi zima la ufundi kwa kile ilichoeleza ni kutokana na mwenendo mbaya wa timu hiyo dimbani.**

Hata hivyo, jana Zahera alianika kila kitu huku akieleza kuwa tatizo kubwa lilianzia kwa kukataa kuchaguliwa kocha msaidizi mpya, lakini akimtaja mtu mmoja kwa jina moja la Ndama kuwa alishinikiza atimuliwe.

"Uongozi ulinihakikishia hata kama tutafungwa na kutolewa na Pyramids hawatanifukuza, lakini nilishangaa juzi (Jumanne) wakati tupo mazoezini Meneja wa timu Hafidhi (Saleh) ananiambia naitwa klabuni na msaidizi wangu, Noel Mwandila.

"Ukweli tofauti ilianza baada ya kukataa Mkwasa asiwe msaidizi wangu, na nilikataa kwa sababu katika mkataba wangu unaonyesha msaidizi nitachagua mwenyewe."

Zahera alisema sababu nyingine ya timu hiyo kuondolewa katika mashindano ya kimataifa ni kutokana na kuwapo kwa maandalizi ya kiwango cha chini ukilinganisha na ukubwa wa mashindano hayo ya Afrika.

Kocha huyo alisema kuwa wakati wakiwa njiani kuelekea Botswana kuwakabili Township Rollers, baada ya kushuka na ndege jijini Johanesburg, Afrika Kusini, viongozi walikosa fedha za kulipia usafiri wa basi na yeye alilazimika kutoa kiasi cha Dola za Marekani 2,000 ( zaidi ya Sh. milioni nne za Tanzania) ili kupata huduma hiyo.

"Hawakuniomba, ila wachezaji wangu waligomea kupanda basi hilo la timu pinzani, ilinishangaza, namna gani viongozi mnasafiri bila ya kuwa na fedha za dharura, na hapo Mwakalebela (Makamu Mwenyekiti- Frederick), alitangulia kuweka mambo sawa," aliongeza kocha huyo.

Alisema pia na wakati wanarejea tena Johannesburg kutoka Gaborone, wakitumia muda wa saa sita, uongozi ulisema hakuna fedha za kuwanunulia wachezaji chakula cha njiani, huku wakisema wameandaa mlo mmoja tu na baadaye wakitakiwa kusubiri usafiri kurudi nchini.

"Mwanza pia tulifikia hoteli ya maajabu, soko chini, hatuwezi kukaa hoteli hii na tunaenda kucheza mechi ya kimataifa... hoteli yenyewe wakipika chakula, wachezaji sita au saba wanakosa chakula, namshukuru bosi wa GSM, alitusaidia, tukahamia hoteli nyingine, nasema hivi ili watu wajue na wasiangalie matokeo tu," alisema Zahera.

Kocha huyo alisema pia baada ya kumaliza mechi dhidi ya Pyramids jijini Mwanza, kikosi chao kilizuiwa kuondoka hotelini mpaka watakapotakiwa kulipa deni la Sh. 545,000 na kwa mara nyingine Mwakalebela, alimweleza awasaidie kulipa na wakifika Dar es Salaam, watamrejeshea.

"Lazima wanirejeshee, kila fedha niliyokuwa natoa, tuliandikishiana na walikuwa wakirejeshe," Zahera alisema.

Hata hivyo, kocha huyo alisema kuwa Yanga haikupaswa kumtimua kwa kuangalia matokeo ya mechi dhidi ya Pyramids ya michezo minne ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo timu hiyo imecheza, ikiwa wameshinda mechi mbili, sare moja na wamepoteza mchezo mmoja.

Zahera ameitaka Yanga kubadili mfumo wa uendeshaji wa klabu yao na jambo hilo litasaidia kuwarejesha kwenye soka la ushindani kama walivyo TP Mazembe ya DRC au watani zao Simba.

# Simba SC hesabu kali kwa Prisons

**Na Somoe Ng'itu**

HUKU ikiendelea kukosa huduma ya nahodha wake, John Bocco, Simba inatarajia kuwakaribisha Tanzania Prisons kutoka Mbeya katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, watashuka uwanjani kuwakabili "Maafande" hao wakiwa na kumbukumbu ya ushindi mnono wa mabao 4-0 dhidi ya Mbeya City, lakini ikifahamu kuwa Prisons, haijapoteza mechi hata moja msimu huu.

Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, alisema timu yake imejiandaa kukutana na mchezo mgumu na hiyo inatokana na kikosi cha Prisons kuwa na wachezaji wenye uzoefu na wanaofuata maelekezo zaidi.

"Kikosi cha Prisons kinaundwa na wachezaji wenye ubora, tunafahamu mechi haitakuwa rahisi, ni moja ya timu bora kwenye ligi na pia mpaka sasa haijafungwa," alisema Mbelgiji huyo.

Aliongeza kuwa bado wataendelea kukosa huduma ya Bocco, lakini akiwapa habari njema mashabiki wa Simba kwamba, kiungo, Jonas Mkude amerejea kikosini huku afya ya Miraji Athumani na Mohammed Hussein (Zimbwe Jr), ikiendelea kufanyiwa kazi.

Naye Kocha wa Prisons, Adolph Rishard, alisema kuwa amewaandaa wachezaji wake kucheza kwa utulivu katika mchezo huo na kusisitiza kwamba mechi zote za Ligi Kuu Bara msimu huu ni ngumu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >